# WINGILUGHA NA ATHARI ZAKE KATIKA UTEKELEZAJI WA MAENDELEO KAUNTI YA MACHAKOS, KENYA

**WILLINGTON KILONZO PETER**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA LUGHA NA FASIHI, KITIVO CHA ELIMU NA SAYANSI ZA JAMII KWA MINAJILI YA KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA KUTUZWA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA MARAFIKI CHA KAIMOSI**

**2022**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu asili na haijawahi kuwasilishwa kwa ajili ya shughuli yoyote ile wala kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote kile.

………………………. ……………………

DGS/EDK/G/0002/2019 Tarehe

## IDHINI

Tasnifu hii imewasilishwa kwa ajili ya kutahiniwa kwa ridhaa yetu tulioteuliwa rasmi kama wasimamizi na Chuo Kikuu cha Marafiki cha Kaimosi

………………………………. …..…………………

Dkt. Nabeta Sangili Tarehe

Idara ya Lugha na Fasihi

Chuo Kikuu cha Marafiki cha Kaimosi

…………………………. ....…………………

Dkt. Solomon Aunga Tarehe

Idara ya Lugha na Fasihi

Chuo Kikuu cha Marafiki cha Kaimosi

# IKISIRI

Kila lugha ina mchango wake katika maendeleo na wingilugha unaweza kuathiri maendeleo kwa njia chanya au hasi. Utafiti huu uliongozwa na madhumuni matatu: kuchanganua ruwaza za matumizi ya lugha katika Kaunti ya Machakos, kutathmini uhusiano na athari za lugha mbalimbali katika utekelezaji za maendeleo na kutambua nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha mahsusi za kuundia na kuwasilishia sera za maendeleo katika Kaunti ya Machakos. Msingi wa kifalsafa wa utafiti huu ulijengwa na nadharia mbili; Kiunzi cha Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi na Nadharia ya Utendaji Razini. Ili kufikia lengo hili, utafiti huu ulitumia muundo mseto huku muundo afikivu mseto ukitumika kufasili data za kitaamuli na zile za kitakwimu. Sampuli ya utafiti huu ilihusisha watafitiwa 146; wananchi 142 kutoka kwa vijiji sita vilivyotabakishwa na waundaji sera wanne kutoka kwa idara nne lengwa. Kwa msingi kuwa huu ni utafiti mseto, uchunguzi huu ulitumia mbinu nasibu na zisizonasibu za usampulishaji. Usampulishaji utabakishaji sinasibu ulitumika kuteua vijiji lengwa sita huku usampulishaji nasibu sahili ukitumika kuteua kadiri ya asilimia ya sampuli ya kila kijiji. Mbinu ya usampulishaji kimakusudi ilitumika kuteua viongozi wa idara nne lengwa. Utafiti huu ulitumia vifaa vya hojaji funge na nusu-funge, dodoso nusu-funge, mwongozo wa uchunzaji na kiunzi cha kuchanganulia nyaraka zilitumika kukusanya data. Zanatepe ya Kichanganuzi Data za Kitakwimu za Sayansi Jamii ilitumika kuchanganua data za kitakwimu huku uchanganuzi kidhamira ukitumika kuchanganua data za kitaamuli. Ili kuhakikisha uthabiti na uhalali wa utafiti na vifaa vya ukusanyaji data, utafiti wa majaribio ulifanywa katika eneo la Kitengela na uhalali wa maudhui kufanywa kwa vifaa husika mtawalia. Matokeo yalionyesha kuwa katika maeneo vizingasifa ya mashinani, lugha ya Kikamba na mseto wa Kikamba na Kiswahili ni maarufu zaidi huku lugha za Kiingereza na Kiswahili zikiwa maarufu zaidi katika maeneo vizingasifa ya mjini na kuwa zina athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo katika maeneo husika. Mielekeo chanya kwa lugha ya Kikamba katika maeneo ya mashinani yalichangia matumizi mapana ya lugha hii. Kwa jumla, matokeo yalionyesha kuwa wingilugha una athari chanya au hasi kwa utekelezaji wa maendeleo kulingana na jinsi lugha husika zinavyotumika katika mawanda mbalimbali. Matokeo ya utafiti huu yatawasilishwa kwa waundaji sera wa Kaunti ya Machakos ili kuwaarifu kihakikifu vigezo sahihi vya uteuzi wa lugha katika mchakato wa kuunda na kuwasilisha sera za maendeleo kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa maendeleo. Matokeo haya pia yatairutubisha taaluma ya isimujamii.

**ABSTRACT**

Every language has its contribution towards development implementation, and multilingualism can positively or negatively affect development implementation. This study was guided by three research objectives: to analyze patterns of language use, evaluate the relationship and the effects of various languages to development implementation, and determine the contribution of attitudes in the selection of specific languages of formulating and presenting development policies in Machakos County. The philosophical foundation of this inquiry was based on two theories: Language and Socio-Economic Development Theoretical Framework founded and the Theory of Reasoned Action. To achieve this goal, this investigation embraced a mixed research method with concurrent research design being used to triangulate the quantitative and the qualitative research. The study's sample size included 146 respondents: 142 sampled from the six stratified villages and four policy developers from the four targeted departments. Premised on the fact that this is a mixed research, this inquiry used both the probability and non-probability sampling. Simple Stratified Sampling technique was used to successfully sample the targeted six villages while simple random sampling was used to sample the respective percentage of respondents from each village. Finally, purposive sampling was used to select four heads of the targeted departments. Moreover, this research used structured and semi-structured questionnaires, semi-structured interviews, observation, and development-related document analysis methods to collect data. The SPSS software was used to analyze the quantitative data while thematic analysis was employed to analyze the qualitative data. To ascertain the reliability and validity of the study and its instruments, a pilot study was conducted in Kitengela area and content validity done on the data collection tools respectively. The findings show that among rural boundaries, Kikamba and a combination of Kiswahili and Kikamba are the most popular while English and Kiswahili are most popular in urban boundaries and that they affect the development implementation positively in these areas. Positive attitudes towards Kikamba in the rural areas resulted to its expansive use. Generally, the findings show that multilingualism has positive and negative effects on the development implementation depending on how the respective languages are used in different contexts. The research findings will be presented to the Machakos County Government's policy developers to objectively inform them on the most effective language selection criteria in the process of formulating and presenting development policies with a view of enhancing development implementation. The findings will also enrich the sociolinguistics discipline.

## YALIYOMO

**UNGAMO** ... ii
**IDHINI** ... ii
**IKISIRI** ... iii
**ABSTRACT** ... iv
**ORODHA YA VIFUPISHO** ... viii
**ORODHA YA VIAMBATISHO** ... ix
**UFAFANUZI WA ISTILAHI** ... x
**SURA YA 1** ... 1
**UTANGULIZI** ... 1
1.1. Usuli wa Mada ... 1
1.2. Suala la Utafiti ... 3
1.3. Madhumuni ya Utafiti ... 4
1.4. Maswali ya Utafiti ... 4
1.5. Sababu za Uteuzi wa Mada ... 5
1.6. Upeo na Mipaka ya Utafiti ... 7
1.7. Umuhimu wa Utafiti ... 8
1.8. Misingi ya Kinadharia ... 9
1.8.1. Kiunzi cha Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi. ... 10
1.8.2. Nadharia ya Utendaji Razini ... 14
**SURA YA 2** ... 17
**UHAKIKI WA MAANDISHI** ... 17
2.1. Utangulizi ... 17
2.2. Ruwaza za Matumizi ya Lugha ... 17
2.3. Uhusiano Uliopo Kati ya Lugha Mbalimbali na Athari zake Katika Utekelezaji Maendeleo ... 22
2.4. Nafasi ya Mielekeo katika Uteuzi wa Lugha ... 28
2.5. Pengo la Kimaarifa ... 31
**SURA YA 3** ... 33
**MBINU NA NJIA ZA UTAFITI** ... 33
3.1. Muundo wa Utafiti ... 33
3.2. Mahala pa Utafiti ... 33
3.3. Idadi Lengwa ... 33
3.4. Sampuli na mbinu za Usampulishaji ... 35
3.5. Mbinu za Ukusanyaji Data ... 37
3.6. Vifaa vya Ukusanyaji Data ... 38
3.6.1. Hojaji ... 38

3.6.2. Dodoso ..... 39
3.6.3. Mwongozo wa Uchunzaji ..... 39
3.6.4. Kiunzi cha Kukusanya Data kutoka kwa Nyaraka ..... 39
3.7. Uthabiti na Uhalali wa Vifaa vya Utafiti ..... 40
3.7.1. Uthabiti ..... 40
3.7.2. Uhalali ..... 41
3.8. Vikwazo wa Utafiti ..... 41
3.9. Upangaji, Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data ..... 42
3.9.1. Upangaji Data ..... 42
3.9.2. Uchanganuzi wa Data za Kitakwimu ..... 42
3.9.3. Uchanganuzi wa Data za Kitaamuli ..... 43
3.9.4. Uwasilishaji wa Data ..... 43
3.9.5. Ufasili wa Data za Utafiti ..... 43
3.10. Maadili katika Utafiti ..... 44
**SURA YA 4 ..... 45**
**UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO ..... 45**
4.0 Utangulizi ..... 45
4.1 Takwimu za Kimsingi za Utafiti ..... 45
4.2 Nduni za Kidemografia za Watafitiwa ..... 47
4.2.1 Jinsia ..... 47
4.2.2 Umri ..... 48
4.2.3 Kiwango cha Elimu ..... 49
4.2.4 Kazi Wanayoifanya Watafitiwa ..... 50
4.3 Ruwaza za Matumizi ya Lugha Katika Kaunti ya Machakos. ..... 51
4.3.1 Sokoni ..... 52
4.3.2 Nyumbani ..... 56
4.3.3 Hospitalini ..... 59
4.3.4 Shambani ..... 62
4.3.5 Kazini ..... 65
4.3.6 Mikutano ya Michakato ya Maendeleo ..... 68
4.3.7 Mafunzo ya Kilimo ..... 72
4.3.8 Biashara ..... 74
4.4. Uhusiano na Athari za Lugha Mbalimbali kwa Utekelezaji wa Maendeleo ..... 77
4.4.1 Matumizi ya Lugha Miongoni mwa Viongozi ..... 77
4.4.2 Lugha Pendwa za Wananchi za Kuelezea Masuala ya Maendeleo ..... 81
4.4.3 Lugha Pendwa katika Usomaji wa Nyaraka za Maendeleo ..... 86

4.4.4 Idadi ya Lugha Wanazozungumza Watafitiwa ................................ 90
4.4.5 Athari za Lugha Mbalimbali kwa Utekelezaji wa Maendeleo. ........ 94
4.5 Nafasi ya Mielekeo katika Uteuzi wa Lugha. ...................................... 101
4.5.1 Lugha ya Kwanza ni Bora Kuleta Maendeleo katika Nyaraka za Maendeleo ........................................................................................ 101
4.5.2 Istilahi za Lugha ya Kiswahili Huifanya kuwa Ngumu ................ 105
4.5.3 Natumia Lugha ya Kwanza Zaidi.................................................. 108
4.5.4 Ninapendelea Viongozi Wakitumia Kiingereza............................ 111
4.5.5 Ninatumia Kiswahili na Watu wa Jamii Nyingine......................... 112
4.6 Hitimisho.............................................................................................. 114
**SURA YA 5.......................................................................................... 115**
**MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........................ 115**
5.1 Utangulizi.............................................................................................. 115
5.2 Muhtasari .............................................................................................. 115
5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ......................................................... 115
5.3.1 Ruwaza za Matumizi ya Lugha ..................................................... 115
5.3.2 Uhusiano na Athari za Lugha Mbalimbali kwa Utekelezaji wa Maendeleo ........................................................................................ 117
5.3.3 Nafasi ya Mielekeo Katika Uteuzi wa Lugha ............................... 118
5.4 Mahitimisho .......................................................................................... 119
5.4.1 Ruwaza za Matumizi la Lugha...................................................... 119
5.4.2 Uhusiano na Athari za Lugha Mbalimbali kwa Utekelezaji wa Maendeleo ........................................................................................ 120
5.4.3 Nafasi ya Mielekeo katika Uteuzi wa Lugha. ............................... 120
5.5 Mapendekezo ........................................................................................ 121
5.5.1 Mapendekezo kwa Kaunti ya Machakos....................................... 121
5.5.2 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye ............................................ 121
**MAREJELEO ....................................................................................... 122**
**VIAMBATISHO .................................................................................. 128**

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| Kiing | : Kiingereza |
| Kik | : Kikamba |
| Kisw | : Kiswahili |
| LINEE | : Languages in a Network of European Excellence |
| N | : Nakubali |
| NK | : Nakubali Kabisa |
| S | : Sikubali |
| SH | : Sina Hakika |
| SK | : Sikubali Kabisa |
| SPSS | : Statistical Package for Social Science |

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho 1 A: Hojaji Funge.................................................................. 128
Kiambatisho 1 B: Hojaji Nusu-funge.......................................................... 131
Kiambatisho 2: Dodoso................................................................................. 133
Kiambatisho 3: Mwongozo wa Uchunzaji ..…………………………………...135
Kiambatisho 4: Kiunzi Cha Uchanganuzi Wa Nyaraka ................................ 136
Kiambatisho 5: Ramani ya Kaunti ya Machakos …………………….………..137
Kiambatisho 6: Mahojiano na Afisa Mkuu Idara ya Utamaduni…………….…..138
Kiambatisho 7: Mahojiano na Afisa Mkuu Kitengo cha Mimea……….….. 141
Kiambatisho 8: Mahojiano na Afisa Mkuu Idara ya Biashara …………….. 144
Kiambatisho 9: Mahojiano, Afisa Mkuu Idara ya Nyumba na Ukuaji wa Miji ……………………………………………………………………………147
Kiambatisho 10: Nyaraka ya Maelekezo ya Kilimo kwa Kiingereza na Kiswahili..........................................................................................................150
Kiambatisho 11: Nyaraka ya Maelekezo ya Kilimo kwa Kiingereza na Kiswahili……………………………………………………………….…...151
Kiambatisho 12: Nyaraka ya Maelekezo ya Kilimo kwa Kiswahili na picha……………………………………………………………………………152
Kiambatisho 13: Nyaraka ya Maelekezo ya Kilimo kwa Kiswahili……….. 153
Kiambatisho 14: Idhini ya chuo ……......……………………………………...154
Kiambatisho 15: Idhini ya NACOSTI ……………………………..……..155
Kiambatisho 16: Idhini ya Kaunti ya Machakos …………………….……..... 156

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

| | |
|---|---|
| Athari | Matokeo hasi au chanya yanayopatikana katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo Kaunti ya Machakos kwa mujibu wa data za maendeleo kutokana na kutumia au kutotumia lugha. |
| Nduni za kidemografia | Sifa maalumu za watafitiwa au vitafitiwa |
| Maendeleo | Upunguzaji wa umaskini kutokana na uongezekaji wa kiwango cha mapato cha wakaazi wa Kaunti ya Machakos kama matokeo ya matumizi ya lugha mbalimbali katika mchakato wa kutekeleza maendeleo. |
| Mdafao | Idadi ya utokeaji wa jibu maalum miongoni mwa watafitiwa au vitafitiwa. |
| Mielekeo | Miegemeo ya kisaikolojia au mitazamo ya kiakili ya watafitiwa kuhusu lugha mbalimbali zinazounda wingilugha katika Kaunti ya Machakos |
| Muundo wa kitaamuli | Muundo wa utafiti uliokusanya data zilizolenga kutambua sifa za watafitiwa au vitafitiwa. |
| Vizingasifa | Maeneo ya mipakani yanayounganisha Kaunti ya Machakos na kaunti nyingine zenye kutumia lugha tofauti na ya Kikamba. |
| Wingilugha | Matumizi ya lugha zaidi ya mbili katika Kaunti ya Machakos |

# SURA YA 1

# UTANGULIZI

## 1.1. Usuli wa Mada

Katika dunia ya leo, maingiliano kati ya watu wa asili tofautitofauti hayawezi kuepukika kutokana na kupanuka kwa shughuli za kikazi, kielimu, kijamii na kibiashara. Hivyo ndivyo yalivyo maingiliano ya lugha. Crystal (2010) anahoji kuwa mtagusano wa lugha, katika dunia iliyo na takriban lugha elfu tano, hauna budi kutokea katika kiwango cha kijamii na cha kitaifa. Awali, barani Afrika maingiliano yalikuwa miongoni mwa Waafrika wenyewe kwa wenyewe na hasa wale waliokuwa katika eneo moja kijiografia kutokana na ufinyu wa mbinu za usafiri na mawasiliano. Katika Afrika Mashariki, hali ya maingiliano ilikuwa hii katika zama hizo za kale. Shughuli tofautitofauti zilianza kupanua mtagusano baina ya watu wa jamii tofauti na mojawapo ni ujio wa wafanyibiashara katika pwani ya Afrika Mashariki na baadaye ujio wa wakoloni. Kadri maingiliano yalivyozidi kuongezeka ndivyo lugha ilivyozidi kuathiriwa, hali iliyopelekea kuzaliwa kwa uwililugha na baadaye wingilugha. Uwililugha ulitokana na shughuli za kibiashara katika Pwani ya Afrika Mashariki zilizosababisha kuzaliwa kwa Kiswahili. Baadaye, ujio wa wakoloni, ambao walikuja na lugha zao, ulizaa wingilugha ambako lugha asilia za Waafrika, lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza zilitumika katika mazingira sawia. Hali hii inashabihiana na maoni ya Frawley (2003) ambaye anasema kwamba uwililugha na wingilugha hutokana na mtagusano wa lugha katika jamii. Nchini Kenya shughuli za biashara na ukoloni zilizaa wingilugha. Katika mazingira ya wingilugha, ruwaza za matumizi ya lugha husika hutofautiana kutegemea mawanda ambamo lugha husika zinazungumzwa (Wamalwa na Wenzake, 2019).

Lugha ni sehemu muhimu sana ya utamaduni wa jamii zote ulimwenguni. Katika kila jamii, lugha huwa ni msingi wa kuendesha harakati za kubuni na kuendeleza amali kama vile biashara (Kawonga, 2019). Hii ina maana kwamba, bila lugha itakuwa vigumu sana kuendeleza shughuli zozote katika jamii. Kawonga (2019) anaendelea kusema kuwa 'lugha huteuliwa kuwa mtaji kwa lengo la kupata faida katika harakati za kiuchumi' (263). Maoni haya yanaonyesha umuhimu wa lugha katika harakati za uchumi na maendeleo kwa jumla. Pendakur na Pendakur (2015) wanasisitiza msimamo huu kwa kuandika kuwa lugha ni rasilimali muhimu katika maendeleo. Katika muktadha wa wingilugha, kila lugha inayozungumzwa huwa na manufaa yake katika jamii. Hata hivyo, watafiti hawa wanaonya kwamba lugha inaweza pia kutumika vibaya hasa pale ambapo inatumika kama kigezo cha kutambua watu wa eneo fulani na wale wasio wa eneo fulani katika maswala ya ajira. Hivyo basi, pale ambapo wingilugha unatumika vizuri, utekelezaji wa maendeleo ya kiuchumi na kijumla huathirika kwa hali chanya.

Mielekeo bayana ya lugha hujitokeza katika mazingira ya wingilugha kuhusu kila mojawapo ya lugha inayozungumzwa katika jamii husika kama anavyosema Batibo (2005) katika Kamau (2015). Ajzen na Fishbein (1980) wanafafanua mielekeo kama uwezo wa kuitikia ama vizuri au vibaya kwa kitu, mtu, taasisi au tukio. Hivyo, mielekeo ya lugha ni uwezo wa watu kuitikia ama vizuri au vibaya kwa lugha fulani. Kaunti ya Machakos ina wingilugha kwa sababu lugha za Kiingereza, Kiswahili, Kikamba na lugha nyingine za mama huzungumzwa na hivyo mielekeo ya lugha lazima iwepo. Hata hivyo, hali ya ruwaza za matumizi ya lugha hizi na uhusiano na athari za lugha husika kwa utekelezwaji wa maendeleo havijatafitiwa. Zaidi, nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha ya

kutumiwa katika kuunda na kusambaza sera za maendeleo ni jambo ambalo halijachunguzwa pia. Utafiti huu ilichunguza wingilugha na athari zake katika utekelezaji wa maendeleo Kaunti ya Machakos.

### 1.2. Suala la Utafiti

Kaunti ya Machakos, kama lilivyo taifa la Kenya na ulimwengu wote kwa jumla, inaathiriwa kwa kasi na hatua kubwa za maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano, biashara na teknolojia ya usafiri. Athari hizi zinazidi kusababisha wingilugha dhahiri kutokana na mtagusano wa lugha mbalimbali kijamii na kitaifa. Katika mazingira ya wingilugha, ruwaza za matumizi ya lugha huchukua mikondo tofauti katika mawanda mbalimbali kwa sababu kila lugha huwa na nafasi yake katika maendeleo ya kiuchumi, kielimu, kibiashara na hata kijamii kutokana na tofauti za kiisimujamii. Katika diskosi ya haki za kibinadamu, wingilugha hulenga kuleta usawa wa lugha zote tofauti lakini pragmatiki ya kiuchumi hupendelea lugha moja au muungano wa lugha maalumu ili kufanikisha malengo ya kiuchumi. Tatizo la lugha ipi au zipi zitumike katika muktadha wa utekelezaji maendeleo linazuka hasa katika maeneo ya mijini na katika maeneo vizingasifa kuliko na watu wa jamii tofautitofauti. Hivyo, katika mazingira haya, wingilugha huathiri maendeleo ama kwa hali chanya au hasi.

Ukosefu wa sera ya lugha ya kitaifa unaongeza uzito tatizo hili kwa kuwa hakuna maelekezo ya namna ya kutumia lugha katika viwango vya kitaifa na kaunti. Wananchi na washikadau wengine wakiwepo waundaji sera za maendeleo hulazimika kuchagua lugha ya kutumia katika masuala ya maendeleo kwa kuzingatia sababu tofauti. Hivyo, kutokana na uhuru huu wa uteuzi wa lugha, mielekeo huzaliwa na kuchukua nafasi kubwa hivi kwamba kila mwananchi na

kila muundaji sera atakuwa na mielekeo tofauti kuhusu lugha tofauti katika mazingira haya ya wingilugha kwa sababu mbalimbali. Hivyo, kutokana na mielekeo hii ya lugha, uteuzi wa lugha ya kutumiwa katika mchakato wa utekelezaji maendeleo katika wingilugha huu utaweza kuathiri utekelezaji huu kwa njia tofauti.

### 1.3. Madhumuni ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza jinsi wingilugha unavyoathiri utekelezaji wa maendeleo katika Kaunti ya Machakos. Ili kufikia lengo kuu hili, madhumuni yafuatayo yaliongoza utafiti huu;

i. Kuchanganua ruwaza za matumizi ya lugha katika Kaunti ya Machakos.
ii. Kutathmini uhusiano na athari za lugha mbalimbali katika utekelezaji wa maendeleo Kaunti ya Machakos.
iii. Kutambua nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha mahsusi za kuundia na kuwasilishia sera za maendeleo katika Kaunti ya Machakos.

### 1.4. Maswali ya Utafiti

Maswali yafuatayo yalitumika katika kuendeleza shughuli za ukusanyaji data za utafiti huu;

i. Je, kuna ruwaza zipi za matumizi ya lugha katika Kaunti ya Machakos?
ii. Lugha husika zinahusiana na kuathiri utekelezaji wa maendeleo vipi katika Kaunti ya Machakos?
iii. Je, mielekeo ina nafasi gani katika uteuzi wa lugha mahsusi ya kuundia na kuwasilishia sera za kimaendeleo katika Kaunti ya Machakos?

### 1.5. Sababu za Uteuzi wa Mada

Kwanza, mada ya utafiti huu iliteuliwa kutokana na ukosefu wa utafiti wa ruwaza za matumizi lugha katika Kaunti ya Machakos na mchango wa kila lugha husika katika utekelezaji wa maendeleo kaunti hiyo. Hakuna utafiti wowote ambao umefanywa unaochunguza suala hili na hivyo kusababisha uteuzi wa mada. Lengo la uteuzi huu lilikuwa kutafiti na kuchunguza ruwaza za matumizi ya lugha ndani ya wingilugha katika Kaunti ya Machakos na athari zake katika utekelezaji wa maendeleo katika kaunti hiyo.

Mada hii iliteuliwa pia kufuatia matokeo ya tafiti tofautitofauti kuwa kila lugha huwa na nafasi yake maalumu katika maendeleo ya jamii husika (Kawonga, 2019). Jain (2011) akinukuliwa na Kawonga (2019) anafafanua kuwa lugha ni sifa ya kijamii yenye umuhimu bia katika kuamua matokeo ya kiuchumi. Anachosema Jain hapa ni kuwa lugha ina nafasi kubwa katika uzalishaji wa raslimali na ujenzi wa uchumi. Kutokana na haya, mtafiti aligundua kuwa kila lugha na kila ruwaza inayotumiwa katika Kaunti ya Machakos ina uhusiano wa kiwango fulani na utekelezaji wa maendeleo katika kaunti hiyo na hivyo kulenga kutambua uhusiano huu.

Aidha, suala la mielekeo ya lugha katika mazingira ya uwililugha na wingilugha haliwezi kuepukika. Nyandwaro (2015) akimnukuu Ting (2003), anaandika kuwa mielekeo bayana hujitokeza katika miktadha iliyo na lugha mbili au zaidi. Hata hivyo mielekeo husika itaendana na mchango wa lugha maalumu katika kufikia malengo ya wanajamii. Hivyo, utafiti huu ulitamatisha kuwa mielekeo katika mazingira ya wingilugha ina nafasi katika uteuzi wa lugha ya au za

kuundia na kuwasilishia sera za kimaendeleo, jambo lililopelekea mada hii kuteuliwa.

Kaunti ya Machakos iliteuliwa kwa sababu tatu kuu. Kwanza, lugha ni sehemu ya utamaduni wa jamii yoyote na hivyo ili kuchunguza lugha lazima mtafiti auelewe utamaduni wa jamii husika. Mtafiti katika utafiti huu anauelewa utamaduni wa jamii inayoishi katika kaunti hii na hivyo kupelekea kuteuliwa kwa kaunti hiyo. Pili, hali halisi ya Kaunti ya Machakos inalingana na pendekezo la matumizi ya fomyula ya lugha tatu ya Walsh (2006) kama mojawapo ya suluhu kwa matatizo yanayokumba maeneo yenye wingilugha. Fomyula hii inapendekeza matumizi ya lugha ya kimataifa, lingua franka ya kitaifa na lugha asili katika maeneo yenye wingilugha kama njia ya kuhakikisha maendeleo. Katika Kaunti ya Machakos, Kiingereza kinachukua nafasi ya lugha ya kimataifa, Kiswahili kinachukua nafasi ya lingua franka ya kitaifa huku Kikamba, Kimaasai, Kikikuyu, Kiembu, na lugha nyingine za kwanza zikichukua nafasi ya lugha asili katika mchakato wa utekelezaji maendeleo. Pia, ni kaunti iliyo na wingilugha ulio bayana kutokana na uwepo wa watu kutoka jamii mbalimbali hasa mjini Machakos na katika maeneo vizingasifa. Vizingasifa hivi, kama inavyoonyeshwa na Kiambatisho 5, ni upande wa Kusini Magharibi ambapo inapakana na Kaunti ya Kajiado (jamii ya Wamaasai), upande wa Kaskazini inapakana na Kaunti ya Embu (jamii ya Waembu), upande wa Kaskazini Magharibi inapakana na Kaunti ya Muranga (jamii ya Wagikuyu), na upande wa Magharibi inapakana na Kaunti za Nairobi na Kiambu (jamii ya Wagikuyu na nyinginezo) (Machakos County, 2022). Vilevile, wingilugha huu unaimarishwa zaidi na ujirani na Mji wa Nairobi, ambao kama Kamau (2015) anavyokiri kuwa hujumuisha wazungumzaji wa takriban lugha zote

zinazozungumzwa nchini Kenya, hali inayotofautisha kaunti hii na za Kitui na Makueni.

### 1.6. Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika Kaunti ya Machakos, ambayo ni mojawapo ya kaunti arobaini na saba za taifa la Kenya chini ya katiba ya 2010. Kwa kuwa unahusiana na wingilugha na athari zake katika utekelezaji wa maendeleo ya kaunti hiyo, utafiti ulifanyika katika maeneo vizingasifa ya kaunti hii pamoja na mjini Machakos ambapo ndipo makao makuu ya Serikali ya Kaunti ya Machakos na ni eneo lenye wingililugha dhahiri. Sababu kuu ya eneo hili kuteuliwa ni kwa sababu lugha ni sehemu ya utamaduni wa jamii na mtafiti anauelewa utamaduni wa jamii inayoishi katika kaunti hii. Utafiti huu ulihusisha uchunguzi wa wingilugha na athari zake kwa utekelezaji wa maendeleo katika Kaunti ya Machakos ambapo uliangazia maendeleo ya kiuchumi. Suala hili liliangaziwa kwa sababu wingilugha unaendelea kukua kila uchao kutokana na kuongezeka kwa maingiliano miongoni mwa watu wa tamaduni tofautitofauti wanaozungumza lugha tofauti. Vilevile, lugha yoyote ile huathiri utekelezaji wa maendeleo ya kiuchumi ya maeneo inamozungumzwa. Utafiti huu uliangazia lugha kama kigezo kimoja tu kati ya vigezo vingine muhimu katika utekelezaji wa maendeleo.

Utafiti huu ulihusisha watafitiwa tofautitofauti ambao ni pamoja na wasimamizi wanne wa idara lengwa ambao huanzisha mchakato wa maendeleo kwa kuunda sera na kuziwasilisha kwa utawala na wananchi. Data zilizotolewa na wasimamizi hawa zilisaidia pakubwa kujibu maswali ya utafiti huu. Baada ya sera za kimaendeleo kuundwa huwasilishwa kwa wananchi ili kuzitekeleza.

Hivyo, utafiti huu ulihusisha wananchi wanaoishi katika maeneo vizingasifa na wale wa mjini Machakos ili kukadiria jinsi wingilugha unavyoathiri utekelezaji wa maendeleo katika kaunti hiyo. Pia utafiti huu ulitambua nafasi ya mielekeo ya watafitiwa katika uteuzi wa lugha ya kutumia katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo.

### 1.7. Umuhimu wa Utafiti

Kothari na Garg (2019) wanadai kuwa utafiti hutoa msingi kwa takriban sera zote za serikali ndani ya mfumo wake wa kiuchumi. Kauli hii inaonyesha ukweli wa utafiti huu. Kwanza, katika Kaunti ya Machakos, na Kenya kwa ujumla, hakuna sera inayoelekeza namna ya kutumia lugha katika muktadha wa maendeleo. Matokeo ya utafiti huu yatawasilishwa kwa waundaji sera wa Kaunti ya Machakos ili kusaidia uundaji wa sera zinazohusiana na masuala ya lugha na maendeleo katika viwango vya kaunti.

Pia, tafiti ambazo zimefanywa kuhusu wingilugha na maendeleo zimefanywa katika mataifa ya nje ya Kenya kama vile India (Pattanayak, 2015), Afrika Kusini (Rassool na wenzake, 2006), Nigeria (Abiodun, 2013) na nyinginezo. Hata hivyo, hakuna utafiti wowote ambao umefanywa katika Kaunti ya Machakos na hata nchini Kenya kwa jumla kuhusu suala hili. Ukosefu huu wa utafiti unaohusiana na wingilugha na utekelezaji wa maendeleo nchini Kenya ulichangia pakubwa katika uteuzi wa mada ya utafiti huu ili kutathmini athari za wingilugha katika utekelezaji wa maendeleo Kaunti ya Machakos iliyo nchini Kenya.

Aidha, utafiti huwa ni nguzo muhimu na ndio msingi wa elimu. Utafiti huu umekuwa wa muhimu katika taaluma ya Isimujamii kwa sababu umerutubisha

taaluma hii kwa kuonyesha uhusiano uliopo kati ya wingilugha na utekelezaji wa maendeleo. Zaidi, utafiti huu ulifanywa kwa lugha ya Kiswahili ambayo haijatumika sana katika tafiti za wingilugha na maendeleo kama zilivyo na lugha nyingine kuu kama vile Kiingereza na Kihispania.

Suala la lugha ya kutumia katika miktadha ya kaunti pia limekuwa suala nyeti katika taifa la Kenya. Viongozi mbalimbali wamekuwa na maoni mbalimbali kuhusu lugha gani ya kutumiwa katika viwango vya kaunti. Kiongozi wa upinzani wa wakati huo, Raila Odinga, akizungumzia suala hili alipendekeza lugha za kwanza kutumika katika miktadha ya mabunge ya kaunti (Nation, 2015), jambo ambalo lilipokelewa kwa hisia mseto na viongozi. Hata hivyo mswada huu haujaendelezwa na yeyote na hivyo matokeo ya utafiti huu yatasaidia katika kutambua suala la lugha ipi au zipi zinazopendelewa katika muktadha wa Kaunti ya Machakos.

### 1.8. Misingi ya Kinadharia

Nadharia mbili zilitumika katika utafiti huu kuongoza na kuelekeza shughuli za ukusanyaji data, uchanganuzi na ufasiri wa data husika. Kwanza ni Kiunzi cha Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi kilichoasisiwa na John Walsh (2006) na pili ni Nadharia ya Utendaji Razini yao Ajzen na Fishbein (1980). Kiunzi chake John Walsh kilisaidia kuchanganua data zilizohusiana na madhumuni ya kwanza na ya pili. Hii ni kwa sababu lengo kuu la kiunzi hiki ni kuonyesha uhusiano wa lugha na maendeleo kwa kuonyesha jinsi lugha yoyote inavyoleta maendeleo katika sehemu mbalimbali za maisha ya wanadamu. Nadharia ya Utendaji Razini nayo ilisaidia katika kuchanganua data zilizolengwa na swali la tatu. Ilifaa zaidi kwa sababu kama Kavoi (2019)

anavyosema, lengo kuu la nadharia hii ni kuelezea uhusiano uliopo kati ya imani, mielekeo, tabiania na tabia yenyewe.

### 1.8.1. Kiunzi cha Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi.

Kiunzi hiki kiliasisiwa na John Walsh mwaka wa 2006. Lengo lake kuu lilikuwa ni kuchunguza nafasi ya lugha katika maendeleo na kuwezesha uunganishaji wa karibu wa taaluma za upangaji na sera ya lugha na maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Malengo yake yaliakisi hali halisi ya madhumuni ya kwanza na ya pili ya utafiti huu kwa sababu kwanza mojawapo ya mihimili yake ni wingilugha na maendeleo ambalo ndilo suala kuu la utafiti huu na pili kinaonyesha mchango wa lugha katika maendeleo. Walsh alikijenga kiunzi hiki katika msingi kuwa lugha huwa na jukumu katika maendeleo kutokana na athari yake katika uelewa. Walsh alirejelea wazo la Johann Gottfried Herder ambaye alidai kuwa kuna usambamba wa mawazo ya taifa na lugha yake. Kiunzi hiki cha kinadharia kilifaa utafiti huu zaidi kutokana na usambamba wa mihimili yake na utafiti huu kama ifuatavyo:

*1.8.1.1 Upangaji lugha na sera ya lugha huchangia maendeleo ya kielimu.*

Mhimili huu ulijengwa katika msingi wa ripoti ya Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) ya mwaka wa 1953. Ripoti hii ilionyesha kuwa mafunzo kwa lugha ya kwanza huchangia katika maendelezo ya vigezo vya kijamii, kitamaduni na kimaendeleo katika jamii. Katika utafiti huu, wapo watu ambao hushughulikia uundaji wa sera za kimaendeleo katika Kaunti ya Machakos. Hata hivyo, ili maendeleo lengwa yapatikane, ni sharti sera hizi zieleweke na wananchi ambao ndio walengwa wakuu wa sera husika. Jambo hili linalazimu uwasilishaji wa sera hizi kwa wananchi kutumia lugha. Kwa

mujibu wa nadharia hii, lugha ya kwanza huwa muhimu katika mafunzo yanayohusiana na maendeleo ya kijamii, kitamaduni na kimaendeleo. Hivyo, nadharia ilielekeza utafiti kutathmini nafasi na athari za lugha za kwanza kwa utekelezaji wa maendeleo katika Kaunti ya Machakos. Mhimili huu ulisaidia kuchanganua madhumuni ya pili kwa kuelekeza mtafiti katika kuchunguza uhusiano na athari za lugha ya kwanza na nyingine zinazounda wingilugha na elimu ya maendeleo ya uchumi katika Kaunti ya Machakos.

*1.8.1.2 Lugha na Maendeleo ya binadamu*

Mhimili huu ulijengwa kutokana na ripoti ya Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa ya mwaka 1990. Ripoti hii iliainisha vigeu vitatu vya kukadiria maendeleo ya binadamu. Vigeu hivi ni pamoja na elimu, miaka tarajiwa ya kuishi na kiwango cha mapato. Ripoti hii iligundua kwamba lugha ya binadamu ilikuwa kigezo cha msingi katika maendeleo haya. Mhimili huu pia umewekewa msingi katika utamaduni wa jamii husika. Lugha imeelezwa kama sehemu ya utamaduni wowote ule na huchangia katika kuumba na kuendeleza utamaduni. Ni katika msingi huu ambapo mhimili huu ulikuwa msingi mkubwa wa kuchanganua ruwaza za matumizi ya lugha zinazotumiwa katika Kaunti ya Machakos na wananchi ili kupata faida na mapato. Nafasi ya mhimili huu ilikuwa maalumu katika utafiti huu kwa sababu ulisaidia kuonyesha jinsi ruwaza mbalimbali za matumizi ya lugha zinavyosaidia utekelezaji maendeleo ya kiuchumi. Maendeleo haya yanayohusiana na kigeu cha kiwango cha mapato na faida kama sehemu muhimu ya uchumi wa watu wanaoishi katika kaunti hiyo.

*1.8.1.3 Wingilugha na Maendeleo*

Ripoti ya Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa mwaka wa 2004 iliendeleza suala la utamaduni kwa kuzingatia kigezo cha uhuru wa utamaduni. Ripoti hii ilionyesha kuwa uhuru wa watu wa utamaduni ni sehemu muhimu ya maendeleo ya binadamu pamoja. Ripoti hii pia ilibainisha nafasi ya uundaji wa sera za wingilugha katika maendeleo na tatizo la utekelezaji wa sera kwa mataifa yaliyo na sera za wingilugha. Kulingana na mhimili huu, wingilugha ni suala ambalo linaweza kuwa na athari chanya au hasi kutegemea jinsi wingilugha unavyotumika, jambo ambalo ndilo suala kuu la utafiti huu. Mhimili huu unapendekeza pia uendelezaji wa fomyula ya lugha tatu, yaani lugha ya kimataifa, lingua franka ya kitaifa na lugha asili ili kuhakikisha maendeleo ya eneo husika. Hali hii ya utatu lugha ya kiunzi hiki inaakisi hali ya eneo la utafiti huu ambamo lugha ya Kiingereza inachukua nafasi ya lugha ya kimataifa, lugha ya Kiswahili inachukua nafasi ya lingua franka ya kitaifa na lugha ya Kikamba inachukua nafasi ya lugha asili ya eneo hili. Hata hivyo, suala nyeti lilikuwa ni kutambua iwapo fomyula hii inasuluhisha matatizo ya wingilugha katika Kaunti ya Machakos. Hivyo, mhimili huu ukawa nguzo katika kuelekeza ukusanyaji na uchanganuzi wa data zilizolenga madhumuni ya kwanza na madhumuni ya pili. Mhimili huu ulisaidia utafiti huu katika kutambua jinsi fomyula hii ya lugha tatu ilivyoathiri utekelezaji wa maendeleo katika maeneo ya mjini na maeneo vizingasifa kuliko na wingilugha.

*1.8.1.4 Nafasi ya lugha katika mifumo ya ubunifu ya kitaifa*

Mhimili huu unashikilia kwamba utambulisho na umoja wa kitaifa ni muhimu katika kuanzisha na kuendeleza ubunifu na maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Mhimili huu umejengwa sana na Nadharia ya Mfumo wa Ubunifu wa Kitaifa

inayoshikilia kwamba kila taifa lina upekee wake maalumu. Hivyo, upekee wa matumizi ya lugha huwa na nafasi katika maendeleo. Kama ilivyo katika kiwango cha kitaifa, kila kaunti lazima iwe na utambulisho wake wa kiisimu, jambo ambalo ni sehemu ya wingilugha. Hivyo, mhimili huu unahusiana kwa karibu sana na madhumuni ya kwanza na pili ya utafiti huu. Njia mojawapo iliyotumika kukusanyaji data katika utafiti huu ilikuwa ni mahojiano na wasimamizi wa uundaji sera katika idara nne zinazohusiana kwa karibu na maendeleo ya kiuchumi ya Kaunti ya Machakos. Mhimili huu ulikuwa msingi mkubwa wa mahojiano haya kwa kuwa ulielekeza mahojiano haya katika juhudi za kutambua nafasi ya lugha mbalimbali katika mifumo ya ubunifu wa kiuchumi kupitia kwa uundaji wa sera za kimaendeleo na uwasilishaji wake kwa wananchi. Zaidi, utafiti huu ulitumia mhimili huu kama kigezo cha kukadiria upekee wa kiisimu wa Kaunti ya Machakos na jinsi lugha mbalimbali zinavyotumika katika kuanzisha na kuendeleza utekelezaji wa maendeleo.

Mbali na kuchanganua ruwaza za matumizi ya lugha katika Kaunti ya Machakos, utafiti huu ulitambua uhusiano na athari za lugha mbalimbali zinazounda wingilugha katika kaunti hii katika utekezaji wa maendeleo. Hata hivyo, ili kufafanua ruwaza husika za matumizi ya lugha na uhusiano uliopo kati ya lugha hizi na utekelezaji wa maendeleo, suala la mielekeo ya lugha liliangaziwa katika madhumuni ya tatu. Madhumuni haya yalidhamiria kutambua nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha mahsusi ya au za kuundia na kuwasilisha sera za kimaendeleo kwa wananchi ambao ndio walengwa wakuu na pia uteuzi wa lugha ya au za kutumia katika michakato ya utekelezaji wa maendeleo miongoni mwa wananchi. Hata hivyo, kiunzi hiki hakikuweza kushughulikia suala la mielekeo kama yalivyo madhumuni ya tatu. Upungufu huu wa kiunzi hiki cha

kinadharia ulisababisha kuhusishwa kwa Nadharia ya Utendaji Razini kama njia mbadala ya kupambanua mwelekeo kuhusu nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha.

### 1.8.2. Nadharia ya Utendaji Razini

Nadharia hii iliasisiwa na Ajzen na Fishbein mwaka wa 1980 kwa lengo la kueleza uhusiano uliopo kati ya imani, mielekeo, tabiania na tabia yenyewe (Kavoi, 2019). Nyandwaro (2015) anaiita nadharia hii Nadharia ya Vitendo Vilivyofikirika ambapo anaeleza kwamba inadai kuwa binadamu ni kiumbe mwenye urazini na anayeweza kutumia maarifa aliyo nayo kwa utaratibu. Hivyo, kwa mujibu wa nadharia hii, matendo ya mtu fulani huwa yameathiriwa na fikra zake. Fikra hizo nazo huathiriwa na mielekeo, imani na tabiania. Ukweli wa kauli hii ni maelezo ya Nyandwaro (2015) kuwa iwapo binadamu yeyote anafanya jambo litakalomnufaisha atakuwa na mtazamo kubalifu na iwapo jambo analolifanya halimnufaishi, basi atakuwa na mtazamo usiokubalifu. Kavoi (2019) naye anaunga mkono maoni haya ya Nyandwaro kwa kusema kuwa kiukulio muhimu cha kubashiri tabia ni nia au azma au kusudi la tabia husika. Nao Ajzen na Fishbein (1980), Fishbein na Middlestadt (1989) na Montano na Kasprzyk (2002) katika Kavoi (2019), wanaonyesha ukweli huu zaidi wanaposema kuwa kiukulio cha moja kwa moja ambacho hubashiri tabiania za watu ni mielekeo yao kuhusu kutenda tabia fulani, ikiendana sambamba na kanunibinafsi. Hivyo, nadharia hii ilielekeza utafiti huu katika kutambua mielekeo ya watafitiwa kuhusu lugha mbalimbali na nafasi ya mielekeo husika katika uteuzi wa lugha ya au za kutumia katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo. Ufaafu wa nadharia hii katika utafiti huu unaendana na ufumbuzi wa Montano na Kasprzyk (2002) kama anavyonukuliwa na Kavoi

(2019) kwamba nadharia hii ilifaulu kuelezea tabia katika mazingira ya uteuzi huru. Hii ni kwa sababu utafiti huu ulihusisha mazingira ambapo watafitiwa wana uhuru wa kuchagua lugha ya au za kutumia katika utekelezaji wa maendeleo. Mihimili ya nadharia hii ni kama ifuatavyo;

*1.8.2.1 Mielekeo ya Mhusika.*

Kavoi (2019) aliandika kuwa huu ndio mhimili mkuu wa nadharia hii ambao unahusisha tabiania ya mhusika ambapo akiwanukuu Fishbein na Ajzen (1980) anafafanua tabiania kama mizani ya kupima uwezekano wa mhusika kutekeleza kitendo kusudiwa. Nyandwaro (2015) naye anaeleza kwamba kwa mujibu wa nadharia hii, ijapokuwa yanaweza kuwepo matokeo yasiyotarajiwa, ni rahisi kutabiri tabia ya binadamu. Zaidi ya haya ni ufafanuzi wa Fishbein katika Kavoi (2019) kuwa nia au kusudi ni dhamira ya kutekeleza au kutenda kitendo ama tabia kusudiwa. Katika msingi huu, mielekeo katika nadharia hii huwa ni kiukulio muhimu cha kubashiri iwapo mhusika angetimiza kitendo fulani au la. Katika msingi huu, mhimili huu ulisaidia mtafiti kutambua na kuchanganua mielekeo ya wakaazi wa Kaunti ya Machakos na wasimamizi wa idara nne lengwa wanaounda sera za kimaendeleo za idara husika kuhusu lugha mbalimbali zinazounda wingilugha wa kaunti hiyo. Jambo hili ndilo linalolengwa na madhumuni ya tatu ya utafiti huu. Ili kutathmini nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha za kutumiwa katika mchakato wa kutekeleza maendeleo, kauli mbalimbali zilitumiwa katika hojaji (Viambatisho 1A na 1B). Katika Kiambatisho cha 1A watafitiwa walitakiwa kukubaliana au kutokubaliana na kauli husika zilizolenga kutambua mielekeo yao kuhusu lugha mbalimbali zinazounda wingilugha. Kwa msingi wa mhimili huu, majibu ya watafitiwa yalitumika kuonyesha uwezekano wa kutumia lugha lengwa katika

shughuli mbalimbali za kimaendeleo. Zaidi, ufumbuzi wa nafasi ya mielekeo ulisaidia kujenga msingi imara wa kuonyesha uhusiano na athari za lugha mbalimbali kwa utekelezaji wa maendeleo.

#### *1.8.2.2 Kanunibinafsi*

Nyandwaro (2015) aliandika kuwa nia au kusudi la mtu hutathminiwa kwa vipengele viwili vya kimsingi; kipengele cha nia yake kibinafsi na pili, ushawishi wa kijamii. Kipengele cha nia ya mtu binafsi huhusisha manufaa atakayoyapata kutokana na tabia, jambo ambalo linaathiri mwelekeo wake kuhusu tabia husika. Kipengele cha ushawishi wa kijamii nacho huhusisha ukubalifu au ukataaji wa tabia kutokana na ukubalifu wake na jamii. Kama Kavoi (2019) anavyohoji, mhimili huu hujikita katika ubinafsi wa mhusika na ushawishi wa wanaomzunguka. Kipengele cha ubinafsi wa mtafitiwa katika utafiti huu kilitumika kupima mielekeo ya wahusika katika kutathmini namna watafitiwa mbalimbali walivyoonelea manufaa ya lugha mbalimbali na vilevile ukosefu wa manufaa ya lugha nyingine. Kwa upande mwingine, ushawishi wa wanaowazunguka watafitiwa ulizingatiwa katika kujua nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha. Ijapokuwa lugha za Kiswahili na Kiingereza ni lugha rasmi ambazo zimekubalika na serikali ya Kenya chini ya Katiba ya 2010, utafiti huu ulitathmini pia ukubalifu wa lugha hizi na wananchi wa Kaunti ya Machakos. Ukubalifu huu wa lugha mbalimbali ulichunguzwa kwa mujibu wa viwango vyao vya elimu, umri, kazi wanazozifanya na hata jinsia. Hili lilisaidia kutambua nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha kwa mujibu wa vipengele hivi miongoni mwa watafitiwa hasa kutokana na majibu yao kuhusu maswali ya hojaji nusu-funge (Kiambatisho 1B) yaliyolengwa kupata maelezo ya mielekeo husika kuhusu lugha mbalimbali.

# SURA YA 2

# UHAKIKI WA MAANDISHI

## 2.1. Utangulizi

Sura hii inahakiki wa maandishi ambayo yamekwisha andikwa kutokana na tafiti zinazohusiana na mada ya utafiti huu ili kuonyesha pengo la kimaarifa ambalo utafiti huu ulinuia kuziba. Uhakiki huu ulifanywa kulingana na madhumuni ya utafiti huu. Ulianza kwa kuhakiki kazi ambazo zimefanywa kuhusu ruwaza za matumizi ya lugha katika hali ya wingilugha kama yalivyo madhumuni ya kwanza na kisha kufuatia uhakiki wa maandishi yanayohusiana na uhusiano na athari za lugha mbalimbali kwa utekelezaji wa maendeleo. Sura hii pia imehakiki maandishi yanayolenga mielekeo na nafasi yake katika uteuzi wa lugha ya kutumia katika miktadha mbalimbali ya maendeleo kama yalivyo madhumuni ya tatu ya utafiti huu. Mwisho, mtafiti ameonyesha pengo la kimaarifa ambalo tafiti ambazo zimehakikiwa zimewacha, jambo ambalo limethibitisha uhalali wa utafiti huu.

## 2.2. Ruwaza za Matumizi ya Lugha

Tafiti tofautitofauti zinaonyesha kwamba katika mazingira ya wingilugha, ruwaza za matumizi ya lugha huwa tofauti kutegemea mawanda husika. Sridhar (1996) anafafanua kuwa pale wingilugha unapoonekana kama jambo la kijamii, masuala ya kimsingi huwa ni sita. Masuala haya huhusisha hadhi na majukumu ya lugha husika katika jamii, mielekeo kuhusu lugha, viukulio vya uteuzi wa lugha, matumizi ya kiishara na ya kiutendaji ya lugha na mahusiano kati ya matumizi ya lugha na vipengele vya kijamii kama vile dini, hadhi na makabila. Uchunguzi wa LINEE (2010) nao unaoyesha kuwa wingilugha unastahili

kutumika kama njia ya kufikia ufanisi wa kiuchumi na hivyo ruwaza za matumizi ya lugha kutokea katika kila mazingira ya wingilugha. Hivyo, ruwaza za matumizi ya lugha hutofautiana katika mazingira ya wingilugha kama inavyodhihirika katika tafiti zifuatazo:

Kwanza ni utafiti wa Nursanti na wenzake (2020) uliochunguza Ruwaza za Matumizi ya Lugha miongoni mwa Wanafunzi wa Kiingereza wa Vyuo Vikuu wenye Wingilugha, nchini Indonesia. Utafiti wao ni elezi na ulitumia muundo mseto ambapo mbinu ya hojaji na mahojiano zilitumika kukusanya data lengwa. Data za kitakwimu zilichanganuliwa na zanatepe ya Kichanganuzi Data za Kitakwimu za Sayansi Jamii huku zile za kitaamuli zikichanguliwa kidhamira. Watafitiwa wa utafiti wao walihusisha wanafunzi 162 wa programu ya Fasihi ya Kiingereza, Kitivo cha Lugha na Sanaa wa mwaka wa 2015-2017 katika Chuo Kikuu cha Negeri Yogyakarta. Matokeo ya utafiti wao yalidundua kuwa ruwaza za matumizi ya lugha zilibadilika katika mawanda tofauti.  Katika mawanda ya nyumbani, wengi wa wanafunzi walitumia Kijavani kuwasiliana na wazazi, ndugu na dada zao, majirani wa umri mkubwa na watu wa rika yao. Kwa mujibu wao, chaguo hili hutokana na kuwa lugha hii ya Kijavani ni lugha yao ya mama na huwa na sifa ya kujamiiana. Wanafunzi walioishi vijijini, walitumia Kikrama, ambayo ni lahaja kolevu na kongwe ya Kijavani na wazazi na majirani wakongwe.

Katika maingiliano na wageni, ruwaza ya kutumia lugha ilibadilika kwa sababu Kibahasa cha Indonesia kilitumika kwa sababu wengi wa wageni ni washiriki wa mazungumzo ambao hawawajui au kwa sababu hawana hakika iwapo wanaweza kuzungumza Kijavani au la. Asilimia ndogo ya wanafunzi hata hivyo hutumia lugha hii kuwasiliana na jamaa zao kwa sababu pengine waliitumia

kutoka utotoni au mmoja wa wazazi wao si mzaliwa wa eneo la Java. Katika mawanda ya vyombo vya habari, asilimia kubwa ya wanafunzi hawa, japo ni wanafunzi wa Kiingereza, walitumia lugha ya Kibahasa cha Indonesia huku asilimia ndogo kabisa wakitumia lugha ya Kiingereza. Ruwaza ya matumizi ya lugha katika mawanda ya chuoni kwa mujibu wa matokeo yalitokea kuwa sawa na yale ya katika vyombo vya habari. Matumizi makubwa yalikuwa ya lugha ya Kibahasa cha Indonesia yakifuatiwa na ya Kiingereza kisha Kijavani. Hata hivyo, katika muktadha wa darasani, lugha ya Kiingereza hutumika zaidi ikilinganishwa na lugha hizi zingine. utafiti huu unalingana na utafiti huu kwa sababu tafiti zote zinahusiana na wingilugha, mielekeo na ruwaza za matumizi ya lugha katika mazingira ya wingilugha. Pia, utafiti wao ulitumia muundo mseto kama ulivyo utafiti huu. Hata hivyo, utafiti wao ulifanywa nchini Indonesia ilhali huu unafanywa nchini Kenya. Vilevile, utafiti wao ulihusisha wanafunzi wa chuo kikuu ilhali huu unahusisha wananchi wa jumla.

Kevogo na wenzake (2015) nao walichunguza Wingilugha na Ruwaza za Matumizi ya Lugha kwa kuangazia Mielekeo ya Wanafunzi kuhusu Kiswahili mjini Garissa, Kaunti ya Mandera nchini Kenya ambapo waliwalenga wanafunzi wa shule za upili. Watafiti hawa walikusanya data kutoka kwa wanafunzi 100 kutumia hojaji elekezi ambapo walitumia mbinu ya usampulishaji nasibu sahili kufikia idadi hii ya sampuli. Walikusanya data za kitakwimu na kuzichangua kiuelezi na kwa kutumia majedwali. Matokeo ya utafiti wao yanaonyesha kuwepo kwa ruwaza maalumu za matumizi ya lugha katika mawanda ya shuleni na nyumbani. Katika mawanda ya nyumbani, 100% ya wanafunzi waliotafitiwa walitumia Kisomali kuwasiliana na wazazi, huku Kisomali kikitumika na 95%

yao kuwasiliana na ndugu na dada zao. Vilevile, 100% yao walitumia lugha hii kuwasiliana na marafiki zao wakiwa nyumbani.

Hali ni tofauti katika mawanda ya shuleni kwa sababu 25% tu ndio waliokubali kutumia Kisomali kuwasiliana na wenzao, hali ambayo watafiti wanagundua kuletwa na sera ya lugha shuleni. Ruwaza ya matumizi ya msimbo wa Kiswahili na Kiingereza ilikuwa tofauti kabisa. Kwanza, lugha ya Kiswahili ilitumika zaidi (80%) katika mazungumzo na watu wa makabila mengine ikilinganishwa na 15% iliyotumia Kiingereza. Shuleni, 23% walitumia Kiswahili kuwasiliana na walimu wao huku 77% wakitumia Kiingereza kuwasiliana na walimu shuleni. Utafiti huu wa Kevogo na wenzake (2015), japo unalingana na huu kutokana na kushughulikia ruwaza za matumizi ya lugha katika wingilugha, unatofautiana na huu kwa njia mbili kuu. Kwanza, utafiti wao ulifanywa miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili, hali tofauti kabisa na huu uliohusisha wananchi kwa jumla wanaoishi katika maeneo yenye wingilugha dhahiri. Pili, utafiti wao ulifanywa katika Kaunti ya Mandera, ambalo ni eneo tofauti kabisa kijiografia na la utafiti huu uliofanywa Kaunti ya Machakos.

Wamalwa na wenzake (2019) nao walifanya uchunguzi uliolenga kutambua mielekeo ya lugha na ruwaza za matumizi ya lugha za walimu wa Kiswahili wa shule za msingi katika Kaunti ya Siaya. Katika utafiti wao, watafiti hawa wanakiri kuwa, kwanza, uchunguzi wa ruwaza za matumizi ya lugha ni msingi muhimu katika ufafanuzi wa hali ya lugha katika wakati maalumu na pili kuwa hutengeneza msingi wa kutabiri hali ya matumizi ya lugha katika siku za baadaye. Utafiti wao ulizingatia mawanda matatu katika kuchunguza ruwaza hizi: mandhari mahsusi, muungano wa nyakati bainifu na dhima za mawasiliano kama wanavyoinukuu misingi ya Nicolle (2019). Utafiti wao ulitambua ruwaza

mbalimbali za matumizi ya lugha katika shule za msingi za Kaunti ya Siaya. Katika mandhari rasmi, ruwaza ya mseto wa lugha za Kiswahili na Kiingereza ilitumika zaidi hivi kwamba 68% waliitumia katika gwaride, 50% waliitumia ofisini, 44% waliitumia walipowasiliana na walimu wenzao, 68% waliitumia walipowasiliana na wanafunzi na 44% kuitumia katika mikutano shuleni.

Ruwaza ya msimbo wa Kiswahili pekee ilitumika kwa kiwango cha chini kwa sababu 12% ya walimu waliitumia kwenye gwaride, 9% wakiitumia katika mawasiliano ya ofisini, huku 18% wakiitunia katika mawasiliano na walimu wenzao. Zaidi, 18% ya walimu waliwasiliana na wanafunzi wao kutumia Kiswahili pekee huku 9% wakitumia Kiswahili katika mikutano rasmi shuleni. Ruwaza ya msimbo wa Kiingereza pekee ilikuwa tofauti na hizi zingine hivi kwamba matumizi yake miongoni mwa walimu yalikuwa kama ifuatavyo: gwaride (9%), ofisini (21%) na walimu wenzao (9%). Vilevile ruwaza ya mseto wa Kiswahili, Kiingereza na Kiluo ilitokea kuwa 12% waliitumia kwenye gwaride, 21% wakiitumia ofisini huku 29% wakiitumia miongoni mwa mazungumzo ya walimu wao kwa wenyewe. Ruwaza ya matumizi ya lugha na miseto hii ilionekana kubadilika kabisa pale mawasiliano yalipohusisha walimu na wazazi kwa kuwa 44% walitumia mseto wa Kiswahili, Kiingereza na Kiluo huku 26% wakitumia msimbo wa Kiluo pekee. 12% walitumia Kiswahili pekee kuwasiliana na wazazi huku Kiingereza pekee kikitumika kwa kiwango cha chini zaidi (6%).

Katika mawanda ya nje ya shule, ruwaza hizi zilibadilika pia ikilinganishwa na yale ya shuleni ambapo ni katika mawanda ya kanisani pekee ambapo mseto wa Kiswahili, Kiingereza na Kiluo ulitumika kwa asilimia ya juu zaidi (39%) ikilinganishwa na mawanda ya sokoni na familia. Katika mawanda ya sokoni,

ambayo yanahusisha shughuli za biashara, msimbo wa Kiluo pekee ulitumiwa na 35%, mseto wa Kiingereza, Kiswahili na Kiluo 24%, Kiswahili pekee 24%, Kiingereza pekee 6% na lugha nyingine 12%. Katika mawanda ya nyumbani, ruwaza zilikuwa Kiluo pekee (29%), mseto wa Kiingereza, Kiswahili na Kiluo (24%), lugha nyingine (12%), Kiswahili pekee (21%), mseto wa Kiingereza na Kiswahili (9%) na Kiingereza pekee (6%). Japo utafiti wa Wamalwa na wenzake (2019) ulihusu wingilugha na ruwaza za matumizi ya lugha kama ulivyo utafiti huu, tafiti hizi zinatofautiana kwa namna maalum. Kwanza, utafiti wao ulihusisha walengwa walimu wa shule za msingi ambao aghalau wamesoma hadi kiwango cha vyuo vya kati ilhali utafiti huu ulihusha wananchi kwa jumla wenye viwango tofauti vya elimu. Vilevile, utafiti wao ulifanywa katika Kaunti ya Siaya ilhali huu ulifanywa katika Kaunti ya Machakos.

## 2.3. Uhusiano Uliopo Kati ya Lugha Mbalimbali na Athari zake Katika Utekelezaji Maendeleo

Mwangi (2016) akifafanua dhana ya wingilugha anahoji kuwa lugha zinazohusika katika miktadha ya wingilugha huwa na hadhi tofautitofauti katika shughuli fulani mahsusi au kwa misingi ya kijumla. Akiendeleza maoni haya, Wisbey (2016) anahoji kuwa tunaishi katika dunia yenye wingilugha ambapo binadamu hutumia lugha tofautitofauti kwa mambo tofautitofauti. Maoni haya yanaweka usuli thabiti wa sehemu hii ya uhusiano kati ya lugha mbalimbali na athari zake katika utekelezaji wa maendeleo kwa sababu inalenga kuhakiki maandishi yanayohusiana na jinsi lugha mbalimbali katika miktadha ya wingilugha huhusiana na kuathiri utekelezaji wa maendeleo ya jamii husika.

Sridhar (1996) akiangazia mifumo ya matumizi ya lugha anaandika kuwa katika mazingira ya wingilugha, hakuna mgao sawa wa nguvu, hadhi, umuhimu au mielekeo kwa lugha zote kwa sababu baadhi ya lugha huwa na thamani kubwa kuliko zingine. Hili husababisha lugha kupangwa katika ngazi ya mamlaka ambapo nafasi ya lugha katika ngazi hii huamuliwa na nafasi ya lugha husika kipragmatiki. Hivyo, kadri lugha inavyowasaidia wanajamii kufikia mengi ya malengo tarajiwa katika jamii ndivyo inavyokuwa katika ngazi ya juu. Katika suala hili, mtafiti huyu alichunguza hali ilivyokuwa nchini India ambapo anaonyesha kuwa wingilugha miongoni mwa watu waliosoma una idadi kubwa ya lugha au misimbo. Matokeo yanaonyesha kuwa wananchi hutumia lugha au lahaja asili zaidi wanapoingiliana na watu wa familia au watu wa ukoo, lugha au lahaja zinazochukua jukumu la utambulisho wa kikabila kama kilivyo *Kibrahman*, lahaja ya Kitulu, katika taifa ndogo la Karnata. Hata hivyo, ruwaza ya kutumia lugha hubadilika katika elimu, utawala, biashara, utangazaji na fasihi ambapo lugha ya *Kannada* hutumika na kuwapa wazungumzaji wake utambulisho wa kimkoa na uwezo wa kutembea katika taifa ndogo lote.

Kiingereza nacho katika kiwango cha masomo ya baada ya shule ya upili huwapa wazungumzaji wa Tulu nafasi ya masomo ya juu ya kiufundi, kuwasiliana na watu wa mataifa mengine madogo, kuwasiliana kitaifa na kushiriki katika utangazaji na uanahabari wa kitaifa. Zaidi, lugha hii ya Kiingereza huwapa nafasi ya kutembea eneo lolote kitaifa na kimataifa katika soko la ajira sawa na kuwapa hadhi na fahari. Hata hivyo, mzungumzaji anayejua lugha hizi hulazimika pia kujifunza lingua franka ya *Kihindi* maarufu katika video za Kihindi ili kufanikisha mawasiliano na mataifa mandogo ya Kaskazini mwa India na ambayo ndiyo lugha rasmi ya serikali kuu. Sridhar anafafanua

kwamba yapo majukumu ambayo hayawezi kutimizwa kikamilifu na mojawapo ya lugha hizi kibinafsi au zote kwa pamoja kama vile kufikia, kutunza na kuonyesha maarifa ya jadi katika nyanja kama vile za dini na matibabu. Hali hii huwalazimu Watulu kujifunza lugha ya *Kisanskriti*. Kuzingatia biashara na maingiliano ya kibinafsi, watafitiwa hujifunza lugha ya kimkoa moja au zaidi kama vile *Kitamil, Kitelugu au Kimarathi*. Kutokana na hali hii, Sridhar anahitimisha kuwa, katika wingilugha, kila lugha hutimiza majukumu maalumu kwa njia ya kipekee na kuwakilisha tambulisho tofautitofauti. Anahitimisha pia kuwa lugha zote hubadilishana ili kutimiza mahitaji changamano ya mawasiliano katika taifa.

Japo utafiti huu Sridhar unafanana na huu kwa kiwango kikubwa, zipo tofauti bayana kwa sababu wake uliangazia majukumu ya lugha kwa ujumla ilhali utafiti huu ulichunguza uhusiano na athari za lugha mbalimbali kwa utekelezaji wa maendeleo. Vilevile, utafiti wake ulifanywa katika muktadha wa taifa ndogo la Karnataka India Kusini ilhali huu ulifanywa katika Kaunti ya Machakos nchini Kenya, ambayo ni maeneo mawili yaliyo tofauti sana kijiografia.

Rassool na wenzake (2006) walichunguza lugha na maendeleo katika mazingira ya wingilugha kwa kufanya uchunguzi kifani wa kubadilishana maarifa na elimu kwa mwalimu Afrika Kusini. Matokeo ya utafiti wao yanaonyesha kuwa katika muktadha wa elimu, asilimia 50 ya masomo yalifunzwa kwa lugha ya Kiingereza na asilimia nyingine 50 kwa lugha ya Kiafrikana katika kiwango cha shule za upili. Hata hivyo, mafunzo kwa lugha ya mama yalilemaza kiwango cha ujuzi wa kusoma na kuandika cha asilimia 80 ya wanafunzi walioshindwa kuendelea na masomo kwa sababu ya umaskini. Hivyo, wingilugha katika muktadha huu ulilemaza maendeleo. Lugha ya Kiingereza nayo ilitumika na watu waliosoma

na hivyo kutengeneza matapo mawili ya kiuchumi huku ikileta maendeleo kwa wale waliosoma na kulemaza maendeleo kwa wale ambao hawakusoma. Utafiti huu ni wa kina kwa sababu unaonyesha uwezo wa wingilugha kulemaza maendeleo pale ambapo lugha husika zinatumika kwa njia ya kibaguzi.

Hoja hii inalandana na kauli ya Pendakur na Pendakur (2015) kuwa lugha inaweza kutumika vibaya hasa pale ambapo inatumika kama kigezo cha kutambua watu wa eneo fulani na wale wasio wa eneo fulani. Utafiti huu wa Rassool na wenzake (2006) ulifanywa Afrika Kusini jambo linaloutofautisha na huu uliofanywa nchini Kenya. Hata hivyo, utafiti huu ulitumia matokeo yao kuwa wingilugha unaweza kuathiri maendeleo kwa namna hasi katika kutathmini athari za wingilugha kwa utekelezaji wa maendeleo katika maeneo ya mijini na maeneo vizingasifa ambayo ni maeneo yenye wingilugha dhahiri.

Mwangi (2016) akichunguza changamoto na manufaa ya kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha Narok Kaskazini anafafanua nafasi ya lugha katika shughuli za kitamaduni, kikazi, kibiashara, na kiserikali ambapo anaonyesha jinsi lugha zinavyotimiza majukumu mbalimbali. Kwa mujibu wa utafiti wake, Kimaasai kimepewa hadhi kubwa katika shughuli za kitamaduni na kijamii lakini hadhi ya chini katika shughuli za kikazi na kibiashara ambapo Kiswahili kimepewa hadhi ya juu zaidi. Lugha ya Kiingereza nayo imepewa hadhi ya juu katika shughuli rasmi za kiserikali huku lugha nyinginezo zikitumika zaidi katika muktadha wa familia. Naye Kamau (2015) akifafanua wingilugha katika miktadha ya miji nchini Kenya anaonyesha jinsi lugha mbalimbali zinavyopewa hadhi tofautitofauti. Kwa mujibu wake, miji mikuu nchini Kenya, hasa Nairobi, hujumuisha wazungumzaji wa takriban lugha zote zinazozungumzwa nchini Kenya. Hata hivyo, lugha za mama huzungumzwa

kwa viwango vya chini ikilinganishwa na lugha za Kiingereza, Sheng' na Kiswahili. Lugha ya Kiswahili, ambayo ni lugha rasmi pamoja na Kiingereza na lugha ya taifa hutumika katika mawasiliano miongoni mwa watu wa jamii tofauti kuendesha shughuli zao za kimaendeleo. Lugha ya Kiingereza nayo, hutumika kuendesha shughuli rasmi za kiserikali na elimu. Zaidi, anaonyesha uhalisia wa miji mikubwa, Nairobi ikiwepo, kuwa lugha ya Sheng' hutumika kwa kiwango cha juu hasa katika mawasiliano ya vijana.

Tafiti hizi za Mwangi na Kamau zinalingana na utafiti huu kwa karibu kwa sababu zote zilifanywa katika muktadha wa taifa la Kenya. Pia, tafiti zao zilionyesha wingilugha na majukumu ambayo lugha tofauti zimetwika. Ijapokuwa utafiti huu ulilenga pia kuchunguza suala hili, tafiti zao hazikuonyesha uhusiano na athari za lugha husika katika maendeleo jambo ambalo lililengwa na utafiti huu. Zaidi, utafiti wa Mwangi ulifanywa katika Kaunti ya Narok na ule wa Kamau katika Kaunti za Nairobi na Kiambu ilhali utafiti huu ulifanywa katika Kaunti ya Machakos.

Chhaya (2017) akichunguza maendeleo ya kiuchumi na lugha kwa kuangalia hali nchini India anafafanua kuwa maendeleo si tu upunguzaji wa umaskini bali pia maendeleo ya kisosholojia, nafasi sawa za kushiriki katika mchakato wa maendeleo, uboreshaji wa afya na elimu na ushiriki katika demokrasia. Matokeo ya utafiti wake yalibainisha kwamba India ina lugha kama vile Kihindi na Kibengali ambazo huzungumzwa na idadi kubwa ya watu hata nje ya mipaka ya taifa hilo. Hali hii imefanya lugha hizi kusaidia katika maingiliano yao ya wenyewe kwa wenyewe na pia maingiliano na mataifa mengine ambayo yanatumia lugha hizo na hivyo kusababisha maendeleo ya kiuchumi. Kutokana na maingiliano haya kupitia lugha, utafiti wake Chhaya unaonyesha kwamba

India ilipanua biashara na mataifa mengine kutoka asilimia 0.70 mwaka wa 2000 hadi asilimia 1.60 mwaka wa 2012 ya mauzo kwa mataifa mengine ya ulimwengu. Hivyo kutokana na utafiti wake, ni wazi kwamba lugha ina nafasi kubwa katika maendeleo. Vilevile, matokeo ya mtaalamu huyu yalionyesha kuwa nchi ya Uchina ilipanua mazao yake ya ndani mwa nchi mwaka wa 2016 kwa asilimia 6.7 bado ikitumia lugha yake ya Kichina hali inayoonyesha nafasi ya lugha asili katika maendeleo.

Utafiti huu wa Chhaya (2017) unachunguza na kuonyesha athari za lugha kwa maendeleo hali inayofanana sana na utafiti huu. Vilevile, utafiti wao ulijikita katika kuchunguza maendeleo ya kiuchumi kama ulivyo utafiti huu. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana kwa sababu utafiti wao uliangazia maendeleo ya kiuchumi kwa ujumla ilhali utafiti huu uliangazia utekelezaji wa maendeleo. Pia, tafiti hizi zinatofautiana kwa sababu wake ulifanya nchini India ilhali huu ulifanywa nchini Kenya.

Utafiti mwingine ni ule uliohusu Kiswahili na Maendeleo ya Mashambani nchini Kenya uliofanywa na Saidi (2021). Akimnukuu Todaro (1992) Saidi anabainisha kwamba lazima maendeleo yahusishe mabadiliko ya msimamo, miundo, mbinu na asasi, makuzi ya uchumi kumaliza umaskini na upunguzaji wa ukosefu wa usawa. Katika kuchunguza mchango wa Kiswahili katika maendeleo haya, Saidi alifanya utafiti katika kaunti tatu (Kwale, Uasin Gishu, na Machakos) ambapo aliwahoji watu tofautitofauti kuhusu mchango wa Kiswahili katika maendeleo. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa Kiswahili kiliathiri maendeleo kwa njia chanya katika sekta mbalimbali kama vile kilimo, viwanda na juakali kwa kufanikisha mawasiliano. Hivyo, utafiti huu unaonyesha nafasi halisi ya lugha ya Kiswahili katika maendeleo. Lugha ya Kiswahili ikiwa lugha mojawapo ya

zile zinazounda wingilugha katika Kaunti ya Machakos, utafiti huu ulichunguza hadhi ya lugha hii katika wingilugha ikilinganishwa na zingine na jinsi lugha zote huathiri utekelezaji wa maendeleo katika kaunti hiyo. Mwingiliano huu katika kuchunguza athari za lugha ya Kiswahili kwa maendeleo unadhihirisha mlingano wa tafiti hizi. Hata hivyo, tofauti kuu ni kwamba utafiti wa Saidi ulichunguza lugha ya Kiswahili pekee tofauti na huu ambao ulichunguza athari za lugha mbalimbali zinazotumiwa katika Kaunti ya Machakos kwa utekelezaji wa maendeleo.

### 2.4. Nafasi ya Mielekeo katika Uteuzi wa Lugha

Painter na Dixon (2012) walifanya utafiti kuhusu mielekeo ya lugha Afrika Kusini. Wanahoji kuwa japo tafiti za mielekeo ya lugha zilianza kufanywa kwa utaratibu katika miaka ya sitini, mielekeo ya lugha nchini humo ilianza kujidhihirisha kitambo sana katika kipindi cha ujio wa Wareno katika mji wa Cape takriban karne sita zilizopita. Wakati Wareno walipoingia nchini humo, walipatana na watu wa jamii ya Khoikhoi waliozungumza lugha ya Kikhoikhoi na wengine. Watafiti hawa wanaeleza kuwa Wareno hawa walizaa mielekeo hasi kuhusu lugha hizi za Kiafrika na kuishia kuzieleza kwa maneno katili na yasiyokuwa na utu. Kwa mujibu wa wataalamu hawa, baadhi ya wale waliotumia maneno haya katili ni John Davys mwaka wa 1598, John Milward mwaka wa 1614, Thomas Herbert mwaka wa 1634 na Jean-Baptiste Tavernier mwaka wa 1694. Kwa mfano, Jean-Baptiste Tavernier kama anavyonukuliwa na Mostert (1992) katika Painter na Dixon alifafanua lugha ya watu wa mji wa Cape kwa maneno haya "*wanapoongea, wao huwa na vidoko kwa ndimi zao ndani ya vinywa vyao"* (tafsiri yetu). Hali hii ya mielekeo hasi ya wakoloni kwa lugha za Kiafrika iliendelea hadi katika kipindi cha ukoloni ambapo utafiti wa Painter na

Dixon unafafanua kwamba siasa za lugha za kikoloni na lugha za ubaguzi wa rangi zilikuwa na athari kubwa kwa mielekeo ya lugha za kikoloni na lugha asili katika eneo hilo.

Kwa mujibu wa ripoti yao, Painter na Dixon (2012) wanaandika kuwa mielekeo ya lugha iliendelea hadi katika kipindi cha baada ya ukoloni ambapo viongozi walipendelea lugha za wakoloni kutumika. Wakitoa mfano, wanahoji kwamba wananchi wengi waliionelea lugha ya Kiingereza kama lugha bia ya mawasiliano kati ya tamaduni na makabila tofautitofauti hali inayoonyesha mielekeo chanya kwa lugha hii. Kwa mujibu wa Giliomee (2004), kama anavyonukuliwa na watafiti Painter na Dixon (2012), waliokuwa na mielekeo chanya kwa lugha ya Kiingereza na hasi kwa lugha ya Kiafrikana sio wasomi tu pekee bali pia viongozi wa kisiasa wa Kiafrikana. Hata hivyo, yapo makundi ya wananchi waliokuwa na mwelekeo hasi kuhusu lugha za wakoloni na walioziona kama zana za kuwagawanya wananchi nchini humo.

Kutokana na mabadiliko haya ya mielekeo ya lugha nchini humo, Louw (2004) katika Painter na Dixon (2012) anasema kuwa katika miaka ya hivi majuzi, wahamasishaji watendaji wa lugha ya Kiafrikana wamesababisha lugha ya Kiafrikana kupewa hadhi ya lugha rasmi. Kutokana na matokeo ya utafiti huu wa Painter na Dixon (2012), ni wazi kuwa mielekeo ilichangia pakubwa katika uteuzi wa lugha za kutimiza malengo maalumu miongoni mwa wakoloni, Waafrikana na wananchi wa Afrika Kusini. Vivyo hivyo, japokuwa utafiti wao ulihusu uteuzi lugha kwa jumla, utafiti huu ulichunguza nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha za kutumia katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo katika Kaunti ya Machakos, nchini Kenya.

Mohochi (2011) naye akichunguza mielekeo ya wasomi wa Kiswahili na viongozi wa Afrika Mashariki kuhusu lugha ya Kiswahili anaonyesha jinsi mielekeo tofauti ilivyochangia katika uteuzi wa lugha za kutumia ili kutekeleza majukumu maalumu. Katika utafiti wake, Mohochi anafafanua kwamba lugha ya Kiswahili inaendelea kukumbwa na pingamizi huku akiorodhesha mielekeo ya lugha inayobainika katika jamii kama mojawapo ya vikwazo hivyo. Anaendelea kufafanua kwamba suala kuu katika lugha ya Kiswahili si mielekeo ya wazungumzaji wake kuhusu kujifunza kwa sababu tayari wanaifahamu lugha hii bali ni mielekeo yao kuhusu kuitumia katika miktadha tofautitofauti. Japo utafiti wake ulijikita katika lugha ya Kiswahili, wazo hili la Mohochi linabeba ukweli uliolengwa na madhumuni ya tatu ya utafiti huu kuhusu nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha ya kutumia katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo katika Kaunti ya Machakos.

Katika utafiti wake, Mohochi anaeleza kwamba viongozi wa Afrika Mashariki wamekuwa na mielekeo tofauti kuhusu lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, anafafanua kuwa Rais wa kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere alikuwa mtetezi na mpenzi wa lugha ya Kiswahili, yaani alikuwa na mwelekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili kama chombo muhimu cha ujenzi wa jamii inayojitegemea. Mwelekeo huu chanya wa kiongozi huyu unaeleza sababu za matumizi mapana ya lugha ya Kiswahili nchini humo kama lugha rasmi. Kuhusu Kenya, Mohochi anafafanua kwamba Rais wa kwanza, Mzee Jomo Kenyatta alikuwa na mwelekeo chanya kuhusu Kiswahili na kuwa alitambua umuhimu wa lugha hii. Mwelekeo huu ulimsababisha kutoa amri ya Kiswahili kutumika bungeni kama lugha rasmi sambamba na lugha ya Kiingereza. Hata hivyo, uwepo wa viongozi waliokuwa na mielekeo hasi kuhusu Kiswahili ulipelekea

amri hii kutotimizwa. Kwa mfano, aliyekuwa mwanasheria mkuu wa wakati huo, Bwana Charles Njonjo alipinga matumizi ya Kiswahili katika miktadha rasmi hadi kusema kwamba ni lugha ambayo watu wanaweza kuiokota sokoni na hivyo haikufaa kufundishwa shuleni. Kwa upande wake, Rais wa pili Daniel Arap Moi anaelezwa kama aliyekuwa na mwelekeo chanya kuhusu Kiswahili hali iliyochangia juhudi zake za kukipigisha Kiswahili hatua hasa kupitia mapendekezo ya tume alizoteua katika vipindi tofautitofauti vya uongozi wake.

Nchini Uganda, marais watatu wa Uganda: Milton Obote, Idi Amin na Yoweri Museveni wamekuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili. Mielekeo yao imesababisha kukua kwa matumizi ya Kiswahili nchini humo katikati ya upinzani mkubwa kutoka kwa baadhi ya sehemu za jamii ya Waganda. Hivyo basi, ni wazi kwamba mielekeo huchukua nafasi maalumu katika uteuzi wa lugha katika wingilugha na hivyo katika madhumuni ya tatu ya utafiti huu, mtafiti alilenga kutambua nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha maalumu ya kutumiwa au za kutumiwa katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo katika Kaunti ya Machakos.

## 2.5. Pengo la Kimaarifa

Katika maandishi ambayo yamehakikiwa katika sura hii, mapengo ya kimaarifa yamejitokeza katika kila sehemu ambayo utafiti huu ulidhamiria kuziba. Kwanza, katika sehemu ya kwanza ya ruwaza za matumizi ya lugha katika mazingira ya wingilugha, watafiti tofautitofauti wamefanya tafiti kuhusu suala hili. Hata hivyo, baadhi ya tafiti ambazo zimehakikiwa zinazungumzia hali katika nchi za nje ya Kenya kama vile Indonesia. Zile ambazo zimefanywa nchini Kenya zimefanywa katika Kaunti za Mandera na Siaya. Tofauti na tafiti

hizi ni kuwa utafiti huu ulichunguza ruwaza za matumizi ya lugha katika Kaunti ya Machakos ambalo ni eneo tofauti kabisa kijiografia na yale yaliyokwisha kufanyiwa utafiti. Pia, ni wazi kuwa hakuna utafiti ambao umefanywa unaoonyesha uhusiano uliopo kati ya lugha zinazohusisha wingilugha Kaunti ya Machakos na jinsi zinavyoathiri utekelezaji wa maendeleo. Ule ambao umefanywa unaonyesha lugha ya Kiswahili na maendeleo ambayo ni mojawapo ya lugha lengwa. Zaidi, uhakiki huu umeonyesha dhahiri kuwa mielekeo huchukua nafasi maalumu katika uteuzi wa lugha katika mazingira ya wingilugha. Hata hivyo, hakuna utafiti ambao umechunguza nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha mahsusi ya kutumia au za kutumia katika utekelezaji wa maendeleo katika Kaunti ya Machakos, jambo ambalo utafiti huu ulichunguza.

# SURA YA 3

# MBINU NA NJIA ZA UTAFITI

## 3.1. Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulichukua muundo mseto. Huu ni muundo ambao unahusisha kukusanya, kuchanganua na kuchanganyisha data za kitakwimu na data za kitaamuli (Dhingra & Dhingra, 2012). Hata hivyo, asilimia kubwa ya utafiti huu ilikuwa ni muundo wa kitaamuli ikilinganishwa na ule wa kitakwimu kwa sababu utafiti ulilenga kufafanua ruwaza za matumizi ya lugha katika wingilugha na athari zake kwa utekelezaji wa maendeleo. Muundo huu ulifaa zaidi kwa sababu kwanza unaongeza kiwango cha uhalali na uthabiti wa utafiti kwa kupunguza au hata kumaliza makali ya pungufu za kila muundo mmojawapo. Pia, maswali ya utafiti huu yalilenga kukusanya data za kitakwimu na za kitaamuli jambo ambalo lilisaidia kujibu maswali ya utafiti kikamilifu.

## 3.2. Mahala pa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika nyanjani katika Kaunti ya Machakos. Hivyo, kwa kuwa ulikuwa wa nyanjani, data za kimsingi zilikusanywa moja kwa moja kutoka kwa wasimamizi wa idara lengwa na wakaazi wa vijiji sita lengwa vya Kaunti ya Machakos katika utathmini wa wingilugha na athari zake katika utekelezaji wa maendeleo Kaunti ya Machakos.

## 3.3. Idadi Lengwa

Kwa mujibu wa Bryman (2012) katika Sangili (2019), idadi lengwa ya utafiti huhusisha watu wote, vitu vyote au matukio yote yanayolengwa kutafitiwa na mtafiti. Maelezo ya Tromp (2007) katika Sangili (2019) yanaongeza kigezo kingine kwa dhana ya idadi lengwa kwamba watu, vitu au matukio yote

yanayolengwa sharti yawe na nduni zinazoweza kutafitika. Hivyo, tunaweza kuifafanua idadi lengwa kama jumla ya watu, vitu au matukio yaliyo na nduni maalumu zinazoweza kutafitika ambazo mtafiti analenga kuchunguza ili kupata data anazohitaji. Kaunti ya Machakos ina wakazi 1,421,932 (KNBS, 2019). Hata hivyo, utafiti huu ulilenga maeneo ambayo yana wingilugha dhahiri ambayo ni maeneo vizingasifa, yaani maeneo yanayopakana na Kaunti zenye wananchi ambao ni wa jamii nyingine. Maeneo haya yanayopakana na kaunti zenye wananchi wa jamii nyingine ni tano na mjini Machakos ambapo kuna watu kutoka kwa jamii tofautitofauti. Maeneo haya yanapakana na kaunti za Kajiado (Kusini Magharibi) ambapo kuna Wamaasai, Embu (Kaskazini) ambapo kuna Waembu, Muranga (Kaskazini Magharibi) ambapo kuna Wagikuyu, Nairobi na Kiambu (Magharibi) ambazo zina Wagikuyu na makabila mengine.

Utafiti huu ulihusisha kijiji kimoja katika maeneo haya vizingasifa. Vijiji hivi ni pamoja na Konza (Machakos/Kajiado), Mlolongo (Machakos/Nairobi), Kianzambe (Machakos/Kiambu), Ndithini (Machakos/Muranga) na Katulye (Machakos/Embu). Mjini Machakos, eneo la Grogon liliteuliwa kimakusudi kwa sababu lina wingilugha dhahiri na pia shughuli zinazoendeshwa na wafanyabiashara zinahusiana na maendeleo ya kiuchumi ya sekta mbalimbali. Hivyo, vijiji vitano vilihusishwa katika utafiti huu na eneo moja mjini Machakos, ambalo lilichukuliwa kama kijiji kimoja katika utafiti huu. Nchini Kenya, kijiji huwa na ukubwa wa takriban kilomita moja mraba (Mutua & Kiruhi, 2021). Kwa mujibu wa data za KNBS (2019), katika Kaunti ya Machakos, upana wa kilomita moja mraba una watu takriban 236. Hivyo, idadi lengwa ya utafiti huu ikawa ni watu 1416.

### 3.4. Sampuli na mbinu za Usampulishaji

Sampuli huwa ni kiwakilishi cha idadi lengwa. Kothari na Garg (2019) wanaeleza kwamba wakati ambapo sampuli lengwa ni ndogo, basi huwa ni muhimu watafitiwa wote kuhusishwa lakini pale ambapo sampuli lengwa ni kubwa, huwepo na haja ya kuteua sampuli ambayo itashiriki utafiti kama kiwakilishi cha wengine wote. Hivyo, anafafanua usampulishaji kama uteuzi wa watafitiwa au vitafitiwa vichache kuwakilisha idadi lengwa katika utafiti. Ili kufikia idadi ya vijiji sita vya kushiriki katika utafiti, mbinu ya utabakishaji sinasibu ilitumika kwa sababu ni mbinu inayotumika pale ambapo sampuli lengwa si laiki (Kothari na Garg, 2019). Hata hivyo, mbinu hii ilihusisha usampulishaji wa hatua anuwai hivi kwamba maeneo bunge sita yenye wingilugha dhahiri yaliteuliwa kimakusudi. Ndani ya kila eneobunge, kata moja yenye uzingasifa ilichaguliwa kinasibu na kisha kijiji kimoja katika kila kata kuchaguliwa kati ya vile vyenye uzingasifa kutumia usampulishaji nasibu. Hivi ni kumaanisha kuwa makataa ya uhusishwaji wa vijiji hivi katika utafiti huu yalikuwa ni wingilugha dhahiri kutokana na uzingasifa wake. Kuhusu watafitiwa, kigezo cha uhusishwaji kilikuwa ni umri wa miaka kumi na minane na zaidi.

Katika kuteua sampuli ya utafiti huu maoni ya watafiti mbalimbali kuhusu idadi ya sampuli yalizingatiwa. Kwanza ni yale ya Best na Khan (2010) ambao walihoji kwamba hakuna maafikiano baina ya watafiti kuhusu idadi halisi ya sampuli ambayo inafaa kuteuliwa kutoka kwa jumuiya kwa sababu watafiti tofauti hutumia fomyula na asilimia tofauti katika uteuzi wa sampuli. Hata hivyo, kuhusiana na uteuzi wa sampuli, Milroy (1987) katika Kamau (2015) anapendekeza idadi ndogo ya sampuli kutokana na mantiki kuwa sampuli

kubwa, hasa katika lugha, hukusanya data nyingi yenye uradidi mwingi. Kothari (2004) anapendekeza kuwa idadi ya sampuli wakilishi inastahili kuwa kati ya asilimia 10 na 15 ya idadi lengwa. Maoni haya yaliungwa mkono na watafiti wengine kama vile Mugenda na Mugenda (2003) na Imbunya (2020) ambao wanasema kuwa kwa kiwango cha chini kabisa, idadi ya sampuli inafaa kuwa aghalau asilimia 10 ya idadi lengwa. Ni katika msingi huu ambapo utafiti huu ulitumia asilimia kumi ya idadi lengwa (1416). Hivyo, sampuli ya utafiti huu ilihusisha watafitiwa 142.

Kwa kawaida, ina mantiki kuwa mtafiti angewashirikisha watafitiwa 24 kutoka kila eneo teule la utafiti kwa kuwapa hojaji. Hata hivyo, data za KNBS (2019) zinaonyesha kuwa maeneo bunge ya Mavoko, Machakos Mjini, Masinga, Matungulu, Yatta na Kalama yana msongamano wa watu 368, 609, 106, 278, 162 na 113 mtawalia kwa kila kilomita moja mraba. Ijapokuwa eneo bunge la Kalama halikuwa eneo bunge kikamilifu katika kipindi cha utafiti huu, data hizi zinazoonyesha msongamano wa watu kama ilivyojitokeza katika sensa ya 2019. Data hizi zilitumika jinsi zilivyo katika utafiti huu kwa sababu ni za kina kwa kuwa zinaonyesha tofauti kati ya eneo bunge la Machakos Mjini na Kalama ambapo ndiko kuliko na kijiji cha Konza. Hivyo basi, jumla ya idadi ya msongamano wa wananchi katika maeneo bunge haya kwa kila kilomita moja mraba ni 1654. Ili kuhakikisha kuwa tofauti za kiwingi wa watu katika kila eneo bunge zimezingatiwa katika utafiti huu, uwiano wa asilimia ulitumika. Matokeo yalikuwa kwamba uwiano wa asilimia ya maeneo bunge ya Mavoko, Machakos Mjini, Masinga, Matungulu, Yatta na Kalama ni 23%, 37%, 6%, 17%, 10% na 7% mtawalia. Asilimia hizi zilitumika kufikia idadi ya watafitiwa kutoka kila kijiji. Hivyo, idadi ya watafitiwa kutoka vijiji vya Mlolongo, Grogon, Katulye,

Kianzambe, Ndithini na Konza ikawa ni 33, 52, 9, 24, 14 na 10 mtawalia ambapo mbinu na usampulishaji nasibu sahili ilitumika kuwafikia japo kwa kuzingatia kigezo cha umri wa miaka kumi na minane na zaidi. Utafiti huu ulihusisha pia mahojiano na wasimamizi wanne wa idara nne lengwa (Idara ya Biashara, Viwanda na Ubunifu, Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Miji, Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Idara ya Utamaduni na Michezo) ambao husimamia mchakato wa uundaji na uwasilishaji wa sera za maendeleo katika idara husika. Mbinu ya usampulishaji kimaksudi ilitumika kuteua wasimamizi wa idara hizi. Hivyo sampuli ya jumla ya utafiti huu ilikuwa ni watafitiwa 146.

### 3.5. Mbinu za Ukusanyaji Data

Kutokana na kutumika kwa muundo mseto katika utafiti huu, mbinu za utafiti wa kitakwimu na utafiti wa kitaamuli zilitumika kwa pamoja. Mbinu hizi ni pamoja na hojaji, mahojiano, uchunzaji na uhakiki wa nyaraka. Hojaji funge za likati zilitumika kukusanya data za kitakwimu, huku zile nusu-funge zikitumika kukusanya data za kitakwimu na za kitaamuli. Hojaji hizi zilijazwa na wananchi katika vijiji teule vya utafiti huu ambapo mtafiti alihusisha watafiti wasaidizi wawili katika kila kijiji. Mahojiano, kwa mujibu wa Kothari (2004), katika muktadha wa utafiti ni mazungumzo kati ya mtafiti na mtafitiwa au watafitiwa kuhusu mada ya utafiti husika. Mbinu hii ya mahojiano ilitumika kukusanya data kutoka kwa wasimamizi wa idara nne lengwa ambao ndio waliosimamia uundaji na uwasilishaji wa sera za maendeleo kwa wananchi katika idara husika za Kaunti ya Machakos. Mbinu ya tatu iliyotumika ilikuwa ni uchunzaji ambapo mtafiti pamoja na wasaidizi walikusanya data kwa kutazama jinsi watafitiwa walivyotumia lugha katika shughuli mbalimbali za maendeleo. Utafiti huu ulitumia pia mbinu ya uhakiki wa nyaraka zilizotumika kuwasilishia sera na

masuala ya maendeleo kwa wananchi. Kinyume na mbinu za awali zilizolenga kukusanya data za msingi, mbinu hii ilikusanya data za sekondari. Katika mbinu hii, mtafiti aliweka makini ya kiwango cha juu ili kuhakikisha kwamba data lengwa zilikuwa za kuaminika na kutegemeka kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti huu kama wanavyoonya Kothari na Garg (2019).

## 3.6. Vifaa vya Ukusanyaji Data

Kutokana na mbinu zilizojadiliwa hapo juu, vifaa vya hojaji, dodoso, mwongozo wa uchunzaji na kiunzi cha kukukusanya data za nyaraka zilitumika kukusanya data.

### 3.6.1. Hojaji

Kothari (2004) anaeleza hojaji kama maswali yaliyoandikwa katika karatasi na ambayo huulizwa mtafitiwa ili kupata taarifa kuhusu tatizo la utafiti. Anaendelea kufafanua kuwa zipo aina mbili za hojaji: hojaji funge na hojaji huru. Kwa mujibu wa utafiti huu, hojaji funge na nusu-funge zilitumika kukusanya data za kitakwimu na kitaamuli mtawalia. Hojaji funge ya likati (Kiambatisho 1A) na hojaji nusu-funge (Kiambatisho 1B) zilitumika kukusanya data zilizolenga kuchanganua ruwaza za matumizi ya lugha katika wingilugha, kutathmini uhusiano na athari za lugha husika katika utekelezaji wa maendeleo na kutambua nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha maalumu ya au za kutumiwa katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo katika Kaunti ya Machakos. Hojaji nusu-funge (Kiambatisho 1B) ndiyo iliyotumika kutathmini uhusiano na athari za lugha mbalimbali katika utekelezaji maendeleo kwa sababu iliwapa uhuru wa kueleza jinsi lugha mbalimbali zilivyoathiri mchakato wa utekelezaji wa maendeleo katika kaunti hiyo.

### 3.6.2. Dodoso

Ili kuhakikisha mahojiano yalifanyika kulingana na madhumuni ya utafiti huu, mtafiti alitumia dodoso ya kuelekeza mahojiano na wasailiwa. Katika mahojiano haya, mtafiti alilenga kutumia mbinu ya kurekodi mahojiano kwa hiari ya watafitiwa ambapo watatu walikubali kurekodiwa huku mmoja akidinda kurekodiwa. Mahojiano na yule mmoja aliyekataa kurekodiwa yalinakiliwa katika daftari kutumia kalamu. Katika uchanganuzi huu wa baadaye, mtafiti alifanya unukuzi wa majibu kutoka kwa rekodi ya simu na kuyaweka katika maandishi kisha kuyachanganua. Data zilizokusanywa kutumia kifaa hiki (Kiambatisho 2) zilisaidia kujibu swali la kwanza, la pili na la tatu. Mahojiano haya yalikuwa ya ana kwa ana.

### 3.6.3. Mwongozo wa Uchunzaji

Mbinu ya uchunzaji ilihusisha mtafiti pamoja na watafiti wasaidizi kuwa sehemu ya watafitiwa ambapo walishiriki katika shughuli zao kama vile uuzaji na ununuzi sokoni, mafunzo ya kilimo, mikutano ya maendeleo, kuungana na wagonjwa hospitalini, nyumbani, na hata kazini ili kutazama jinsi walivyotumia lugha katika shughuli husika. Yaani, mtafiti na watafiti wasaidizi walijumuika na watafitiwa katika shughuli zao za kila siku katika mawanda ya sokoni, mikutano ya michakato ya maendeleo, nyumbani, vipindi vya elimu ya kilimo na hospitalini na kunakili matokeo ya uchunzaji wao katika kifaa cha mwongozo wa uchunzaji (Kiambatisho 3) kisha mtafiti akayachanganua baadaye.

### 3.6.4. Kiunzi cha Kukusanya Data kutoka kwa Nyaraka

Kama wanavyoonya Kothari na Garg (2019), ukusanyaji wa data za sekondari ni njia ambayo ina changamoto nyingi sana katika utafiti kwa sababu ni rahisi mtafiti kupata data ambazo haziendani na utafiti wake. Hivyo, wanapendekeza

kwamba mtafiti anastahili kuzingatia mambo matatu ya data ya sekondari: ufaafu wa data husika, uaminikaji wake na utoshelevu wake. Ili kuhakikisha kwamba utafiti huu ulikusanya data zilizoendana na madhumuni ya utafiti huu, mtafiti alitumia kiunzi cha kukusanyia data za nyaraka (Kiambatisho 4) kilichomwelekeza kukagua data zilizopatikana. Kiunzi hiki pia kilimsaidia mtafiti kuepuka ukusanyaji wa data nyingi isiyo na maana yoyote katika utafiti huu, jambo ambalo lilisaidia kukwepa tatizo la uhitaji wa muda mwingi wa upangaji wa data kama hii. Kiunzi hiki kilitumika kukusanya nyaraka kutoka kwa wananchi walioshiriki kupitia kwa hojaji. Mtafiti alikusanya nyaraka walizokuwa nazo kutoka kwa serikali kuu, serikali ya kaunti na mashirika mengine yaliyohalalisha na Kaunti ya Machakos au serikali kuu. Data za nyaraka zilipangwa na zilichanganuliwa kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti na matokeo yake kuwasilishwa katika sura ya nne.

### 3.7. Uthabiti na Uhalali wa Vifaa vya Utafiti

Kutokana na umuhimu wa kuhakikisha uthabiti na uhalali wa utafiti kabla ya kufanya utafiti halisi, sehemu hii inafafanua dhana hizi pamoja na kuonyesha jinsi utafiti huu ulivyohakikisha uthabiti na uhalali.

#### 3.7.1. Uthabiti

Uthabiti katika utafiti hutokana na kufuatwa kwa taratibu zote za utafiti kama zilivyoainishwa katika pendekezo la utafiti. Kama wanavyonukuliwa na Sangili (2019), Kombo na Tromp (2007) wananafafanua uthabiti kama uwezo wa matokeo ya vipimo vya mjarabu kutegemeka. Ili kupima uthabiti wa utafiti huu na wa vifaa vilivyotumika katika utafiti huu, hasa hojaji, utafiti wa majaribio ulifanywa katika eneo la Kitengela, Kaunti ya Machakos. Utafiti huu wa

majaribio ulihusisha wananchi 15 ambao ni 10.56% ya sampuli ambayo ililandana na pendekezo la Nieswiadomy (2002) katika Sangili (2019). Eneo hili lilifaa zaidi kwa sababu ni eneo kizingasifa kutokana na kupakana kwake na Kaunti ya Kajiado na pia liko mjini. Muhimu zaidi ni kuwa ni eneo lililo katika Kaunti ya Machakos na hivyo lina sifa sawa za kiisimujamii na maeneo lengwa. Hata hivyo, kijiji hiki hakikujumuishwa katika utafiti halisi.

### 3.7.2. Uhalali

Sarantakos (2005) anafafanua kwamba uhalali ni sifa na mchakato wa kuangalia iwapo vipimo ni sahihi. Anaendelea kueleza kwamba uhalali huuliza maswali kama vile iwapo vifaa vya utafiti vinapima kile vinavyotarajiwa kupima. Kwanza, utafiti huu ulitumia mbinu ya upimaji wa uhalali wa maudhui katika vifaa vya utafiti. Ili kufanikisha hili, maoni ya wasimamizi, kama wataalamu, yalitumiwa kupimia uhalali wa vifaa vya data ya kitaamuli na uwiano wa uhalali wa maudhui kutumiwa katika kupima kiwango cha uhalali wa vifaa vya data ya kitakwimu. Pia, matokeo ya utafiti wa majaribio yalionyesha kiwango cha uhalali cha vifaa vya utafiti huu na hivyo kusaidia kurekebisha na kuondoa dosari zote zilizokuwepo. Hili lilihakikisha kwamba vifaa hivi vina kiwango cha juu cha uhalali katika utafiti halisi.

## 3.8. Vikwazo wa Utafiti

Katika harakati za ukusanyaji data, utafiti huu ulikumbwa na vikwazo vya aina mbili: vile vilivyotokana na utafiti wenyewe na vile vilivyotokana na mtafiti. Kikwazo cha kwanza kilitokana na hali kwamba utafiti huu ulifanywa katika kipindi cha siasa jambo ambalo liliathiri upatikanaji wa walengwa. Tatizo hili lililazimu mtafiti kushirikisha watafiti wasaidizi wawili tofauti na ilivyokuwa

imeratibiwa mtafiti msaidizi mmoja katika kila eneo la utafiti ili kuifikia sampuli ya kila eneo. Pili, utafiti huu ulikumbwa na tatizo la umbali mkubwa wa maeneo lengwa sita ya utafiti huu hali iliyohitaji gharama ya juu ya usafiri. Ili kupunguza makali ya tatizo hili, mtafiti alihusisha watafiti wasaidizi ambao ni wakaazi wa eneo husika jambo liliosaidia kupunguza gharama ghali za usafiri. Pia, mtafiti alikodi chumba cha kulala katika kila eneo lengwa hadi kukamilisha ukusanyaji data katika eneo husika. Mwisho, utafiti huu ulikumbwa na tatizo la wahojiwa wasimamizi wa idara husika ambapo baadhi yao hawakuona uhusiano kati ya utafiti wa lugha na idara zao. Tatizo hili lilipelekea msimamizi mmoja kusukumia jukumu hili afisa anayefanya kazi chini yake lakini aliyeketi katika vikao vya kuunda sera za maendeleo.

## 3.9. Upangaji, Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

### 3.9.1. Upangaji Data

Ili kuhakikisha kwamba data hizi zimewekwa katika zanatepe ya Kichanganuzi Data ya Kitakwimu za Sayansi Jamii, mtafiti alizipanga na kuziweka katika misimbo ya nambari moja hadi tano kisha kuziwewa katika zanatepe. Kwa upande mwingine data za kitaamuli zilinakiliwa na pangwa kwa mujibu wa madhumuni katika maandishi.

### 3.9.2. Uchanganuzi wa Data za Kitakwimu

Data za kitakwimu zilichanganuliwa kutumia zanatepe ya Kichanganuzi Data ya Kitakwimu za Sayansi Jamii. Kama wanavyoelekeza Wambugu & Njoroge (2022) na katika muktadha wa utafiti huu, data hizi zilihusisha data zilizokusanywa na hojaji funge na baadhi ya data za hojaji nusu-funge pamoja.

Uchanganuzi wa data hizi ulifanywa kulingana na madhumuni ya utafiti na nadharia za utafiti huu.

### 3.9.3. Uchanganuzi wa Data za Kitaamuli

Kwa upande mwingine, data za kitaamuli nazo zilichanganuliwa kwa njia ya uchanganuzi kidhamira (Mishra na wenzake, 2019). Dhamira zilizotumika katika uchanganuzi huu zilihusisha madhumuni ya utafiti huu. Yaani, zilichanganuliwa kwanza kuzingatia madhumuni ya kwanza ambayo yalihusisha uchanganuzi wa ruwaza za matumizi ya lugha katika Kaunti ya Machakos, madhumuni ya pili ambayo yalihusisha utathmini wa uhusiano na athari za lugha mbalimbali katika utekelezaji wa maendeleo katika Kaunti ya Machakos na tatu utambuzi wa nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha mahsusi ya au za kutumiwa katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo.

### 3.9.4. Uwasilishaji wa Data

Baada ya data kuchanganuliwa, takwimu elezi sahili za asilimia, modi na wastani (Mishra na wenzake, 2019) zilitumika kuwasilishia matokeo ya data za kitakwimu. Kwa upande mwingine, matokeo ya data za kitaamuli yaliwasilishwa kinathari kwa njia ya maelezo na ufafanuzi kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti huu.

### 3.9.5. Ufasili wa Data za Utafiti

Kwa sababu utafiti huu ulikusanya data za kitaamuli na za kitakwimu, mtafiti alitumia muundo afikivu mseto katika kufasili data. Kwa mujibu wa muundo huu, mtafiti hukusanya data za kitakwimu na za kitaamuli kiuafikivu na kuzichanganua kiuafikivu ili kupata matokeo (Imbunya, 2020). Almeidai (2018) na Wambugu & Njoroge (2022) wanakubaliana kuwa katika muundo huu,

ukusanyaji na uchanganuzi wa data za kitakwimu na kitaamuli hufanyika kandokando lakini kwa wakati mmoja na matokeo kuunganishwa katika hatua ya uwasilishaji, ufasili na ufafanuzi. Yaani, data za hojaji, dodoso, mwongozo wa uchunzaji na kiunzi cha kukusanya data za nyaraka zilikusanywa na kuchanganuliwa kiuafikivu kulingana na madhumuni ya utafiti huu ili kupata matokeo ya utafiti.

### 3.10. Maadili katika Utafiti

Arnold (2021) anafafanua kwamba kumekuwepo na ongezeko la utovu wa maadili katika utafiti wa kiusomi. Kutokana na ongezeko hili, suala la maadili katika utafiti wowote limekuwa jambo la muhimu na hivyo kupelekea mtafiti kuhakikisha maadili ya kiwango cha juu. Kama sehemu ya maadili ya utafiti, mtafiti alitafuta idhini za kufanya utafiti kutoka kwa Chuo Kikuu cha Kaimosi (Kiambatisho 16), Halmashauri ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (Kiambatisho 17) na Serikali ya Kaunti ya Machakos (Kiambatisho 18). Idhini hizi ziliwasilishwa kwa usimamizi wa vijiji husika kabla ya kukusanya data halisi. Pili, mtafiti aliwaeleza wasailiwa umuhimu wa utafiti huu kwa serikali ya Kaunti ya Machakos na pia taifa la Kenya ili washiriki kwa hiari yao. Mtafiti aliwapa watafitiwa nafasi ya kufanya uamuzi wa kuendelea au kujiondoa kwa utafiti huu wakati wowote kadri ya hiari yao. Vilevile, mtafiti aliwahakikishia watafitiwa usiri wa data walizozitoa kwa ajili ya utafiti huu na kwamba zingetumika kwa makusudi ya utafiti huu pekee na wala si kusudi lingine lolote. Aidha, katika mahojiano, mtafiti aliwaomba wasailiwa ruhusa ya kurekodi mahojiano husika ambapo alirekodi wale watatu waliompa ruhusu na kunakili majibu kutumia kalamu majibu ya yule aliyekataa kurekodiwa.

## SURA YA 4

## UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO

### 4.0 Utangulizi

Sura hii inawasilisha matokeo ya utafiti ambayo yanatokana na uchanganuzi wa data zilizopatikana kutoka kwa mbinu za ukusanyaji data za utafiti huu. Matokeo haya yanawasilishwa kwa mujibu wa madhumuni matatu ya utafiti. Hata hivyo, kabla ya kuwasilisha matokeo haya, sura hii inaanza kwa kuwasilisha sifa za kidemografia za watafitiwa waliohusishwa. Watafitiwa hawa wanahusisha wale walioshiriki kupitia kwa kujaza hojaji na wale walioshiriki kupitia kwa mahojiano. Katika kuwasilisha matokeo, sura hii inawasilisha uchanganuzi wa kauli mbalimbali ambazo zililenga kuyajibu maswali matatu ya utafiti huu. Kutokana na madhumuni ya kwanza, sura hii inawasilisha uchanganuzi wa ruwaza za matumizi lugha katika mawanda manane: sokoni, nyumbani, hospitalini, shambani, kazini, mikutano ya maendeleo, vipindi vya mafunzo ya kilimo, na biashara. Pia, sura hii inachanganua matokeo ya kauli mbalimbali zilizolenga kutathmini uhusiano na athari za lugha mbalimbali katika utekelezaji wa maendeleo na mwisho kuchanganua matokeo ya kauli tano zilizolenga kutambua nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha mahsusi ya au za kuundia na kuwasilishia sera za maendeleo katika eneo la utafiti huu. Pia sura hii inachanganua data zilizokusanywa kutokana na uchunzaji, mahojiano na uchanganuzi wa nyaraka.

### 4.1 Takwimu za Kimsingi za Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuwashirikisha watafitiwa 142 kwa njia ya hojaji kutoka vijiji sita. Idadi hii ilifaa kusambazwa kwa maeneo haya sita kama ifuatavyo:

Mlolongo 33, Grogon 52, Katulye 9, Kianzambe 24, Ndithini 14 na Konza 10. Hivyo hojaji 142 zilisambazwa kulingana na idadi lengwa ya kila kijiji. Hata hivyo hojaji 27 zilijazwa kwa njia mbovu hivi kwamba hazikushirikishwa katika utafiti huu na hivyo uchanganuzi huu ukafanywa kutokana na hojaji 115 zilizokuwa zimejazwa kwa njia iliyostahili. Jedwali 4.1 linawasilisha msambao wa hojaji zilizojazwa vyema na kutumika katika uchanganuzi wa data na jedwali 4.2 kuwasilisha msambao wa hojaji zilizoharibiwa katika kila kijiji.

***Jedwali 4.1: Msambao wa hojaji zilizojazwa vizuri***

| Kijiji | Sampuli Lengwa | Mdafao | Asilimia | Kiwango cha Mwitiko |
|---|---|---|---|---|
| Konza | 10 | 9 | 7.8 | 90.0 |
| Grogon | 52 | 41 | 35.7 | 78.8 |
| Mlolongo | 33 | 26 | 22.6 | 78.8 |
| Katulye | 9 | 9 | 7.8 | 100 |
| Kianzambe | 24 | 19 | 16.5 | 79.2 |
| Ndithini | 14 | 11 | 9.6 | 78.6 |
| **Jumla** | **142** | **115** | **100.0** | |

*(Chanzo: Utafiti wa nyanjani, 2022)*

***Jedwali 4.2 Msambao wa hojaji zilizoharibika***

| Kijiji | Sampuli Lengwa | Mdafao | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Konza | 10 | 1 | 10.0 |
| Grogon | 52 | 11 | 21.2 |
| Mlolongo | 33 | 7 | 21.2 |
| Katulye | 9 | 0 | 0 |
| Kianzambe | 24 | 5 | 20.8 |
| Ndithini | 14 | 3 | 21.4 |
| **Jumla** | **142** | **27** | |

*(Chanzo: Utafiti wa nyanjani, 2022)*

Kwa jumla, hojaji 115 ndizo zilitumika katika uchanganuzi huu ambazo ziliwakilisha 81.0% ya sampuli lengwa. Kulingana na Baruch (1999) na Cook na wenzake (2009), ambao wanasema kuwa kiwango cha chini kabisa cha mwitiko wa hojaji kinastahili kuwa 80%, idadi hii ilikuwa inatosha kuwakilisha watafitiwa wote na kuzalisha matokeo ya kutegemeka na kuaminika.

## 4.2 Nduni za Kidemografia za Watafitiwa

Ili kusaidia kuchanganua matokeo ya utafiti huu kiuhakikifu, nduni nne za kidemografia za watafitiwa zilichunguzwa pia na matokeo yake yakawa kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Jinsia

Kutokana na utafiti wa nyanjani, matokeo yalionyesha kuwa kati ya watafitiwa 115 ambao hojaji zao zilishirikishwa katika uchanganuzi wa matokeo, 59 (51.3%) walikuwa wa kike na 56 (48.7%) walikuwa wa kiume. Uwiano huu wa asilimia hizi za washiriki wa kike kwa kiume unaonyesha msambao sawa wa washiriki kijinsia hali ambayo ilisaidia matokeo kusawazisha pande zote mbili na kuondoa uwezekano wa kuegemea jinsia moja. Jedwali lifuatalo linaonyesha msambao wa watafitiwa kijinsia katika vijiji vyote sita.

***Jedwali 4.3: Msambao wa Kijinsia***

| | **Jinsia** | | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| | ***Kike*** | ***Kiume*** | |
| Konza | 4 | 5 | 9 |
| Grogon | 22 | 19 | 41 |
| Mlolongo | 13 | 13 | 26 |
| Katulye | 5 | 4 | 9 |
| Kianzambe | 9 | 10 | 19 |
| Ndithini | 6 | 5 | 11 |
| **Jumla** | **59** | **56** | **115** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Kutokana na msambao huu wa kijinsia, takwimu hizi zinaonyesha kuwa uwiano huu wa kijinsia haukuwa tu katika takwimu za jumla bali ulisambaa pia katika vijiji vyote sita vya utafiti huu. Hii inamaanisha kwamba matokeo ya utafiti huu yanaonyesha hali ilivyo kijinsia katika maeneo yote lengwa.

#### 4.2.2 Umri

Nduni ya umri ilihusishwa katika utafiti huu. Nduni hii iligawika katika makundi matatu ya kiumri: miaka 18-35, miaka 36-45 na zaidi ya miaka 46. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti, kati ya watafitiwa 115, waliokuwa wa kundi la miaka 18-35 walikuwa 37 (32.2%), kundi la miaka 36-45 walikuwa 40 (34.8%) na kundi la miaka zaidi ya 46 walikuwa 38 (33.0%). Data hizi zinaonyesha kuwa matapo haya matatu ya kiumri yalishirikishwa kwa viwango sawa na hivyo kuhakikisha kwamba matokeo ya utafiti huu hayaegemei katika kundi moja la kiumri la watafitiwa. Jedwali lifuatalo linaonyesha msambao wa watafitiwa kiumri katika kila kijiji:

***Jedwali 4.4 Msambao wa watafitiwa kiumri katika kila kijiji***

| | | Kijiji | | | | | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Konz-a | Grogon | Mlolo-ngo | Katu-lye | Kianza-mbe | Ndithi-ni | |
| Miaka 18-35 | Mdafao | 3 | 12 | 8 | 6 | 4 | 4 | 37 |
| | Asilimia | 33.3% | 29.3% | 30.8% | 66.7% | 21.1% | 36.4% | 32.2% |
| Miaka 36-45 | Mdafao | 4 | 16 | 8 | 0 | 7 | 5 | 40 |
| | Asilimia | 44.4% | 39.0% | 30.8% | 0.0% | 36.8% | 45.5% | 34.8% |
| Miaka zaidi ya 46 | Mdafao | 2 | 13 | 10 | 3 | 8 | 2 | 38 |
| | Asilimia | 22.2% | 31.7% | 38.5% | 33.3% | 42.1% | 18.2% | 33.0% |
| **Jumla** | **Mdafao** | **9** | **41** | **26** | **9** | **19** | **11** | **115** |
| | **Asilimia** | **100.0%** | **100.0%** | **100.0%** | **100.0%** | **100.0%** | **100.0%** | **100.0%** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Matokeo haya yanaonyesha kwamba utafiti huu uliwahusisha watafitiwa kwa njia inayosawazisha makundi yote matatu ya kiumri katika vijiji vyote sita. Usawazishaji wa watafitiwa hawa kiumri ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu matokeo ya utafiti yanaonyesha jinsi hali ilivyo katika vijiji hivi na hivyo

kukadiria hali halisi katika jamii yoyote ile kwa sababu watu wa makundi haya ya kiumri hupatikana katika Kaunti ya Machakos na kaunti nyinginezo.

### 4.2.3 Kiwango cha Elimu

Utafiti huu ulihusu uchunguzi wa wingilugha, ambapo watu tofautitofauti huelewa na kutumia lugha mbalimbali kulingana na mambo mbalimbali na mojawapo ni kiwango cha elimu. Hivyo, ili kuchunguza ruwaza za matumizi ya lugha na nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha kama yalivyo madhumuni ya kwanza na tatu ya utafiti huu, nduni ya kiwango cha elimu ni muhimu sana. Katika utafiti huu, nduni hii iligawika katika makundi manne: wale ambao hawajawahi kusoma, waliofika darasa la nane, waliofika kidato cha nne na waliofika vyuo vya kati na vikuu. Matokeo yanaonyesha kuwa walioshiriki katika utafiti huu walikuwa na viwango vya elimu kama inavyowakilishwa katika jedwali lifuatalo:

***Jedwali 4.5 Kiwango cha Elimu***

| | **Mdafao** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Sijawahi Kusoma | 5 | 4.3 |
| Darasa la 8 | 32 | 27.8 |
| Kidato cha nne | 45 | 39.1 |
| Chuo cha Kati/Kikuu | 33 | 28.7 |
| **Jumla** | **115** | **100.0** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Kutokana na takwimu hizi, kundi la watafitiwa lililorekodi idadi ya juu kabisa ni lile la watafitiwa waliosoma hadi kiwango cha shule za sekondari ambao waliwakilisha 39.1%. Kundi lililorekodi asilimia ya chini kabisa ni lile la washiriki ambao hawajawahi kusoma waliowakilisha 4.3%. Makundi ya waliopata masomo ya shule za msingi na wale waliosoma hadi vyuo vya kati na vikuu yaliwakilisha 27.8% na 28.7% mtawalia. Idadi ndogo ya wale ambao

hawajawahi kusoma ilitambua kwamba wapo katika jamii za leo na kuwa ni walengwa wa maendeleo. Zaidi, matokeo haya yalikuwa kiini kikubwa cha kuchunguza jinsi matumizi ya lugha mbalimbali yalivyoathiri utekelezaji wa maendeleo miongoni mwa watu wa viwango hivi vya elimu ambalo ndilo lengo kuu ya utafiti huu.

### 4.2.4 Kazi Wanayoifanya Watafitiwa

Vilevile, utafiti huu ulitambua kwamba matumizi ya lugha katika muktadha wa wingilugha hutumia ruwaza tofautitofauti katika kazi mbalimbali, jambo ambalo lilikuwa msingi mkuu wa kuhusisha nduni hii. Matokeo yalionyesha kuwa watafitiwa walifanya kazi mbalimbali kama ilivyo katika jedwali lifuatalo:

***Jedwali 4.6 Kazi Wanayoifanya Watafitiwa***

| | **Mdafao** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Ofisini | 12 | 10.4 |
| Nyumbani | 14 | 12.2 |
| Shambani | 21 | 18.3 |
| Hospitalini | 6 | 5.2 |
| Biashara | 38 | 33.0 |
| Sehemu Nyingine | 24 | 20.9 |
| **Jumla** | **115** | **100.0** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Kwa mujibu wa takwimu hizi, watafitiwa wanafanya kazi katika sekta mbalimbali: zile rasmi na zile zisizo rasmi. Hata hivyo, takwimu hizi zinaonyesha kuwa asilimia kubwa zaidi (33%) walikuwa ni wafanyabiashara wakifuatiwa kwa karibu na waliofanya kazi katika sehemu nyingine kwa 20.9% ambao walihusisha sana waliokuwa wameajiriwa. Asilimia ya chini kabisa ilikuwa ni 5.2% ambayo iliwakilisha waliofanya kazi hospitalini. Hivyo, nduni hii ilisaidia utafiti huu katika kuchanganua na kufafanua ruwaza za matumizi ya lugha katika mawanda ambayo kazi hizi hufanyika, kutathmini athari na

uhusiano wa lugha mbalimbali katika utekelezaji wa maendeleo na kutambua nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha katika mawanda haya.

### 4.3 Ruwaza za Matumizi ya Lugha Katika Kaunti ya Machakos.

Sehemu hii inachanganua matokeo ya data zilizolenga madhumuni ya kwanza ambayo yalichunguza ruwaza za matumizi ya lugha katika Kaunti ya Machakos. Uchanganuzi huu unahusisha lugha au miseto ya lugha iliyotumika katika mawanda ya sokoni, nyumbani, hospitalini, shambani, kazini, mikutano ya maendeleo, vipindi vya mafunzo ya kilimo na biashara. Sehemu hii inatathmini kwa kina ruwaza za matumizi ya lugha katika wingilugha katika mawanda haya maalumu. Udhahiri wa wingilugha huu ulionyeshwa na matokeo ya uchanganuzi wa miitiko ya watafitiwa kuhusu kauli mbili kuwa Kaunti ya Machakos ina watu kutoka jamii mbalimbali na kuwa lugha zaidi ya tatu zinazungumzwa katika Kaunti ya Machakos. Katika kauli ya kwanza, mtafitiwa mmoja anayewakilisha 0.9% ya watafitiwa hakuwa na hakika kuhusu uwepo wa watu kutoka jamii mbalimbali. Watafitiwa 40 (34.8%) walikubali huku wengine 74 (64.3%) wakikubali kabisa. Kwa jumla, watafitiwa (114) 99.1% walikubali kuwa Kaunti ya Machakos ilikuwa na watu kutoka jamii mbalimbali. Hakuna mtafitiwa yeyote aliyekosa kukubali uwepo wa watu kutoka jamii mbalimbali, hali inayoonyesha wingilugha dhahiri katika Kaunti ya Machakos. Katika kauli ya pili, matokeo yalionyesha kuwa watafitiwa 70 (60.9%) walikubali kabisa, 43 (37.4%) walikubali, huku 2 (1.7%) wakiwa hawana hakika. Kwa jumla watafitiwa 113 (98.3%) walikubali kuwa lugha zaidi ya tatu zilizungumzwa katika kaunti hiyo, matokeo yanayodhihirisha uwepo wa wingilugha ulio dhahiri. Lugha ambazo watafitiwa waliziorodhesha kuzungumzwa katika Kaunti ya Machakos ni Kikamba, Kiswahili, Kiingereza, Kimaasai, Kiembu, Kigikuyu,

Kiluo, lahaja za Kiluhya, lahaja za Kikalenjin, Kisomali, Kimbeere, Kimeru, Kiturkana, Kihindi, Kitaita na Kiborana. Katika hali hii, matokeo ya uchanganuzi wa ruwaza za matumizi ya lugha katika mawanda haya yalionyesha kuwa zilitofautiana huku kwingine zikifanana. Sehemu inayofuata inawasilisha matokeo ya uchanganuzi wa ruwaza za matumizi ya lugha katika mawanda haya.

### 4.3.1 Sokoni

Katika mawanda ya sokoni, lugha zilitumika kwa namna tofauti. Matokeo ya uchanganuzi wa data yalitambua ruwaza zifuatazo katika muktadha huu wa sokoni:

***Jedwali 4.7 Ruwaza za Matumizi ya Lugha Sokoni***

| | | **Kik** | **Kisw** | **Kisw+ Kik+ Kiing** | **Kisw+ Kik** | **Kisw+ Kiing** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Konza | Mdafao | 0 | 2 | 1 | 6 | 0 | 9 |
| | Asilimia | 0.0% | 22.2% | 11.1% | 66.7% | 0.0% | 100.0% |
| Grogon | Mdafao | 2 | 2 | 3 | 33 | 1 | 41 |
| | Asilimia | 4.9% | 4.9% | 7.3% | 80.5% | 2.4% | 100.0% |
| Mlolongo | Mdafao | 0 | 7 | 2 | 14 | 3 | 26 |
| | Asilimia | 0.0% | 26.9% | 7.7% | 53.8% | 11.5% | 100.0% |
| Katulye | Mdafao | 5 | 1 | 0 | 3 | 0 | 9 |
| | Asilimia | 55.6% | 11.1% | 0.0% | 33.3% | 0.0% | 100.0% |
| Kianzambe | Mdafao | 1 | 1 | 1 | 16 | 0 | 19 |
| | Asilimia | 5.3% | 5.3% | 5.3% | 84.1% | 0.0% | 100.0% |
| Ndithini | Mdafao | 0 | 4 | 0 | 7 | 0 | 11 |
| | Asilimia | 0.0% | 36.4% | 0.0% | 63.6% | 0.0% | 100.0% |
| **Jumla** | **Mdafao** | **8** | **17** | **7** | **79** | **4** | **115** |
| | **Asilimia** | **7.0%** | **14.8%** | **6.1%** | **68.7%** | **3.5%** | **100.0%** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Matokeo haya yanaonyesha kuwa katika kijiji cha Konza, misimbo ya Kikamba pekee, Kiingereza pekee na lugha nyingine pekee haikutumika katika muktadha wa sokoni, watafitiwa 2 (22.2%) walitumia msimbo wa Kiswahili pekee, 1

(11.1%) walitumia mseto wa Kikamba, Kiswahili na Kiingereza, huku 6 (66.7%) wakitumia mseto wa Kiswahili na Kikamba. Katika eneo la Grogon lililo mjini Machakos, watafitiwa 2 (4.9%) walitumia msimbo wa Kikamba pekee sawa na 2 (4.9%) waliotumia msimbo wa Kiswahili pekee. Mseto wa Kikamba, Kiswahili na Kiingereza nao ulitumiwa na watafitiwa 3 (7.3%) huku 33 (80.5%) wakitumia mseto wa Kiswahili na Kikamba. Ni mtafitiwa 1 (2.4%) pekee aliyetumia mseto wa Kiswahili na Kiingereza. Hata hivyo, misimbo ya Kiingereza pekee na lugha nyingine pekee haikutumiwa. Matokeo yalionyesha pia kuwa katika kijiji cha Mlolongo, ruwaza za matumizi ya lugha zilikuwa: Kikamba pekee watafitiwa 0 (0.00%), Kiswahili Pekee 7 (27.0%), Kiingereza pekee 0 (0.0%), Lugha nyingine pekee 0 (0.0%), mseto wa Kikamba, Kiswahili na Kiingereza 2 (7.7%), mseto wa Kikamba na Kiswahili 14 (53.8%) na mseto wa Kikamba na Kiingereza 3 (11.5%).

Matokeo haya yanaonyesha pia kuwa katika kijiji cha Katulye msimbo wa Kikamba pekee ulitumiwa na watafitiwa 5 (55.6%), Kiswahili pekee 1 (11.1%), Kiingereza pekee 0 (0.0%), Lugha nyingine pekee 0 (0.0%), mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza 0 (0.0%), mseto wa Kikamba na Kiswahili 3 (33.3%), na mseto wa Kikamba na Kiingereza 0 (0.0%). Katika kijiji cha Kianzambe msimbo wa Kikamba pekee ulitumiwa na mtafitiwa 1 (5.3%), msimbo wa Kiswahili pekee 1 (5.3%), mseto wa Kikamba, Kiswahili na Kiingereza 1 (5.3%) na mseto wa Kikamba na Kiswahili 16 (84.1%). Misimbo ya Kiingereza pekee, lugha nyingine pekee 0.0% sawa na miseto ya Kikamba na Kiingereza na Kiswahili na Kiingereza ambayo haitumiki katika kijiji hiki. Katika kijiji cha Ndithini, lugha ilitumiwa kama ifuatavyo: Kikamba pekee 0 (0.0%), Kiswahili pekee watafitiwa 4 (36.4%), mseto wa Kikamba, Kiswahili na Kiingereza 0

(0.0%) na mseto wa Kikamba na Kiswahili 7 (63.6%). Misimbo ya Kiingereza pekee, lugha nyingine pekee na miseto ya Kikamba na Kiingereza na Kiswahili na Kiingereza haikutumika. Mahojiano ya Afisa Mkuu wa Kitengo cha Mimea katika Idara ya Mimea, Mifugo na Uvuvi na Afisa Mkuu Idara ya Biashara yalionyesha ukweli wa matokeo haya. Kauli zao zilionyesha ruwaza hizi na kutoa sababu za ruwaza za mawanda ya sokoni.

> Afisa Mkuu wa Kitengo cha Mimea*: Katika maeneo ya mjini utapata kuna watu wa kila aina na hivyo tunachanganya lugha zote tatu (Kiswahili, Kikamba na Kiingereza) lakini mashinani ambapo Wakamba huwa takriban asilimia 90 tunatumia Kikamba sana na kuchanganya na Kiswahili pale panapohitajika.*
>
> Afisa Mkuu Idara ya Biashara: *Tukiwa katika mazingira ya mijini, … tunatumia Kiswahili zaidi kikifuatiwa na matumizi ya Kiingereza na iwapo Kikamba kitatumika, kitatumika kidogo sana kwa sababu katika maeneo haya kuna watu ambao si Wakamba na hawaelewi Kikamba kabisa.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022).

Katika uchunzaji, mtafiti alithibitisha matokeo haya ya data za hojaji na mahojiano. Katika maeneo yote ya utafiti huu, lugha ya Kiswahili ilitumiwa kwa wingi zaidi na Kiingereza kwa kiwango cha chini. Kiswahili kilitumika zaidi, hasa katika siku za soko huria kwa sababu watu wa jamii mbalimbali walihusika. Mjini Machakos, katika shughuli za uchunzaji, wauzaji wote katika soko ya Marikiti walimkaribisha mtafiti kutumia lugha ya Kiswahili sawa na wateja wengine na pale wateja walipozungumza Kikamba basi wauzaji wanabadili msimbo na kutumia Kikamba.

Matokeo haya yanalandana na Uchunguzi wa LINEE (2010) ambao ulionyesha kuwa wingilugha hutumika kama njia ya kufikia ufanisi wa kiuchumi na hivyo ruwaza za matumizi ya lugha kutokea katika kila mazingira ya wingilugha. Tofauti za ruwaza za matumizi ya lugha ni dhahiri katika mawanda ya sokoni, tofauti ambazo kwa kiasi kikubwa zinatokana na tofauti za kimazingira. Katika

vijiji hivi, viwili (Grogon na Mlolongo) ni maeneo vizingasifa ya mjini na vingine vinne ni maeneo vizingasifa ya mashinani. Tofauti bayana zinajitokeza katika ruwaza za matumizi ya lugha za mazingira haya mawili. Umaarufu wa ruwaza zinazohusisha lugha ya Kikamba ni zaidi katika vizingasifa vya mashinani ikilinganishwa na mjini. Vilevile, umaarufu wa ruwaza zinazohusisha Kiingereza unaongezeka katika vizingasifa vya mjini.

Vilevile, matokeo haya yanalandana na kutofautiana na yale ya utafiti wa Wamalwa na wenzake (2019). Yanalandana katika matumizi ya Kiswahili kwa sababu katika tafiti zote lugha ya Kiswahili inatumika katika viwango takriban sawa. Katika utafiti wao, matumizi haya ya Kiswahili yanasababishwa na kiwango cha walimu cha elimu huku katika utafiti huu yakisababishwa na mazingira ya wingilugha. Hata hivyo, utofauti wa kimatokeo unajitokeza kwa sababu utafiti wao unaonyesha matumizi mapana ya Kiluo ambayo ndiyo lugha asili ya eneo la utafiti wao ilhali matokeo ya utafiti huu yanaonyesha matumizi ya kiwango cha chini ya matumizi ya Kikamba ambayo ndiyo lugha asili ya eneo la utafiti huu katika maeneo yote. Hata hivyo, msingi mkubwa wa tofauti hii ni wa kimuktadha kwa sababu utafiti wao ulifanywa katika kaunti ambayo iko mbali sana na mji mkuu wa Kenya ilhali huu ulifanywa katika kaunti iliyo na wingilugha dhahiri kutokana na ujirani na mji wa Nairobi, ulio na watu wa jamii zote za Kenya na za nje ya Kenya na uzingasifa. Vilevile, utafiti huu kwa mujibu wa matokeo ya kazi wanazozifanya watafitiwa katika sehemu ya 4.2.4, ulihusisha watu wanaofanya kazi tofautitofauti ikilinganishwa na wao ambao ulihusisha tu walimu wa shule za msingi ambayo ni sababu nyingine inayoakisiwa na utafiti huu kusababisha tofauti hii.

Mhimili wa lugha na maendeleo ya binadamu wa Kiunzi cha Kinadharia cha Lugha na Mendeleo ya Kijamii na Kiuchumi unathibitisha matokeo haya kwa kuiona lugha kama sehemu ya utamaduni wowote ule na kuwa inachangia katika kuumba na kuendeleza utamaduni. Muhimu zaidi ni vigeu vitatu vya kukadiria maendeleo ya binadamu kwa mujibu wa mhimili huu ambavyo ni elimu, miaka tarajiwa ya kuishi na kiwango cha mapato. Mhimili huu unasisitiza kwamba lugha ya binadamu ni kigezo cha msingi katika maendeleo haya. Matokeo haya yanadhihirisha lugha kuwa msingi mkuu wa maendeleo ya wananchi, hasa mno wale wanaofanya kazi sokoni, katika kigeu cha kiwango cha mapato kwa kuwa wanatumia lugha tofautitofauti zinazowasaidia kuwahudumia wateja wote sokoni hali inayoongeza kiwango chao cha mapato.

### 4.3.2 Nyumbani

Katika mawanda haya, ruwaza za matumizi ya lugha ni tofauti na yale ya sokoni. Ruwaza zilijitokeza kuwa kama ilivyo katika jedwali lifuatalo:

*Jedwali 4.8 Ruwaza za Matumizi ya Lugha Nyumbani*

| | | | | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Kik** | **Kisw** | **Kiing** | **L.N** | **Kisw+ Kik+ Kiing** | **Kisw+ Kik** | **Kisw+ Kiing** | |
| Konza | Mdafao | 7 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 9 |
| | Asilimia | 77.8% | 0.0% | 0.0% | 0.0% | 11.1% | 11.1% | 0.0% | 100.0% |
| Grogon | Mdafao | 23 | 1 | 0 | 3 | 10 | 2 | 2 | 41 |
| | Asilimia | 56.1% | 2.4% | 0.0% | 7.3% | 24.4% | 4.9% | 4.9% | 100.0% |
| Mlolongo | Mdafao | 7 | 4 | 1 | 5 | 3 | 3 | 3 | 26 |
| | Asilimia | 26.9% | 15.4% | 3.8% | 19.2% | 11.5% | 11.5% | 11.5% | 100.0% |
| Katulye | Mdafao | 7 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 9 |
| | Asilimia | 77.8% | 0.0% | 0.0% | 11.1% | 0.0% | 11.1% | 0.0% | 100.0% |
| Kianzambe | Mdafao | 12 | 0 | 0 | 2 | 4 | 1 | 0 | 19 |
| | Asilimia | 63.2% | 0.0% | 0.0% | 10.5% | 21.1% | 5.3% | 0.0% | 100.0% |
| Ndithini | Mdafao | 6 | 2 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 11 |
| | Asilimia | 54.5% | 18.2% | 0.0% | 18.2% | 0.0% | 9.1% | 0.0% | 100.0% |
| | **Mdafao** | **62** | **7** | **1** | **13** | **18** | **9** | **5** | **115** |
| **Jumla** | **Asilimia** | **53.9%** | **6.1%** | **0.9%** | **11.3%** | **15.7%** | **7.8%** | **4.3%** | **100.0%** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Matokeo haya yanaonyesha kuwa kwa jumla, msimbo wa lugha ya Kikamba pekee ndio ruwaza maarufu kabisa katika mawanda ya nyumbani kwa sababu kwa jumla unatumika na 53.9% ikilinganishwa na 6.1% ya Kiswahili pekee, 0.9% ya Kiingereza pekee, 11.3% ya lugha nyingine pekee, 15.7% ya mseto wa Kikamba, Kiswahili na Kiingereza, 7.8% ya mseto wa Kiswahili na Kikamba na 4.3% ya mseto wa Kiswahili na Kiingereza. Hali hii inatokea sio tu kwa takwimu za jumla bali pia katika kila kijiji ambapo msimbo wa Kikamba pekee unatumiwa na asilimia kubwa zaidi ya watafitiwa kama inavyoonyeshwa katika jedwali. Ili kutambua sababu za hali hii, mtafiti kupitia uchunzaji alibaini kuwa wengi wa watafitiwa ni Wakamba na hivyo walipokuwa katika mawanda ya nyumbani waliingiliana sana na jamaa zao ambao ni Wakamba na hivyo kupelekea kutumia Kikamba pekee.

Kauli ifuatayo ya mahojiano na Afisa Mkuu wa Idara ya Nyumba na Ukuaji wa Miji kuhusu wananchi wa maeneo ya mashinani yalitomelea takwimu hizi:

> *Tukiwa maeneo ya mashinani tunatumia Kikamba sana, kikifuatiwa na Kiswahili na kama tutatumia Kiingereza itakuwa kidogo sana kwa sababu wengi wa wananchi ni Wakamba na hata kama si Wakamba, hasa katika maeneo ya mipakana na jamii nyingine wamejua Kikamba kutokana na kukaa hapo kwa muda mrefu* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022).

Hata hivyo, ijapokuwa ruwaza hii ndiyo maarufu kabisa, zipo tofauti ambazo zilijitokeza katika vijiji hivi sita. Mseto wa Kikamba, Kiswahili na Kiingereza ndio unaofuata msimbo wa Kikamba pekee kwa umaarufu katika 15.7%. Hata hivyo, mseto huu ni maarufu katika vijiji vitatu ambavyo ni Grogon, kilicho mjini Machakos, Mlolongo kinachopakana na Nairobi na Kianzambe ambacho pia kinakaribiana sana na mji wa Thika. Ruwaza hii ni maarufu katika maeneo haya kwa sababu watu wanaoishi humo ni wa jamii tofautitofauti ikilinganishwa na vijiji vingine ambavyo wingilugha umesababishwa kwa kiwango kikubwa zaidi na uzingasifa. Tofauti hii inawekewa msingi imara na mahojiano ya maafisa waliohojiwa ambao walitoa kauli mbili zilizokaribiana sana kama ifuatavyo:

> Afisa Mkuu Idara ya Utamaduni: *Katika maeneo ya mipakani yaliyo mijini kutokana na watu wa jamii mbalimbali tunatumia Kiswahili na Kiingereza sana lakini katika maeneo ya vizingasifa vya mashinani, utapata kuwa wengi wa wananchi wanaelewa lugha za jirani zao kwa sababu wameingiliana kwa muda mrefu na wamejifunza lugha za kila jamii na hivyo tunatumia Kikamba na nyakati zingine kuchanganya na Kiswahili*
>
> Afisa Mkuu Kitengo cha Mimea: *...katika maeneo haya ya mashambani takriban asilimia 90 ya wananchi ni Wakamba na katika maeneo vizingasifa, hata wale watu wa jamii jirani wamejifunza Kikamba na hivyo wanatumia Kikamba bila tatizo lolote.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Katika usambazi wa hojaji, kauli hizi za maafisa hawa zilithibitika katika kijiji cha Katulye ambapo mzee mmoja wa jamii ya Aembu ambaye hakujua kuandika

alisema kuwa yeye ameishi katika eneo hilo kwa miaka mingi na alielewa lugha za Kikamba na Kiembu kwa ufasaha. Matokeo haya ya ruwaza za matumizi ya lugha nyumbani yanaoana na mhimili wa upangaji lugha na sera ya lugha huchangia maendeleo ya kielimu wa Kiunzi cha Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi unaoshikilia kuwa lugha ya kwanza huwa muhimu katika mafunzo yanayohusiana na maendeleo ya kijamii, kitamaduni na kimaendeleo. Uelewa na matumizi haya ya lugha ya Kikamba miongoni mwa majirani ambao si Wakamba yanathibitishwa ya kweli kutokana na utambuzi wa nafasi za lugha hii katika maendeleo ya maeneo husika hata kwa watu wa jamii jirani. Vilevile, matokeo haya yanaonyesha pia kuwa umaarufu wa lugha nyingine katika mawanda ya nyumbani uko katika kiwango cha 11.3%, matokeo yanayolingana na yale ya utafiti wa Mwangi (2016) yaliyogundua kuwa katika Narok Kaskazini lugha nyingine zilitumika katika mazungumzo ya nyumbani.

### 4.3.3 Hospitalini

Mawanda ya hospitalini ni mawanda ambayo ni rasmi. Wafanyikazi wake hasa wataalamu wa matibabu mara nyingi huwa wa kutoka jamii mbalimbali. Vilevile, afya ni muhimu kwa wananchi katika utekelezaji wa maendeleo na hivyo lugha inayotumika katika mawanda haya huathiri utekelezaji wa maendeleo kwa njia mbalimbali. Jedwali lifuatalo linaonyesha matokeo ya uchunguzi wa ruwaza za matumizi ya lugha katika mawanda ya hospitalini.

*Jedwali 4.9 Ruwaza za Matumizi ya Lugha Hospitalini*

| | | Kik | Kisw | Kiing | Kisw+ Kik+ Kiing | Kisw+ Kik | Kisw+ Kiing | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Konza | Mdafao | 0 | 1 | 0 | 2 | 6 | 0 | 9 |
| | Asilimia | 0.0% | 11.1% | 0.0% | 22.2% | 66.7% | 0.0% | 100.0% |
| Grogon | Mdafao | 1 | 3 | 1 | 11 | 24 | 1 | 41 |
| | Asilimia | 2.4% | 7.3% | 2.4% | 26.8% | 58.5% | 2.4% | 100.0% |
| Mlolongo | Mdafao | 0 | 14 | 0 | 1 | 2 | 9 | 26 |
| | Asilimia | 0.0% | 53.8% | 0.0% | 3.8% | 7.7% | 34.6% | 100.0% |
| Katulye | Mdafao | 0 | 1 | 0 | 0 | 8 | 0 | 9 |
| | Asilimia | 0.0% | 11.1% | 0.0% | 0.0% | 88.9% | 0.0% | 100.0% |
| Kianzambe | Mdafao | 0 | 2 | 0 | 6 | 11 | 0 | 19 |
| | Asilimia | 0.0% | 10.5% | 0.0% | 31.6% | 57.9% | 0.0% | 100.0% |
| Ndithini | Mdafao | 0 | 4 | 0 | 0 | 6 | 1 | 11 |
| | Asilimia | 0.0% | 36.4% | 0.0% | 0.0% | 54.5% | 9.1% | 100.0% |
| **Jumla** | **Mdafao** | **1** | **25** | **1** | **20** | **57** | **11** | **115** |
| | **Asilimia** | **0.9%** | **21.7%** | **0.9%** | **17.4%** | **49.6%** | **9.6%** | **100.0%** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Kwa mujibu wa takwimu za jumla, msimbo wa Kikamba pekee unatumiwa na mtafitiwa 1 (0.9%) ambazo ni takwimu sawa na wanaotumia msimbo wa Kiingereza pekee. Kwa upande mwingine, msimbo wa Kiswahili pekee ulitokea kuwa maarufu kuliko ule wa Kikamba na Kiingereza kwa sababu unatumiwa na watafitiwa 25 (21.7%). Ilitokea kuwa lugha nyingine pekee hazitumiki katika mawanda ya hospitalini. Kwa upande wa miseto ya lugha, mseto wa Kiswahili na Kikamba ndio maarufu zaidi ukitumiwa na watafitiwa 57 (49.6%) takwimu ambazo zinaonyesha kuwa takribani nusu ya wakazi wa maeneo yenye wingilugha hutumia mseto huu katika muktadha wa matibabu. Mseto wa Kikamba, Kiswahili na Kiingereza unafuata kwa umaarufu kwa kutumiwa na watafitiwa 20 (17.4%) huku mseto wa Kikamba na Kiingereza ukitumiwa na watafitiwa 11 (9.6%). Takwimu hizi za jumla zinatokana na takwimu za vijiji ambapo umaarufu wa mseto wa Kikamba na Kiswahili unasambaa katika vijiji vyote sita isipokuwa Mlolongo, ambapo katika kijiji cha Konza mseto huu unatumika na 66.7% ya watafitiwa wa kijiji hicho, katika kijiji cha Grogon

58.5%, katika kijiji cha Mlolongo 7.7%, katika kijiji cha Katulye 88.9%, katika kijiji cha Kianzambe 57.9%. na katika kijiji cha Ndithini 54.5%.

Tofauti inayojitokeza katika kijiji cha Mlolongo inatomelewa na ukweli kuwa ni eneo linalopakana na mji wa Nairobi ambapo kwa mujibu wa Kamau (2015) takriban lugha zote za Kenya huzungumzwa hali inayoeleza umaarufu wa msimbo wa Kiswahili pekee katika 53.8% na mseto wa Kiswahili na Kiingereza ambao unatumiwa na 34.6% ya watafitiwa wa eneo hilo. Tofauti hii ya kijiji cha Mlolongo ilifafanuliwa zaidi na kauli ifuatayo ya Afisa Mkuu wa Idara ya Nyumba na Ukuaji wa Miji.

> *Tukiwa katika mazingira ya mijini, hali hubadilika kwa sababu tunatumia Kiswahili zaidi kikifuatiwa na matumizi ya Kiingereza na iwapo Kikamba kitatumika, kitatumika kidogo sana kwa sababu katika maeneo haya kuna watu ambao si Wakamba na hawaelewi Kikamba kabisa. Mfano mzuri ni eneo la Mlolongo ambako kuna jamii nyingi ambazo zinaishi huko, ikilinganishwa na mjini Machakos* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Ukweli wa hali hii katika mawanda ya hospitalini ulidhihirika zaidi katika mahijiano na Afisa Mkuu Idara ya Biashara ambaye katika kujibu swali kuhusu matumizi ya nyaraka alitoa mfano na mawanda ya hospitalini kuwa:

> *…katika masuala ya afya nyaraka na maandishi yataweza kuwa katika lugha za Kiingereza, Kiswahili na nyakati zingine Kikamba.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Ijapokuwa hakuna utafiti unaoonyesha ruwaza za matumizi ya lugha katika muktadha wa hospitalini kati ya zile zilizohakikiwa, ni muhimu kutambua kwamba mawanda ya hospitalini ni rasmi kama yalivyo ya shuleni. Katika tafiti za Nursanti na wenzake (2020), Kevogo na wenzake (2015) na Wamalwa na wenzake (2019) ruwaza za matumizi ya lugha shuleni, ambayo ni mazingira rasmi kama yalivyo ya hospitalini zinaonekana kuchukua mkondo unaofanana kwa sababu matumizi ya lugha rasmi na za taifa ni ya juu ikilinganishwa na

matumizi ya lugha asili. Kwa kina zaidi, utafiti wa Nursanti na wenzake (2020) unaonyesha kuwa katika mazingira ya nyumbani, Kijavani hutumika zaidi na pale ambapo wahusika ni wazee lahaja ya Kikrama hutumia zaidi lakini katika matangazo ya habari, wanafunzi hawa wenye wingilugha hutumia Kibahasa Indonesia, ambayo ndiyo lingua franka ya kitaifa zaidi ikilinganishwa na Kijavani na Kiingereza huku Kiingereza kikitumika zaidi chuoni pale wanapoingiliana na wanafunzi wa mataifa mengine. Hivyo matokeo haya yanaendana na ya utafiti huu katika mawanda rasmi ya hospitalini kwa sababu matumizi ya Kikamba ni ya kiwango cha chini sawa na Kiingereza tofauti na yalivyo matumizi ya lugha ya Kiswahili. Vilevile, matokeo haya yanasisitizwa na mhimili wa wingilugha na maendeleo wa Kiunzi cha Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi kwa sababu lugha za Kiswahili na Kiingereza, kama mbili za fomyula ya lugha tatu ya eneo hili, zinatumika katika mazingira haya ya hospitalini kutokana na urasmi wa mawanda haya.

### 4.3.4 Shambani

Mawanda haya yalizingatiwa na utafiti huu kwa sababu ni muhimu sana katika maendeleo ya uchumi na mingi ya miradi ya maendeleo ya Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi hulenga mawanda haya. Matokeo ya data za nyanjani ya ruwaza za matumizi ya lugha yalitofautiana na mawanda mengine hata katika kijiji cha Mlolongo kinachopakana na mji wa Nairobi kama ilivyo katika jedwali lifuatalo.

*Jedwali 4.10 Ruwaza za Matumizi ya Lugha Shambani*

| | | Kik | Kisw | L.N | Kisw+ Kik+ Kiing | Kisw+ Kik | Kisw+ Kiing | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Konza | Mdafao | 8 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 9 |
| | Asilimia | 88.9% | 0.0% | 0.0% | 0.0% | 11.1% | 0.0% | 100.0% |
| Grogon | Mdafo | 31 | 3 | 0 | 2 | 4 | 1 | 41 |
| | Asilimia | 75.6% | 7.3% | 0.0% | 4.9% | 9.8% | 2.4% | 100.0% |
| Mlolongo | Mdafao | 8 | 9 | 4 | 1 | 3 | 1 | 26 |
| | Asilimia | 30.8% | 34.6% | 15.4% | 3.8% | 11.5% | 3.8% | 100.0% |
| Katulye | Mdafao | 6 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 9 |
| | Asilimia | 66.7% | 11.1% | 0.0% | 0.0% | 22.2% | 0.0% | 100.0% |
| Kianzambe | Mdafao | 13 | 1 | 1 | 0 | 4 | 0 | 19 |
| | Asilimia | 68.4% | 5.3% | 5.3% | 0.0% | 21.1% | 0.0% | 100.0% |
| Ndithini | Mdafao | 6 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 10 |
| | Asilimia | 60.0% | 20.0% | 0.0% | 0.0% | 20.0% | 0.0% | 100.0% |
| **Jumla** | **Mdafao** | **73** | **17** | **5** | **3** | **14** | **2** | **114** |
| | **Asilimia** | **64.0%** | **14.9%** | **4.4%** | **2.6%** | **12.3%** | **1.8%** | **100.0%** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Matokeo haya yanaonyesha msimbo wa Kikamba pekee kuwa maarufu zaidi katika mawanda ya shambani kwa kutumiwa na jumla ya watafitiwa 73 (64.0%). Umaarufu huu unasambaa pia katika vijiji vyote husika kwa sababu matumizi yake miongoni mwa watafitiwa ni kama ifuatavyo: Konza 8 (88.9%), Grogon 31 (75.6%), Mlolongo 8 (30.8%), Katulye 6 (66.7%), Kianzambe 13 (68.4%), na Ndithini 7 (70.0%). Hali hii ni tofauti kabisa na misimbo ya Kiswahili pekee, Kiingereza pekee, na lugha nyingine pekee kwa sababu kwa jumla matumizi ya misimbo hii ni ya chini katika viwango vya 14.9%, 0.0% na 4.4% mtawalia. Katika vijiji vya Mlolongo na Grogon, japo ni mawanda yalio mjini, zipo sehemu za nje ya mji ambako shughuli za ukulima hufanyika na vilevile upandaji wa mboga kutumia magunia maalumu katika maeneo ya kuishi. Matokeo haya yanaongeza uthabiti wa msingi kuwa wingilugha wa kijiji cha Mlolongo ni tofauti na wingilugha wa eneo la Grogon mjini Machakos kutokana na umaarufu

wa matumizi ya lugha nyingine. Katika kijiji cha Mlolongo lugha nyingine zinatumiwa na 15.4% ikilinganisha na eneo la Grogon ambapo hakuna watu wanaotumia lugha nyingine pekee katika mawanda ya shambani.

Katika upande wa miseto, mseto wa Kiswahili na Kikamba unatumika zaidi ikilinganishwa na miseto mingine kwa sababu unatumiwa na watafitiwa 14 (12.3%), huku mseto wa Kikamba, Kiswahili na Kiingereza ukitumika na watafitiwa 3 (2.6%) na ule wa Kiswahili na Kiingereza ukitumiwa na watafitiwa 2 (1.8%) katika vijiji hivi. Mseto wa Kikamba na Kiingereza hautumiwi katika mawanda ya shambani kwa mujibu wa matokeo haya.

Matokeo haya yalifanana na matokeo ya uchunzaji ambapo katika kijiji cha Katulye, kuliko na mashamba ya mboga ya kunyunyizia karibu na bwawa la Masinga, wengi wa wakulima walitumia Kikamba na wanapochanganya lugha basi kwa kiwango kikubwa walichanya na Kiswahili hali sawa na katika vijiji vingine isipokuwa Mlolongo. Mahojiano na Afisa Mkuu wa Kitengo cha Mimea yalishabiiana na matokeo haya katika kauli ifautayo:

> *Katika maeneo ya mjini utapata kuna watu wa kila aina na hivyo tunachanganya lugha zote tatu lakini mashinani ambapo Wakamba huwa takriban asilimia 90 tunatumia Kikamba sana na kuchanganya na Kiswahili pale panapohitajika…* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Hivyo kutokana na matokeo haya, lugha za Kiswahili, Kikamba na Kiingereza zina nafasi maalumu katika mawanda ya shambani kwa sababu kila moja inatumika kwa njia inayoendeleza utekelezaji wa maendeleo kwa njia ya kipekee. Matokeo haya ni dhihirisho kamili ya pendekezo la Kiunzi cha Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi katika mhimili wa wingilugha na maendeleo unaopendekeza matumizi ya fomyula tatu: lugha asili,

lingua franka ya kitaifa na lugha ya kimataifa kama njia bora ya kuhakikisha maendeleo katika mazingira yenye wingilugha.

### 4.3.5 Kazini

Kama ambavyo Sridhar (1996) anafafanua, baadhi ya masuala ya kimsingi katika wingilugha huwa ni hadhi na majukumu ya lugha husika katika jamii na mahusiano kati ya matumizi ya lugha na vipengele vya kijamii. Kipengele cha kazi ni muhimu sana katika maendeleo ya binadamu ya kiuchumi na hivyo utafiti huu kuchunguza ruwaza za matumizi ya lugha ya kazini. Jedwali lifuatalo linaonyesha ruwaza za matumizi ya lugha katika mawanda haya.

***Jedwali 4.11 Ruwaza za Matumizi ya Lugha Kazini***

| | | **Kik** | **Kisw** | **Kik+ Kisw+ Kiing** | **Kisw+ Kik** | **Kisw+ Kiing** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Konza | Mdafao | 1 | 1 | 2 | 5 | 0 | 9 |
| | Asilimia | 11.1% | 11.1% | 22.2% | 55.6% | 0.0% | 100.0% |
| Grogon | Mdafao | 4 | 2 | 14 | 19 | 2 | 41 |
| | Asilimia | 9.8% | 4.9% | 34.1% | 46.3% | 4.9% | 100.0% |
| Mlolon go | Mdafao | 0 | 6 | 4 | 9 | 7 | 26 |
| | Asilimia | 0.0% | 23.1% | 15.4% | 34.6% | 26.9% | 100.0% |
| Katulye | Mdafao | 4 | 2 | 0 | 3 | 0 | 9 |
| | Asilimia | 44.4% | 22.2% | 0.0% | 33.3% | 0.0% | 100.0% |
| Kianza mbe | Mdafao | 5 | 1 | 3 | 9 | 1 | 19 |
| | Asilimia | 26.3% | 5.3% | 15.8% | 47.4% | 5.3% | 100.0% |
| Ndithin i | Mdafao | 4 | 1 | 0 | 5 | 1 | 11 |
| | Asilimia | 36.4% | 9.1% | 0.0% | 45.5% | 9.1% | 100.0% |
| **Jumla** | **Mdafao** | **18** | **13** | **23** | **50** | **11** | **115** |
| | **Asilimia** | **15.7%** | **11.3%** | **20.0%** | **43.5%** | **9.6%** | **100.0%** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Mawanda ya kazini huwa mapana mno na hutofautiana kulingana na kazi husika. Yapo mawanda ya kazini ambayo huwa rasmi na mengine yasiyo rasmi. Katika uchunguzi huu, mawanda ya kazini yalihusisha yaliyo rasmi na yasiyo rasmi.

Kutokana na takwimu hizi, kwa jumla msimbo wa Kikamba pekee unatumiwa na watafitiwa 15 (15.7%) huku ule wa Kiswahili pekee ukitumiwa na 13 (11.3%). Misimbo ya Kiingereza na lugha nyingine pekee haitumiki. Mseto wa Kikamba na Kiswahili ndio maarufu zaidi katika mawanda ya kazini kwa sababu ulitumiwa na watafitiwa 50 (43.5%) ukifuatiwa na mseto wa Kikamba, Kiswahili na Kiingereza ambao ulitumiwa na watafitiwa 23 (20.0%). Japo kwa kiwango cha chini cha 9.6% (watafitiwa 11), mseto wa Kiswahili na Kiingereza ulitumika katika mawanda haya ya kazini. Kwa mujibu wa vijiji maalumu, uchanganuzi unaonyesha kuwa katika vijiji vya Katulye, Kianzambe na Ndithini, matumizi ya msimbo wa Kikamba pekee ni maarufu zaidi kuliko misimbo ya Kiswahili pekee, Kiingereza pekee, na lugha nyingine pekee kama ilivyo katika jedwali. Pia, katika vijiji hivi, mseto wa Kikamba na Kiswahili ni maarufu zaidi ikilinganishwa na miseto mingine.

Kwa upande mwingine, katika vijiji vya Konza, Grogon na Mlolongo matumizi ya msimbo wa Kikamba pekee ulipungua huku mseto wa Kikamba na Kiswahili ukiongezeka kwa umaarufu ikilinganishwa na vijiji vya Katulye, Kianzambe na Ndithini. Hata hivyo, katika mawanda haya ya kazini, tofauti ilitokea katika kijiji cha Konza kilicho maeneo ya mashambani ambapo umaarufu wa msimbo wa Kikamba pekee ulipungua ikilinganishwa na mawanda mengine. Katika kutathmini hali hii, katika mahojinao na Afisa Mkuu wa Idara ya Utamaduni, afisa huyu alisema kuwa:

> *Tofauti ya maeneo ya mipakani ni katika Kaunti ya Kajiado kuliko na Wamaasai ambao uelewa wao wa Kikamba ni wa kiwango cha chini ikilinganishwa na maeneo tunayopakana na Wagikuyu na Aembu na katika eneo hili tunatumia Kiswahili zaidi.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Kauli hii inaonyesha sababu ya upunguaji wa umaarufu wa msimbo wa Kikamba pekee hasa katika mawanda ya kazini unatokana na ujio wa watu wa asili mbalimbali wanaofanya kazi katika eneo hilo linaloendelea kubadilika. Matokeo haya yanalandana na mhimili wa lugha na maendeleo ya binadamu wa Kiunzi cha Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi ambao unasisitiza kuwa lugha ni sehemu ya utamaduni wowote ule na kuwa huchangia katika kuumba na kuendeleza utamaduni. Katika mawanda haya ya kazini, upunguaji wa matumizi ya lugha ya Kikamba na uongezekaji wa matumizi ya lugha za Kiswahili na Kiingereza unaatambua utamaduni wa wingilugha unaohusisha watu wa jamii mbalimbali. Katika sehemu ya uhakiki wa maandishi, utafiti wa Wamalwa na wenzake (2019) unaonyesha ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa walimu wa shule za msingi. Katika utafiti wao, mazingira ya shuleni yalihusisha mazingira ya kazini miongoni mwa walimu hawa, hali inayoonyesha ulinganifu na sehemu hii ya utafiiti huu. Matokeo yalionyesha kuwa matumizi ya msimbo wa Kiingereza pekee yalikuwa ya kiwango cha juu katika mazingira rasmi kama vile kwenye gwaride, ofisini, na katika mazungumzo na walimu wenzao na wanafunzi ikilinganishwa na misimbo ya Kiswahili na Kiluo ikifuatiwa na msimbo wa Kiswahili. Kwa upande wa miseto ya lugha, mseto wa Kiswahili, Kiingereza na Kiluo ndio ulitumika katika mazingira ya shuleni. Matokeo haya yanatofautiana na matokeo ya utafiti huu kwa sababu katika maeneo haya ya kazini wengi wa watafitiwa wanatumia mseto wa Kiswahili na Kikamba kuliko mseto wa Kiswahili, Kiingereza na Kikamba. Hata hivyo, tofauti hii inajitokeza kwa sababu utafiti wao ulifanywa katika mazingira rasmi ya shuleni ilhali utafiti huu ulihusisha yale rasmi na yasiyo rasmi. Vilevile, utafiti wao ulilenga walimu pekee ambao

wana kiwango cha juu cha elimu ikilinganishwa na huu ambao ulilenga wananchi wote walio na umri wa zaidi ya miaka 18 kama inavyoonyeshwa katika sehemu ya 4.2.3. Hata hivyo, matokeo ya mahojiano na wasimamizi mbili wa idara zilizohusishwa ambao wanafanya kazi katika mazingira rasmi yalilandana sana na haya ya utafiti wao. Kauli zao kuhusu matumizi ya lugha katika mazingira rasmi zilikuwa kama ifuatavyo:

> Afisa Mkuu Idara ya Biashara: *Tunanchanganya lugha hizi kwa sababu nimeona kwamba Kiswahili ni lugha ngumu kwa watu wengi na si kila mtu anaweza kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha pasipo na kuchanganya na Kiingereza.*
>
> Afisa Mkuu Idara ya Utamaduni: *Kikazi na katika shughuli rasmi na wafanyikazi wengine ni lugha ya Kiingereza inayotumika zaidi lakini katika mawasiliano yasiyorasmi na kuwahudumia wananchi ni Kiswahili kwa sababu unawezekana kuwa hajui Kiingereza vizuri ama Kikamba.*

Matokeo haya yanaonyesha wazi kuwa lugha katika mazingira ya kazini inatumika kwa namna tofautitofauti kutegemea muktadha wa kazi mbalimbali. Muhimu zaidi ni kuwa kwa mujibu wa matokeo haya, lugha za Kiswahili, Kikamba na Kiingereza zina nafasi maalumu katika mawanda ya kazini.

### 4.3.6 Mikutano ya Michakato ya Maendeleo

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza wingilugha na athari zake katika utekelezaji wa maendeleo Kaunti ya Machakos. Mojawapo ya hatua kuu ya uundaji sera za maendeleo ni ushirikishwaji umma katika mchakato huu. Maafisa wa Kaunti ya Machakos waliohojiwa walisema kuwa lugha huwa kigezo muhimu katika mchakato wa maendeleo katika hatua ya ushirikishwaji umma. Ili ushirikishwaji umma kufanyika, waundaji sera za maendeleo hutumia mikutano ya umma kuwafikia wananchi na kuchukua maoni yao. Vilevile, baada

ya sera husika kuundwa na kupitishwa na mamlaka husika, sera hizi huwasilishwa kwa wananchi ili kuzielewa ambapo lugha hutumiwa. Utafiti huu ulichunguza ruwaza za matumizi ya lugha katika mikutano ya michakato ya maendeleo ili kukadiria namna lugha inavyotumika katika mchakato huu wa ushirikishwaji umma na uwasilishwaji wa sera za maendeleo.

***Jedwali 4.12 Ruwaza za Matumizi ya Lugha katika Mikutano ya Michakato ya Maendeleo***

| | | | | | | | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Kik** | **Kisw** | **Kiing** | **Kisw+ Kik+ Kiing** | **Kisw+ Kik** | **Kisw+ Kiing** | |
| Konza | Mdafao | 3 | 0 | 0 | 1 | 5 | 0 | 9 |
| | Asilimia | 33.3% | 0.0% | 0.0% | 11.1% | 55.6% | 0.0% | 100.0% |
| Grogon | Mdafao | 6 | 2 | 0 | 12 | 19 | 2 | 41 |
| | Asilimia | 14.6% | 4.9% | 0.0% | 29.3% | 46.3% | 4.9% | 100.0% |
| Mlolong o | Mdafao | 0 | 10 | 1 | 3 | 6 | 6 | 26 |
| | Asilimia | 0.0% | 38.5% | 3.8% | 11.5% | 23.1% | 23.1% | 100.0% |
| Katulye | Mdafao | 6 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 9 |
| | Asilimia | 66.7% | 11.1% | 0.0% | 0.0% | 22.2% | 0.0% | 100.0% |
| Kianza mbe | Mdafao | 8 | 1 | 0 | 3 | 6 | 1 | 19 |
| | Asilimia | 42.1% | 5.3% | 0.0% | 15.8% | 31.6% | 5.3% | 100.0% |
| Ndithini | Mdafao | 4 | 2 | 0 | 1 | 3 | 1 | 11 |
| | Asilimia | 36.4% | 18.2% | 0.0% | 9.1% | 27.3% | 9.1% | 100.0% |
| **Jumla** | **Mdafao** | **27** | **16** | **1** | **20** | **41** | **10** | **115** |
| | **Asilimia** | **23.5%** | **13.9%** | **0.9%** | **17.4%** | **35.7%** | **8.7%** | **100.0%** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Uchanganuzi huu unaonyesha kuwa lugha inatumika kwa namna tofauti katika vijiji lengwa vya utafiti huu. Katika kijiji cha Konza msimbo wa Kikamba pekee unatumika na watafitiwa 3 (33.3%) katika mikutano hii huku misimbo ya Kiswahili pekee, Kiingereza pekee na lugha nyingine pekee ikiwa haitumiki hata kidogo (0.0%). Mseto wa Kikamba, Kiswahili na Kiingereza nao unatumika na mtafitiwa 1 (11.1%) huku ule wa Kikamba na Kiswahili ukiwa maarufu zaidi kwa kutumiwa na watafitiwa 5 wanaowakilisha 55.6% ya watafitiwa wa eneo

hili. Tofauti na miseto hii, miseto ya Kiswahili na Kiingereza na Kikamba na Kiingereza haitumiwi hata kidogo. Katika kijiji cha Grogon, ruwaza za matumizi ya lugha zilihusisha Kikamba pekee (14.6%), Kiswahili pekee (4.9%), Kiingereza pekee (0.0%), mseto wa Kikamba, Kiswahili na Kiingereza (29.3%), mseto wa Kiswahili na Kikamba (46.3%), mseto wa Kiswahili na Kiingereza (4.9%) na mseto wa Kikamba na Kiingereza (0.0%). Katika kijiji cha Grogon, Kikamba pekee ndio maarufu zaidi kuliko misimbo mingine yote huku mseto wa Kikamba na Kiswahili ukiwa maarufu zaidi kuliko miseto mingine yote. Hata hivyo, mseto wa Kikamba na Kiswahili ni maarufu zaidi kuliko msimbo wa Kikamba pekee, hali inayoonyesha umuhimu wa Kiswahili katika mazingira wa wingilugha.

Katika kijiji cha Mlolongo ruwaza za matumizi ya lugha zilitokea kuwa hakuna watafitiwa wanaotumia Kikamba pekee, 10 (38.5%) wanatumia Kiswahili pekee, 1 (3.8%) wanatumia Kiingereza pekee, 3 (11.5%) wanatumia mseto wa Kikamba, Kiswahili na Kiingereza, 6 (23.1%) nao wanatumia mseto wa Kiswahili na Kikamba takwimu sawa na wanaotumia mseto wa Kiswahili na Kiingereza 6 (23.1%). Tofauti kuu kati ya kijiji hiki na kile cha Grogon ni kuwa umaarufu wa msimbo wa Kikamba pekee ulipungua kutoka 33.3% katika kijiji cha Grogon hadi 14.6% huku wa Kiswahili pekee na Kiingereza pekee ukiongezeka kutoka 4.9% hadi 38.5 % na 0.0% hadi 3.8% mtawalia. Pia umaarufu wa mseto wa Kikamba na Kiswahili na wa Kikamba, Kiswahili na Kiingereza ulipungua kutoka 46.3% hadi 23.1% na 29.3% hadi 11.5% mtawalia huku umaarufu wa mseto wa Kiswahili na Kiingereza ukiongereza kutoka 4.9% hadi 23.1%. Katika vijiji vya Katulye, Kianzambe na Ndithini, ruwaza za matumizi ya lugha zilichukua mfumo sawa japo kwa asilimia tofauti. Ruwaza

katika kijiji cha Katulye zilikuwa Kikamba pekee 6 (66.7%), Kiswahili pekee 1 (11.1%), Kiingereza pekee 0 (0.0%), mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza 0 (0.0%), mseto wa Kiswahili na Kikamba 2 (22.2%) na mseto wa Kiswahili na Kiingereza 0 (0.0%).

Katika kijiji cha Kianzambe, ruwaza zilitokea kuwa Kikamba pekee 8 (42.1%), Kiswahili pekee 1 (5.3%), Kiingereza pekee 0 (0.0%), mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza 3 (15.8%), mseto wa Kiswahili na Kikamba 6 (31.6%) na mseto wa Kiswahili na Kiingereza 1 (5.3%). Matokeo ya kijiji cha Ndithini yalionyesha kuwa watafitiwa 4 (36.4%) wanatumia Kikamba pekee, 2 (18.2%) wanatumia Kiswahili pekee, 0 (0.0%) wanatumia Kiingereza pekee, 1 (9.1%) hutumia mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza, 6 (27.3%) wanatumia mseto wa Kikamba na Kiswahili huku 1 (9.1%) akitumia mseto wa Kiswahili na Kiingereza katika mikutano ya michakato ya maendeleo.

Katika matokeo haya, matumizi ya msimbo wa Kikamba pekee una umaarufu mkubwa katika maeneo vizingasifa ya mashinani ikilinganishwa na maeneo vizingasifa ya mjini. Matokeo haya yanaonyesha uongezekaji wa umaarufu wa msimbo wa Kiingereza pekee na miseto inayohusisha Kiingereza katika maeneo ya vizingasifa ya mjini ikilinganishwa na yale ya mashinani. Katika mahojiano na wakuu wa idara nne lengwa, kauli zao zinathibitisha ruwaza hizi katika mikutano ya ushirikishaji umma katika miradi ya maendeleo. Zaidi, mhimili wa wingilugha na maendeleo wa Kiunzi cha Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi unaweka msingi thabiti kwa matokeo haya, hasa kupitia kwa pendekezo lake la matumizi ya fomyula ya lugha tatu katika maeneo ya wingilugha ili kuhakikisha maendeleo ambapo, lugha za Kikamba, Kiswahili na Kiingereza zinatumika katika mikutano hii ambayo ni kiini kikubwa katika

utekelezaji wa maendeleo. Vilevile, mhimili wa kiunzi hiki wa nafasi ya lugha katika mifumo ya ubunifu ya kitaifa unathibitisha matokeo haya kwa kuthibitisha upekee wa Kaunti ya Machakos wa matumizi ya lugha katika mikutano hii kama njia mojawapo ya kuhakikisha utekelezaji bora wa maendeleo.

#### 4.3.7 Mafunzo ya Kilimo

Katika muktadha wa maendeleo ya kaunti nchini Kenya, kilimo huchukua sehemu kubwa ya shughuli za wananchi. Katika Kaunti ya Machakos, kilimo ndiyo kazi kuu kwa wananchi kwa jumla hasa wale wanaoishi katika maeneo ya mashinani. Serikali ya Kaunti ya Machakos ina miradi kadhaa ya kilimo inayotekelezwa na wananchi na huhusisha mafunzo ili kuwasaidia wananchi kuongeza mazao katika mazingira ya misimu mifupi ya mvua kama lilivyo eneo la Mashariki mwa Kenya kwa jumla. Ukweli wa miradi hii ni kauli ya Afisa Mkuu wa Kitengo cha Mimea:

> *Katika Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi tuna miradi ambayo tunaendelea kutekeleza ambayo ni Small Scale Irrigation and Value Addition (SIVAP), Kenya Cereal Enhancement Program- Climate Resilient Agriculture for Livelihood (KCEP-CRAL), Agriculture Sector Support Program II (ASSP II) na Kenya Climate Smart Agriculture Project (KCSAP). Katika miradi hii yote tunatumia mbinu ya vikundi na hatushirikishi mhusika mmoja.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Matokeo ya uchanganuzi wa ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa watafitiwa katika mafunzo ya kilimo yanawasilishwa katika jedwali lifuatalo:

***Jedwali 4.13 Ruwaza za Matumizi ya Lugha katika Mafunzo ya Kilimo***

| | | | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Kik** | **Kisw** | **Kiing** | **Kisw+ Kik+ Kiing** | **Kisw+ Kik** | **Kisw+ Kiing** | |
| Konza | Mdafao | 1 | 0 | 0 | 3 | 5 | 0 | 9 |
| | Asilimia | 11.1% | 0.0% | 0.0% | 33.3% | 55.6% | 0.0% | 100.0% |
| Grogon | Mdafao | 5 | 2 | 0 | 13 | 19 | 2 | 41 |
| | Asilimia | 12.2% | 4.9% | 0.0% | 31.7% | 46.3% | 4.9% | 100.0% |
| Mlolong o | Mdafao | 0 | 10 | 1 | 3 | 7 | 5 | 26 |
| | Asilimia | 0.0% | 38.5% | 3.8% | 11.5% | 26.9% | 19.2% | 100.0% |
| Katulye | Mdafao | 6 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 9 |
| | Asilimia | 66.7% | 11.1% | 0.0% | 0.0% | 22.2% | 0.0% | 100.0% |
| Kianzam be | Mdafao | 5 | 1 | 0 | 4 | 8 | 1 | 19 |
| | Asilimia | 26.3% | 5.3% | 0.0% | 21.1% | 42.1% | 5.3% | 100.0% |
| Ndithini | Mdafao | 4 | 2 | 0 | 1 | 2 | 2 | 11 |
| | Asilimia | 36.4% | 18.2% | 0.0% | 9.1% | 18.2% | 18.2% | 100.0% |
| **Jumla** | **Mdafao** | **21** | **16** | **1** | **24** | **43** | **10** | **115** |
| | **Asilimia** | **18.3%** | **13.9%** | **0.9%** | **20.9%** | **37.4%** | **8.7%** | **100.0%** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Katika matokeo haya, tofauti zinajitokeza kati ya maeneo ya mjini na maeneo ya mashinani ambapo katika vijiji vya Grogon na Mlolongo, vilivyo maeneo ya mjini, na katika kijiji cha Konza matumizi ya msimbo wa Kikamba pekee ni ya chini katika viwango vya 12.2%, 0.0% na 11.1% mtawalia. Hali hii ni tofauti na vijiji vya Katulye, Kianzambe na Ndithini vilivyo mashinani ambapo msimbo huu unatumika na 66.7%, 26.3% na 36.4% ya watafitiwa wa vijiji hivi. Kijiji cha Konza, kilicho katika maeneo ya mashambani kina matumizi duni ya msimbo wa Kikamba pekee hali ambayo ilitokana na hali kuwa kilimo katika eneo hili huhusisha sana ufugaji wa mifugo kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na ukulima wa mimea na pia majirani wa Kaunti ya Machakos katika eneo hili ni Wamaasai ambao ni Wanailoti ambao uelewa wao wa Kikamba ni duni ikilinganishwa na Waembu na Wagikuyu ambao ni Wabantu kama walivyo Wakamba katika vijiji vya Katulye, Kianzambe na Ndithini.

Vilevile, jedwali hili linaonyesha kuwa mseto wa Kikamba na Kiswahili bado ndio maarufu zaidi katika mafunzo ya kilimo. Hata hivyo, ni wazi kuwa umaarufu wa miseto ya lugha inayohusisha matumizi ya lugha ya Kiingereza umeongezeka ikilinganishwa na mawanda mengine. Hali hii inafafanuliwa na Afisa Mkuu wa Kitengo cha Mimea katika Idara ya Kilimo ambaye katika mahojiano alisema kuwa,

> *Tunachanganya lugha katika mafunzo ya kilimo na Kiingereza hutumika kwa sababu kuna baadhi ya maneno ambayo tafsiri yake kwa Kiswahili na Kikamba haipo kama vile mbolea ya DAP na DAN.*
> (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Matokeo haya ya matumizi ya lugha katika mafunzo ya kilimo yanaendana na mhimili wa wingilugha na maendeleo wa Kiunzi cha Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi kinachopendekeza matumizi ya fomyula ya lugha tatu katika wingilugha ili kuhakikisha maendeleo kwa sababu lugha za Kikamba, Kiswahili na Kiingereza zinatumika kutimiza malengo mbalimbali.

### 4.3.8 Biashara

Mawanda ya mwisho yaliyotafitiwa yalikuwa ya biashara. Katika ufafanuzi wa nduni ya kazi wanazozifanya watafitiwa, asilimia kubwa yao (33.0%) ni wafanyabiashara. Asilimia hii inaonyesha nafasi ya biashara katika maendeleo ya Kaunti ya Machakos. Jedwali lifuatalo linawakilisha matokeo ya uchanganuzi wa ruwaza za matumizi ya lugha katika mawanda ya biashara:

***Jedwali 4.14 Ruwaza za Matumizi ya Lugha katika Mawanda ya Biashara***

| | | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Kik** | **Kisw** | **Kisw+ Kik+ Kiing** | **Kisw+ Kik** | **Kisw+ Kiing** | |
| Konza | Mdafao | 0 | 0 | 1 | 8 | 0 | 9 |
| | Asilimia | 0.0% | 0.0% | 11.1% | 88.9% | 0.0% | 100.0% |
| Grogon | Mdafao | 2 | 2 | 15 | 21 | 1 | 41 |
| | Asilimia | 4.9% | 4.9% | 36.6% | 51.2% | 2.4% | 100.0% |
| Mlolong o | Mdafao | 0 | 7 | 8 | 9 | 2 | 26 |
| | Asilimia | 0.0% | 26.9% | 30.8% | 34.6% | 7.7% | 100.0% |
| Katulye | Mdafao | 2 | 1 | 0 | 6 | 0 | 9 |
| | Asilimia | 22.2% | 11.1% | 0.0% | 66.7% | 0.0% | 100.0% |
| Kianzam be | Mdafao | 1 | 1 | 3 | 14 | 0 | 19 |
| | Asilimia | 5.3% | 5.3% | 15.8% | 73.7% | 0.0% | 100.0% |
| Ndithini | Mdafao | 3 | 2 | 2 | 4 | 0 | 11 |
| | Asilimia | 27.3% | 18.2% | 18.2% | 36.4% | 0.0% | 100.0% |
| **Jumla** | **Mdafao** | **8** | **13** | **29** | **62** | **3** | **115** |
| | **Asilimia** | **7.0%** | **11.3%** | **25.2%** | **53.9%** | **2.6%** | **100.0%** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Kwa mujibu wa matokeo haya, kwa jumla watafitiwa 8 (7.0%) hutumia msimbo wa Kikamba pekee katika mawanda ya biashara, 13 (11.3%) hutumia msimbo wa Kiswahili pekee huku misimbo ya Kiingereza pekee na lugha nyingine pekee ikiwa na 0.0% kumaanisha kuwa haitumiki kabisa. Mseto wa Kikamba, Kiswahili na Kiingereza nao unatumika na watafitiwa 29 (25.2%), wa Kikamba na Kiswahili na watafitiwa 62 (53.9%) huku wa Kiswahili na Kiingereza ukitumiwa na 3 (2.6%). Kwa upande wa uundaji na usambazaji wa sera za maendeleo, Afisa Mkuu wa Kitengo cha Biashara katika Kaunti ya Machakos alisema kuwa,

> *Tunapotaka kuwafikia wananchi mijini, sanasana tunatumia lugha rasmi, Kiswahili na Kiingereza lakini mashinani ambako watu wengi wanaongea lugha za mama tunatumia Kikamba. Tunatumia lugha kutegemea mazingira na wasikilizaji. Katika maeneo ya mashinani pia, kabla ya kuanza mkutano, huwa tunauliza kama yupo mtu asiyeelewa Kikamba na tunapopata mmoja inalazimu tutumie*

> *Kiswahili ili tueleweke na kila mmoja na nyakati nyingine kuchanganya Kiswahili na Kikamba kwa sababu maeneo kama haya huwa pia na watu ambao hawaelewi Kiswahili. (*Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Afisa huyu alipoulizwa kuhusu uwezekano wa kuacha nyuma baadhi ya wananchi katika kuchanganya lugha kutokana na kutoelewa baadhi ya mawazo yanayosemwa kwa lugha wasiyoielewa alisema kuwa:

> *Iwapo tunapata hali kama hii, tunatumia lugha moja kisha kukalimani kwa ile nyingine mara hiyo tu.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Kauli hizi zinaonyesha kuwa maafisa wa Kaunti ya Machakos wanatambua ukweli wa data za kipengele cha 2.4.2 na 2.4.3 kinachoonyesha uwepo wa wananchi ambao ni wazee na ambao hawajawahi soma katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo. Matokeo ya uchunzaji yalithibitisha ruwaza hizi ambapo katika biashara za vizingasifa vya mashinani, lugha ya Kiswahili ilitumiwa katika biashara kwa kiwango cha juu huku Kikamba kikitumika na wale ambao wanajuana sana. Katika uchunzaji huu, mtafiti alikaribishwa katika maeneo mbalimbali kwa kutumia Kiswahili kwa sababu hakujulikana lakini wenyeji walitumia Kikamba au mseto wa Kikamba na Kiswahili katika shughuli za biashara.

Kwa jumla, kutokana na matokeo haya, matumizi ya lugha huchukua ruwaza tofautitofauti katika mawanda haya mbalimbali kutegemea sababu tofautitofauti. Hivyo, katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo katika Kaunti ya Machakos, ruwaza hizi ni muhimu ili kuhakikisha kwamba maendeleo lengwa yanatekelezwa kwa ufasaha zaidi na kuwanufaisha wananchi ambao ndio walengwa wakuu wa miradi husika ya maendeleo.


### 4.4. Uhusiano na Athari za Lugha Mbalimbali kwa Utekelezaji wa Maendeleo

Sehemu hii ililenga kuchunguza jinsi lugha mbalimbali zinazounda wingilugha katika Kaunti ya Machakos huhusiana na kuathiri utekelezaji wa maendeleo katika kaunti hiyo. Ili kuchunguza uhusiano na athari za lugha husika katika utekelezaji wa maendeleo, maoni ya Wisbey (2016) ni msingi mkuu kuwa binadamu hutumia lugha tofautitofauti kwa mambo tofautitofauti. Hivyo ili kukadiria jinsi lugha mbalimbali zilivyohusiana na kuathiri utekelezaji wa maendeleo, utafiti huu ulikusanya maoni ya wananchi wa maeneo lengwa yaliyo na wingilugha dhahiri kutumia hojaji. Hojaji hii ilikuwa na sehemu mbili, moja funge na nyingine nusu funge. Sehemu funge ilitumika kukadiria lugha na miseto ya lugha inayotumiwa na misimamo ya watafitiwa kuhusu uhusiano na athari za lugha hizi katika utekelezaji wa maendeleo huku sehemu ya nusu funge ikitumika kupata sababu za majibu yao. Sehemu inayofuata inawasilisha matokeo ya uchanganuzi wa kauli mbalimbali za sehemu hii.

#### 4.4.1 Matumizi ya Lugha Miongoni mwa Viongozi

Lugha wanayotumia au wanazotumia viongozi huwa msingi mkubwa wa utekelezaji wa maendeleo na huathiri uelewa wa wananchi wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Iwapo wananchi wataelewa miradi husika kutoka kupangwa kwake katika hatua ya ushirikishwaji umma hadi utekelezwaji wake, basi maendeleo ya kiwango cha juu yatapatikana. Ni katika msingi huu utafiti huu ulilenga kutathmini lugha wanazotumia viongozi katika muktadha wa maendeleo na matokeo ya uchanganuzi wa data za swali yakawa kama yanavyowasilishwa na kielelezo kifuatacho.

*Kielelezo 4.1 Lugha wanazotumia viongozi kueleza maendeleo*




*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Matokeo haya yanaonyesha kuwa watafitiwa 81 (70.4%) walisema kuwa viongozi wa Kaunti ya Machakos hutumia mseto wa Kiswahili na Kikamba wanapoeleza masuala ya maendeleo huku 27 (23.5%) wakisema kuwa viongozi hutumia mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza. Ni watafitiwa 7 (6.1%) ambao walisema kuwa viongozi wa kaunti hii hutumia msimbo wa Kikamba pekee wanapoeleza masuala ya maendeleo. Uchanganuzi zaidi ulionyesha kuwa kati wale saba waliosema kuwa viongozi hutumia Kikamba pekee, asilimia kubwa walikuwa wa vijiji vya Grogon (28.6%), Katulye (28.6%), Kianzambe (28.6%) na Ndithini (14.3%). Kwa upande mwingine, kati ya waliosema kuwa viongozi hutumia mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza, asilimia kubwa zaidi (51.9%) walikuwa kutoka kijiji cha Mlolongo wakifuatiwa na 14.8% wa Grogon huku ndogo kabisa ikitoka katika kijiji cha Katulye (3.7%). Vilevile, ni

muhimu kutambua kuwa asilimia za vijiji vya Konza (11.1%), Kianzambe (11.1%) na Ndithini (7.4%) ni ndogo pia. Vilevile, kati ya 70.4% waliosema kuwa viongozi hutumia mseto wa Kikamba na Kiswahili, msambao wao unaonyesha kuwa 7.4% walitoka kijiji cha Konza, 43.2% kijiji cha Grogon, 14.8% kijiji cha Mlolongo, 7.4% kijiji cha Katulye, 17.3% kijiji cha Kianzambe na 9.9% kijiji cha Ndithini.

Kwa mujibu wa matokeo haya, ni wazi kuwa viongozi wanapowaelezea wananchi masuala ya maendeleo katika maeneo ya mijini hutumia zaidi mseto wa Kikamba na Kiswahili ikilinganishwa na wanapotumia msimbo wa Kikamba pekee. Ili kuthibitisha ukweli wa matokeo haya mahojiano na maafisa wakuu wa idara lengwa yalionyesha ukweli katika kauli zao.

> Afisa Mkuu Idara ya Utamaduni: *Katika maeneo ya mipakani yaliyo mijini, kutokana na watu wa jamii mbalimbali tunatumia Kiswahili na Kiingereza sana lakini katika maeneo ya vizingasifa vya mashinani, …tunatumia Kikamba na nyakati zingine kuchanganya na Kiswahili.*
>
> Afisa Mkuu Kitengo cha Mimea: *Katika maeneo ya mjini utapata kuna watu wa kila aina na hivyo tunachanganya lugha zote tatu lakini mashinani ambapo Wakamba huwa takriban asilimia 90 tunatumia Kikamba sana na kuchanganya na Kiswahili pale panapohitajika…*
>
> Afisa Mkuu Idara ya Biashara: *Tunapotaka kuwafikia wananchi mijini, sanasana tunatumia lugha rasmi, Kiswahili na Kiingereza lakini mashinani ambako watu wengi wanaongea lugha za mama tunatumia Kikamba zaidi…*
>
> Afisa Mkuu Idara ya nyumba na Ukuaji wa Miji: *Nianze kwa kusema kuwa mimi si Mkamba. Katika maeneo ya mashambani lugha inayotumiwa sana ni Kikamba lakini wakati ninapozungumza na wananchi ninatumia Kiswahili zaidi na kuchanganya na Kiingereza pale ambapo kuna maneno maalumu. …Tukija mijini, mimi ninatumia Kiingereza zaidi na kuchanganya na Kiswahili katika utekelezaji wa miradi ya barabara kwa sababu. (*Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Kauli hizi za maafisa hawa zinathibitisha matumizi ya lugha za Kiswahili, Kikamba na Kiingereza miongoni mwa viongozi kama walivyosema watafitiwa kutoka kila kijiji. Matokeo haya yanawekewa msingi imara na mhimili wa Wingilugha na Maendeleo wa Kiunzi cha Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi unaopendekeza matumizi ya fomyula ya lugha tatu, ambazo katika muktadha huu ni Kiingereza, Kiswahili na Kikamba, katika wingilugha ili kuhakikisha maendeleo. Vilevile, kiunzi hiki kupitia kwa mhimili wake wa Nafasi ya Lugha katika Mifumo ya Ubunifu ya Kitaifa unaosema kuwa kuna usambamba wa mawazo kati ya serikali na mawazo yake ya ubunifu unathibitisha matokeo haya. Katika mhimili wa wingilugha na maendeleo, lugha ya Kikamba inachukua nafasi ya lugha asili, Kiswahili kuchukua nafasi ya lingua franka ya kitaifa na lugha ya Kiingereza kuchukua nafasi ya lugha ya kimataifa. Matokeo haya yanahakikisha usawa na ushirikishwaji wa kila mwananchi katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo hali inayokubaliana na matokeo ya Chhaya (2017) kuwa maendeleo si tu upunguzaji wa umaskini bali pia kuwapa watu nafasi sawa za kushiriki katika mchakato wa maendeleo.

Mhimili wa nafasi ya lugha katika mifumo ya ubunifu ya kitaifa nao unashikilia kuwa utambulisho na umoja wa kitaifa ni muhimu katika kuanzisha na kuendeleza ubunifu na maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Katika muktadha huu, lugha ya Kikamba inatumika sana katika utambulisho wa Kaunti ya Machakos jambo linalohakikisha kuwa maendeleo yanatekelezwa kwa usahihi zaidi katika maeneo ya mashinani. Matokeo haya yanalingana na yale ya utafiti wa Mwangi (2016) kuwa katika Narok Kaskazini, lugha ya Kimaasai imepewa hadhi kubwa katika shughuli za kitamaduni na kijamii kwa sababu lugha ya Kikamba inatumika katika kuhakikisha usawa miongoni mwa wananchi ili kushiriki

katika mchakato wa utekelezaji maendeleo hasa katika maeneo ya mashinani. Kauli ya Afisa Mkuu Idara ya Nyumba na Ukuaji wa Miji inadhihirisha zaidi utambulisho huu kwa sababu kulingana naye, lugha ya Kikamba huwapa maafisa Wakamba nafasi kueleza masuala ya maendeleo ili yaeleweke zaidi. Vilevile, kauli yake kuhusu lugha ya Kikamba katika eneo hili inalandana na mhimili huu kwa kiwango kikubwa kuwa:


> *Katika eneo hili na hasa maeneo ya mashinani, kumekuwa na miradi ambayo imekataliwa na wananchi lakini walipoelezewa kwa Kikamba wakaelewa kabisa, kuikubali na hata kushiriki katika miradi hiyo jambo ambalo lugha za Kiingereza na Kiswahili zilishindwa kufanya.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Mwingiliano huu wa matokeo ya matumizi ya lugha miongoni mwa viongozi na nadharia hii ya utafiti yanathibitisha uhalali na ukweli wa hali halisi katika Kaunti ya Machakos.

### 4.4.2 Lugha Pendwa za Wananchi za Kuelezea Masuala ya Maendeleo

Ili kukadiria uhusiano na athari za misimbo na miseto mbalimbali ya lugha katika utekelezaji wa maendeleo, swali hili liliulizwa ili kusaidia kujua wananchi walipendelea lugha gani kutumiwa na viongozi na washikau wengine wa kimaendeleo katika kuwaelezea masuala ya maendeleo. Matokeo ya data zao yanaonyeshwa na kielelezo hapa chini.

*Kielelezo 4.2 Lugha pendwa za wananchi za kuelezea maendeleo*




*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Kielelezo hiki kinaonyesha kuwa kati ya watafitiwa 115, 24.3% yao wanaelewa masuala ya maendeleo vizuri Kikamba kinapotumia, 16.5% Kiswahili kinapotumiwa, 7.0% Kiingereza kinapotumiwa na 5.2% lugha nyingine zinapotumiwa. Vilevile, 21.7% wanaelewa maendeleo mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza unapotumiwa, 17.4% mseto wa Kiswahili na Kikamba unapotumiwa, 7.0% mseto wa Kiswahili na Kiingereza unapotumiwa na 0.9% mseto wa Kikamba na Kiingereza unapotumiwa. Uchanganuzi zaidi kwa kuzingatia kiwango cha elimu unaonyesha kuwa wengi wa waliosoma hadi kiwango cha vyuo vya kati na vikuu walipendelea lugha za Kiswahili na Kiingereza ikilinganishwa na lugha za mama. Jedwali lifuatalo linawasilisha matokeo ya uchanganuzi wa lugha waliyoipenda watafitiwa kwa mujibu wa viwango vyao vya elimu.

*Jedwali 4.14 Lugha pendwa kwa mujibu wa viwango vya elimu*

| | | | | | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kik | Kisw | Kiing | L.N | Kis+ Kik+ Kiing | Kisw + Kik | Kisw+ Kiing | Kik+K iing | |
| Sijawahi Kusoma | Mdafao | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 |
| | Asilimia | 40.0 % | 40.0 % | 0.0% | 20.0 % | 0.0% | 0.0% | 0.0% | 0.0% | 100.0% |
| Darasa la 8 | Mdafao | 14 | 6 | 0 | 4 | 0 | 9 | 0 | 0 | 33 |
| | Asilimia | 42.4 % | 18.2 % | 0.0% | 12.1 % | 0.0% | 27.3 % | 0.0% | 0.0% | 100.0% |
| Kidato cha nne | Mdafao | 11 | 10 | 2 | 0 | 10 | 10 | 0 | 1 | 44 |
| | Asilimia | 25.0 % | 22.7 % | 4.5% | 0.0% | 22.7% | 22.7 % | 0.0% | 2.3% | 100.0% |
| Chuo cha Kati/ Kikuu | Mdafao | 1 | 1 | 6 | 1 | 15 | 1 | 8 | 0 | 33 |
| | Asilimia | 3.0% | 3.0% | 18.2% | 3.0% | 45.5% | 3.0% | 24.2% | 0.0% | 100.0% |
| **Jumla** | **Mdafao** | **28** | **19** | **8** | **6** | **25** | **20** | **8** | **1** | **115** |
| | **Asilimia** | **24.3 %** | **16.5 %** | **7.0%** | **5.2%** | **21.7%** | **17.4 %** | **7.0%** | **0.9%** | **100.0 %** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Kwa mujibu wa matokeo haya, kiwango cha elimu ni nduni muhimu katika uamuzi wa lugha ya kutumia katika utekelezaji wa maendeleo. Kati ya wale ambao hawajawahi kusoma, jedwali hili linaonyesha kuwa 40.0% yao wanaelewa zaidi msimbo wa Kikamba unapotumika, 40.0% Kiswahili kinapotumika huku 20.0% wakielewa zaidi lugha nyingine zinapotumika. Miongoni mwa waliosoma hadi darasa la nane katika mfumo wa 8-4-4 au waliofika darasa la saba katika mfumo wa 7-4-2-3, asilimia kubwa zaidi (42.4%) wanaelewa zaidi Kikamba kinapotumika, huku 18.2% wakielewa zaidi Kiswahili kinapotumika na 12.1% lugha nyingine zinapotumika. Asilimia 27.3 nao wanaelewa masuala ya maendeleo mseto wa Kiswahili na Kikamba unapotumika. Miongoni mwa waliosoma hadi kidato cha nne, 25.0% wanaelewa masuala ya maendeleo msimbo wa Kikamba unapotumika, 22.7% msimbo wa

Kiswahili unapotumika, 4.5% msimbo wa Kiingereza unapotumika, 22.7% mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza unapotumika, 22.7% mseto wa Kiswahili na Kiingereza unapotumika na 2.3% mseto wa Kikamba na Kiingereza unapotumika. Kama ilivyo katika takwimu hizi, tofauti kati ya viwango vya awali na hiki cha kidato nne zinajitokeza kwa sababu umaarufu wa lugha ya Kiingereza umeongezeka.

Miongoni mwa wale waliosoma hadi vyuo vya kati na vikuu, tofauti zaidi zinajitokeza kwa kuwa umaarufu wa lugha za Kikamba, Kiswahili na lugha nyingine unapungua zaidi huku wa lugha ya Kiingereza na miseto iliyo na Kiingereza ukiendelea kuongezeka. Kwa mujibu wa matokeo yanayoonyeshwa katika jedwali hili, kiwango sawa cha 3.0% katika matumizi ya lugha za Kikamba, Kiswahili na lugha nyingine kinajitokeza. Umaarufu wa Kiingereza unaongezeka ikilinganishwa na viwango vya awali kwa sababu 18.2% yao wanaelewa masuala ya maendeleo kinapotumika. 45.5% nao wanaelewa maendeleo zaidi pale mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza unapotumiwa, huku 3.1% wakielewa zaidi masuala ya maendeleo mseto wa Kiswahili na Kikamba unapotumika. 24.2% nao wanaelewa mseto wa Kiswahili na Kiingereza unapotumika. Hivyo, lugha za Kikamba na Kiswahili zinaathiri kwa njia chanya mchakato wa utekelezaji wa maendeleo pale maendeleo yanapohusisha watu wa viwango vya wale ambao hawajawahi kusoma na waliofika darasa la nane huku matumizi ya lugha ya Kiingereza na miseto yenye Kiingereza ikiathiri utekelezaji wa maendeleo kwa njia hasi. Katika muktadha wa kilimo, kauli ya Afisa Mkuu wa Kitengo cha Mimea alitomelea matokeo haya kwa kusema kuwa:

> *Tumebahatika sana kuwa na wakulima ambao wameenda shuleni na kufikia aghalau kidato cha nne au darasa la nane. Katika maeneo ya mjini na yanayokaribiana na ya mjini, tunachanganya lugha za Kikamba, Kiswahili na Kiingereza na wakulima wote wanaelewa* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Matokea haya yanakubaliana na matokeo ya utafiti wa Wamalwa na wenzake (2019) ya matumizi mapana ya lugha za Kiingereza ikilinganishwa na Kiswahili na Kiluo katika mawanda ya shuleni ambayo ni rasmi hali iliyochangiwa na kiwango chao cha juu cha elimu. Pale ambapo maendeleo yanahusisha watu wa viwango vya kidato cha nne na vyuo, lugha ya Kiingereza nayo inaathiri maendeleo kwa njia chanya ikilinganishwa na lugha za Kikamba, Kiswahili na lugha nyingine. Matokeo ya mahojiano na Afisa Mkuu wa Kitengo cha Mimea yanathibistisha ukweli huu:

> *Huko Mashinani unaweza kwenda na kwa sababu wewe unashughulika na masuala maalumu uzungumze kwa Kiingereza lakini mwisho wa siku utapata kwamba asilimia ndogo kabisa ndio walielewa ulichokuwa ukisema kwa sababu ya kikwazo cha kilugha* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Matokeo haya yanaonyesha kuwa japo wataalamu wa masuala ya maendeleo, viongozi na washidau wengine wa maendeleo wanaweza kuwa na umilisi mkubwa wa lugha maalumu, utekelezaji wa lugha huhitaji kuelewa lugha inayopendwa na inayoeleweka vizuri na walengwa wa maendeleo maalumu ili kuhakikisha kuwa kila mlengwa ameshiriki katika utekelezaji wa maendeleo husika. Hata hivyo, uchanganuzi huu na ule wa sehemu ya 4.4.1 ya matumizi ya lugha miongoni mwa viongozi unaonyesha kuwa matumizi haya ya lugha miongoni mwao na lugha wanazopenda wananchi yanashabihiana. Kutokana na haya, matokeo yanaonyesha kuwa kwa jumla wingilugha una athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo. Vilevile, matokeo haya yanathibitishwa na mhimili wa nafasi ya lugha katika mifumo ya ubunifu ya kitaifa wa Kiunzi cha

Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi unaosisitiza kwamba utambulisho na umoja wa kitaifa ni muhimu katika kuanzisha na kuendeleza ubunifu na maendeleo ya kijamii na kiuchumi, utambulisho unaoletwa na lugha. Vilevile, kwa mujibu wa matokeo haya, wananchi wa Kaunti ya Machakos wanapendelea matumizi ya lugha za Kiswahili, Kikamba na Kiingereza katika utekelezaji wa maendeleo, katika miktadha tofautitofauti, kama ulivyo mhimili wa wingilugha na maendeleo wa kiunzi hiki.

### 4.4.3 Lugha Pendwa katika Usomaji wa Nyaraka za Maendeleo

Katika mchakato wa utelezaji wa maendeleo, utafiti huu ulitambua nafasi muhimu ya nyaraka kwa sababu hutumika zaidi katika kutoa maelekezo ya utekelezaji wa maendeleo mbalimbali. Ili kukadiria mahusiano na athari za lugha mbalimbali katika nyaraka za maendeleo, kauli hii iliulizwa ambapo watafitiwa walitakiwa kuonyesha lugha wanayopenda au wanazopenda katika kusoma nyaraka za maendeleo. Jedwali lifuatalo linawasilisha matokeo ya uchanganuzi wa majibu ya watafitiwa kuhusu kauli hii.

***Jedwali 4.15 Miitiko ya watafitiwa***

| | **Mdafao** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Kikamba | 7 | 6.1 |
| Kiswahili | 31 | 27.0 |
| Kiingereza | 60 | 52.2 |
| Kiswahili+Kikamba+Kiingereza | 4 | 3.5 |
| Kiswahili+Kikamba | 1 | 0.9 |
| Kiswahili+Kiingereza | 9 | 7.8 |
| **Jumla** | **112** | **97.4** |
| Ambao Hawakujaza | 3 | 2.6 |
| **Jumla** | **115** | **100.0** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Matokeo haya yanaonyesha kuwa watafitiwa 7 (6.1%) wanapenda kusoma nyaraka zilizoandikwa kwa Kikamba, 31 (27.0%) wanapenda kusoma zilizoandikwa kwa Kiswahili, 60 (52.2%) wanapenda kusoma zilizoandikwa

kwa Kiingereza, 4 (3.5%) wanapenda kusoma zilizotafsiriwa katika Kiswahili, Kikamba na Kiingereza, 1 (0.9%) anapenda kusoma zilizotafsiriwa katika Kiswahili na Kikamba, huku 9 (7.8%) wakipenda kusoma zilizotafsiriwa kwa Kiswahili na Kiingereza. Hata hivyo, 3 (2.6%) hawakujibu swali hili ambapo uchanganuzi zaidi ulionyesha kuwa asilimia hii ilihusisha watu wa umri wa wazee ambao hawajawahi kusoma. Ijapokuwa wale ambao hawajawahi kusoma walikuwa 5, mtafiti pamoja na wasaidizi waliwasaidia watano hawa katika kujaza hojaji. Hata hivyo, katika kuwasaidia walihakikisha kuwa waliwasomea kauli hizi na kuwapa nafasi za kutoa majibu yao pasipo na kuwashawishi au kuwaelekeza kwa jibu maalumu. Wawili kati ya watano hawa walichagua lugha wanayopenda kutumia kusoma nyaraka lakini watatu walidinda kabisa kujibu na kushikilia msimamo kuwa hawajui kusoma.

Kutokana na matokeo haya, ni wazi kuwa lugha inayopendelewa zaidi katika maandishi ni Kiingereza huku ile isiyopendelewa sana ikiwa ni Kikamba. Hii ina maana kuwa matumizi ya lugha ya Kiingereza katika nyaraka za maendeleo yatafanya utekelezaji wa maendeleo kuwa bora zaidi na hivyo kuleta athari chanya katika utekelezaji wa maendeleo. Kwa upande mwingine, matumizi mapana ya lugha ya Kikamba katika maandishi na nyaraka yataathiri maendeleo kwa njia hasi kwa kuwa matokeo haya yanaonyesha uhusiano mbaya kati ya lugha hii na utekelezaji wa maendeleo kupitia kwa nyaraka. Umaarufu huu wa nyaraka zilizoandikwa kwa lugha ya Kiingereza sio tu miongoni mwa wananchi bali pia miongoni mwa waundaji sera katika idara nne zilizohusishwa katika utafiti huu. Maafisa wanne walioshirikishwa katika utafiti huu kwa njia ya mahojiano walikiri kupenda kuandika na kusoma nyaraka za maendeleo kwa

lugha ya Kiingereza kwa sababu kwao ni rahisi kusoma na kuielewa ikilinganishwa na lugha za Kikamba, Kiswahili na lugha nyingine za mama.

> Afisa Mkuu, Idara ya Utamaduni: …*tunatumia Kiingereza sana hasa katika nyaraka na mawasiliano rasmi…*
>
> Afisa Mkuu, Kitengo cha Mimea: …*katika maandishi ni Kiingereza pekee kinachotumiwa…*
>
> Afisa Mkuu, Idara ya Biashara: *Mara nyingi (lugha ya nyaraka) huwa ni lugha ya Kiingereza na chache kwa lugha za Kiswahili na Kikamba.*
>
> Afisa Mkuu, Idara ya Nyumba na Ukuaji wa Miji: *Iwapo kuna ujumbe kama huu, unakuwa umeandikwa kwa lugha ya Kiingereza…* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Katika kufafanua hali hii lugha ya Kiingereza Afisa Mkuu wa Kitengo cha Mimea alisema kuwa:

> *Ni lugha ambayo nimeisoma zaidi katika masomo mengi shuleni ikilinganishwa na nyingine, ni lugha ambayo msamiati wake ni rahisi kueleweka ikilinganishwa na Kiswahili na lugha za mama na kwamba ni lugha inayoeleweka kwa urahisi na watu wengi. Zilizotafsiriwa kwa lugha mbalimbali huwa ni njia nzuri ya kuelewa mambo yaliyoandikwa kwa ufasaha zaidi kwa sababu yale ambayo hayaeleweki vizuri kwa lugha moja yataeleweka katika lugha badala.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Kauli hii inaonyesha umuhimu wa tafsiri katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo. Ili kufafanua nafasi ya tafsiri Afisa Mkuu, Idara ya Utamaduni alifafanua kuwa:

> *Kwa upande wa tafsiri, tunatafsiri nyaraka wenyewe na hasa katika hatua ya ushirikishaji umma katika mchakato wa maendeleo ambapo iwapo ni nyaraka rasmi ya serikali ya kitaifa au kaunti, huwa imeandikwa kwa Kiingereza na hivyo tunawasomea tukitafsiri kwa sababu hatuna wataalamu wa kutafsiri na pale palipo na haja kuu tunakodi huduma za tafsiri kutoka kwa wataalamu. Vilevile, tunatumia vyombo vya habari, hasa mno vile vya Kikamba, kutafsiri ujumbe huu kwa wananchi.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Afisa Mkuu, Idara ya Nyumba na Ukuaji wa Miji naye alifafanua kuwa:

> *Tafsiri itahusisha tu pale kuliko na ujumbe maalumu kutoka kwa serikali na tunajitafsiria wenyewe wakati tunapozungumza na wananchi. Hata hivyo, ukalimani ndio unatumika sana katika kutekeleza maendele...* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Kauli hizi zinaonyesha nafasi muhimu ya tafsiri na ukalimani katika kuhakikisha kuwa utekelezaji wa maendeleo unafanikiwa. Japo jitihada hizi ni muhimu katika utekelezaji wa maendeleo, ni hatua ambayo ni hatari kwa sababu wasimamizi hawa sio wataalamu wa tafsiri na ukalimani. Hivyo kutokana na ukosefu wa stadi za tafsiri, upo uwezekano mkubwa wa kupitisha ujumbe ambao sio wa kweli jambo ambalo litaathiri utekelezaji wa maendeleo kwa njia hasi.

Mbinu ya uhakiki wa nyaraka ilitumika kwa kina zaidi katika hatua hii ili kutambua jinsi nyaraka za maendeleo zilivyotumia lugha. Katika hatua ya ukusanyaji data, nyaraka 23 zilikusanywa kutoka kwa watafitiwa. Uchanganuzi wa nyaraka hizi ulionyesha kuwa zote (100%) zilikuwa za Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Kati ya hizi 23, 18 (78.3%) zilikuwa zimeandikwa kwa Kiingereza, 3 (13%) kwa Kiswahili na 2 (8.7%) kwa tafsiri ya Kiingereza na Kiswahili. Uhakiki huu wa nyaraka unonyesha ukweli wa matokeo ya uchanganuzi wa data kutoka kwa wananchi. Matokeo ya utafiti huu yanalingana na matokeo ya utafiti wa Rassool na wenzake (2006) kuhusu matumizi ya lugha ya kimataifa na lingua franka ya kitaifa katika nyaraka ambapo utafiti wao ulionyesha kuwa nchini Afrika Kusini, 50% ya nyaraka katika mazingira ya shuleni ziliandikwa kwa Kiingereza na 50% nyingine kwa lugha ya Kiafrikana. Sawa na utafiti wao, utafiti huu unathibitisha matumizi ya lugha za Kiingereza, ambayo ni lugha ya kimataifa nchini Kenya, na Kiswahili, ambayo ni lingua franka. Hata hivyo, matokeo ya tafiti hizi mbili yanatofautiana katika asilimia kwa sababu katika utafiti wao uwiano wa asilimia

katika ya nyaraka za Kiingereza na Kiafrikana ni 50%:50% lakini katika utafiti huu uwiano wa zile za Kiingereza kwa Kiswahili ni 78.3%:21.7%. Zaidi ni kuwa katika utafiti huu, kati ya 21.7% zilizokuwa za Kiswahili, 3 (13% ya jumla ya nyaraka zote) ndizo za Kiswahili pekee huku 2 (8.7%) zikiwa tafsiri ya Kiingereza na Kiswahili. Katika matokeo yao hakuna zozote zilizokuwa na tafsiri ya lugha tofauti.


Hata hivyo, kutokuwepo kwa nyaraka za Kikamba au tafsiri ya Kikamba, ambayo ndiyo lugha asili kunakinzana na mhimili wa Lugha na Maendeleo ya Binadamu wa Kiunzi cha Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi unaoshinikiza kuwa mafunzo kwa lugha ya kwanza huchangia katika maendelezo ya vigezo vya kijamii, kitamaduni na kimaendeleo katika jamii. Katika mahojiano na Afisa Mkuu, Idara ya Biashara aliyekiri kuwa lugha ya Kikamba ni ngumu kutokana na kuwa na vokali nyingi kuliko Kiswahili na Kiingereza na kuwa watu wengi hawawezi kuandika kwa Kikamba, utafiti huu uligundua kuwa kutokuwepo kwa nyaraka za Kikamba ulitokana na ukosefu wa wafasiri wa Kikamba na pia lugha ya Kikamba kukosa istilahi mwafaka. Hata hivyo, kwa sababu kuna wale wanaopendelea lugha ya Kikamba katika kusoma, ni muhimu nyaraka hizi pia zitafsiriwe katika Kikamba ili kuhakikisha kwamba maendeleo haya yanawafikia wananchi wote. Hatua hii italeta athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo katika kaunti hii.

### 4.4.4 Idadi ya Lugha Wanazozungumza Watafitiwa

Kauli hii ilitumika katika utafiti huu ili kukadiria idadi ya lugha ambazo watafitiwa na wananchi kwa jumla wa maeneo lengwa huzungumza. Ukadiriaji huu ulikuwa wa umuhimu mkubwa kwa sababu kauli iliyofuata ilikadiri jinsi idadi husika ya lugha iliwasaidia wananchi kufanya na kupata maendeleo.

Kielelezo kifuatacho kinawasilisha matokeo ya uchanganuzi wa majibu ya kauli hii.

***Kielelezo 4.3 Idadi ya lugha watafitiwa wanoyoelewa na kuzungumza***





*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Kwa mujibu wa kielelezo hiki, watafitiwa 2 (1.7%) walikuwa na uwezo wa kuelewa na kuzungumza lugha moja tu, 9 (7.8%) walielewa na kuzungumza lugha mbili, 71 (61.7%) walielewa na kuzungumza lugha tatu na 33 (28.7%) walielewa na kuzungumza lugha zaidi ya tatu. Matokeo haya yanaonyesha uthabiti wa wingilugha katika Kaunti ya Machakos kwa kuwa jumla ya 98.3% wana uwezo wa kuelewa na kuzungumza lugha zaidi ya moja. Katika mahojiano na Afisa Mkuu wa Kitengo cha Mimea matokeo haya yalithibitishwa na kauli ifuatayo:

> *...tunachanganya lugha za Kikamba, Kiswahili na Kiingereza na wakulima wote wanaelewa* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Kauli iliyofuata ilikadiria namna uelewa wa idadi husika ya lugha ulivyowasaidia watafitiwa katika kufanya na kupata maendeleo na matokeo yake yakawa kama ilivyo katika kielelezo hiki

***Kielelezo 4.4 Manufaa ya uelewa na matumizi wa idadi husika ya lugha katika utekelezaji maendeleo***




*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Uchanganuzi huu wa maoni yao kuhusu manufaa ya uelewa na uwezo wa kuzungumza idadi ya husika lugha nao unaonyesha kuwa asilimia kubwa zaidi (93.9%) ilisaidika sana kimaendeleo ikilinganishwa na 6.1% ambayo ilikiri kusaidika kidogo. Hata hivyo, hakuna mtafitiwa aliyesema kuwa uelewa na uwezo wa kuzungumza idadi husika ya lugha haukusaidia kwa vyovyote katika kupata maendeleo. Katika ufafanuzi wa watafitiwa, uelewa na matumizi ya idadi zaidi ya lugha moja ulisaidia kwa njia zifuatazo: kwa wanabiashara ulisaidia kuongeza kiwango cha mauzo, kwa wanakilimo ulisaidia kupata mafunzo ya kilimo kwa usahihi zaidi kutoka kwa walimu wa kabila lolote na hivyo kuleta

mazao zaidi, kwa wananchi kwa jumla ulisaidia kuelewa sera za maendeleo kwa usahihi kabisa jambo lililosababisha ushiriki wao mkubwa katika mchakato wa maendeleo na kwa wafanyikazi ulisaidia kufanya kazi eneo lolote na kwa mwajiri yeyote. Matokeo haya yanaonyesha nafasi ya wingilugha katika mchakato wa kutekeleza maendeleo kwa sababu husaidia kufanikisha mazungumzo na mawasiliano katika mchakato huu hali inayofanya utekelezaji wa maendeleo kufanikiwa katika Kaunti ya Machakos. Zaidi mchango huu mkubwa wa wingilugha kwa utekelezaji wa maendeleo ulijitokeza kwa uwazi kabisa katika mahojiano ambapo maafisa waliohojiwa walitoa kauli zifuatazo kuhusu manufaa ya wingilugha kwa utekelezaji wa maendeleo;

> Afisa Mkuu, Idara ya Utamaduni: …*matumizi ya lugha hizi (Kiswahili, Kikamba na Kiingereza) yanasaidia sana katika utekelezaji wa maendeleo kwa sababu yanawezesha kufikisha ujumbe wa maendeleo kwa kila mwananchi, awe wa jamii yoyote, kiwango chochote cha elimu, jinsia yoyote, umri wowote na awe anafanya kazi yoyote.*
>
> Afisa Mkuu, Kitengo cha Mimea: *Wingilugha una athari chanya kwa utekelzaji wa maendeleo kwa sababu unaondoa vikwazo vya kimawasiliano na kusaidia wakulima kuelewa mafunzo sawa na kupanua soko ya mazao yao.*
>
> Afisa Mkuu, Idara ya Biashara: *...wingilugha unaathiri utekelezaji wa maendeleo kwa njia nzuri kwa sababu unahakikisha kuwa kila mwananchi ameshirikishwa katika utekelezaji wa maendeleo. Athari hasi itatokea pale tu lugha zinazounda wingilugha zinapotumika kuwabagua watu katika mchakato wa kutekeleza maendeleo.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Matokeo haya yanaonyesha athari za wingilugha katika Kaunti ya Machakos katika utekelezaji wa maendeleo, jambo ambalo ndilo lengo kuu la utafiti huu. Kiunzi cha Kinadharaia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi katika mhimili wa wingilugha na maendeleo kinathibitisha matokeo haya kuwa wingilugha unaathari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo kupitia matumizi ya lugha husika katika majukumu mbalimbali

hasa matumizi ya pendekezo lake la fomyula tatu kama njia ya kuhakikisha maendeleo.

### 4.4.5 Athari za Lugha Mbalimbali kwa Utekelezaji wa Maendeleo.

Ili kutambua uhusiano na athari za lugha mbalimbali katika utekelezaji wa maendeleo katika Kaunti ya Machakos, utafiti huu ulitathmini athari za lugha mbalimbali kwa maendeleo katika vijiji sita husika kwa lengo la kutoa uchanganuzi wa kina. Katika swali la sita na la saba la kiambatisho 1A, watafitiwa walitakiwa kuziorodhesha lugha zinazochangia maendeleo na zile zinazolemaza maendeleo katika vijiji vyao mtawalia. Matokeo yanaonyesha kuwa katika kijiji cha Konza, lugha za Kikamba na Kiswahili zinaboresha utekelezaji wa maendeleo huku lugha nyingine na Kiingereza zikilemaza utekelezaji wa maendeleo. Hali hii ilitokea kuwa sawa katika vijiji vya Katulye, Kianzambe na Ndithini sawa na eneo la Grogon japo kwa kiwango kidogo ikilinganishwa na hivi vingine. Kwa kiasi kikubwa, japo sio kwa asilimia 100, lugha za Kiingereza na lugha nyingine zililemaza utekelezaji wa maendeleo.

Kwa upande mwingine, lugha ya Kikamba na lugha nyingine hulemaza maendeleo katika kijiji cha Mlolongo na Grogon ambavyo ni vijiji vilivyo maeneo ya mjini. Hata hivyo, lugha hizi zililemaza maendeleo katika kijiji cha Mlolongo zaidi ikilinganishwa na kijiji cha Grogon kwa sababu mjini Machakos idadi ya Wakamba ni kubwa na tena makabila yaliyo katika eeno hili ni machache ikilinganishwa na eneo la Mlolongo ambako kuna makabila mengi zaidi kuliko mjini Machakos. Hali hii ilithibitishwa na mahojiano na Mkuu wa Idara ya Nyumba na Ukuaji wa Miji kuwa:

> *…eneo la Mlolongo ambako kuna jamii nyingi ambazo zinaishi huko, ikilinganishwa na mjini Machakos, tunapotekeleza miradi*

> *kama ununuzi wa mashamba, utengenezaji wa barabara na usafishaji kupitia kwa uokotaji takataka, tunatumia lugha kulingana na maeneo hayo maalumu* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Katika maeneo haya ya mjini lugha za Kiswahili na Kiingereza zina athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo ikilinganishwa na lugha nyinginezo. Katika kijiji cha Mlolongo, matokeo yalionyesha kuwa msimbo wa Sheng' una umaarufu katika shughuli za kila siku hasa miongoni mwa vijana kwa kuwa iliorodheshwa kama lugha mojawapo ya zile zinazochangia katika utekelezaji wa maendeleo. Ili kuthibitisha hili, utafiti ulitumia mbinu ya uchunzaji ambapo matokeo yalionyeshwa kuwa katika mazingira ya kazini na biashara hasa za usafiri na uchuuzi, wengi wa vijana walitumia msimbo huu zaidi kuliko lugha za Kiswahili na Kiingereza. Afisa Mkuu, Idara ya Biashara alithibitisha hili zaidi kwa kusema kuwa:

> *Itategemea pia na hadhira yako kwa sababu iwapo unazungumza na wazee mara nyingi wanapenda lugha za mama tofauti na vijana ambao wanapenda lugha za Kiswahili, Kikamba na Sheng' hivyo miongoni mwa wazee lugha za mama zitaleta athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo lakini athari hasi miongoni mwa vijana.*

Hata hivyo, Afisa huyu alisema kuwa:

> *Hatutumii lugha ya Sheng' katika mikutano na shughuli za maendeleo kwa sababu haijatambuliwa kama lugha rasmi au ya taifa na pia haieleweki na watu wote hasa wazee.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Kwa upande wake, Afisa Mkuu, Idara ya Nyumba na Ukuaji wa Miji alikuwa na haya ya kusema kuhusu Sheng'

> *Lugha ya Sheng' katika mazingira ya mjini inatumiwa sana hasa miongoni mwa vijana na wanaipenda sana hasa wale wa mitaani wanaofanya uchuuzi na wanaofanya kazi katika sekta ya usafiri na hivyo miongoni mwao msimbo huu unawasaidia sana katika shughuli zao za kikazi na kila siku.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Katika kauli hizi, maafisa hawa wanatambua nafasi ya Sheng' katika utekelezaji wa maendeleo na maendeleo yenyewe miongoni mwa vijana. Hata hivyo, ni wazi kuwa msimbo wa Sheng' bado haujatambulika kama lugha rasmi ama lugha ya taifa na hivyo hautumiwi katika mchakato wa utekelezaji maendeleo. Kutokana na hali hii, utafiti huu ulifumbua kuwa ijapokuwa msimbo wa Sheng' haujapewa nafasi na serikali kama lugha ya taifa ama rasmi, una nafasi kubwa kuhakikisha utekelezaji bora wa maendeleo miongoni mwa vijana hasa maeneo ya mjini.

Uchanganuzi zaidi katika swali la 8 ya Kiambatisho 1B (Hojaji Nusu-Funge) unaonyesha kuwa katika kijiji cha Konza 77.8% ya watafitiwa wanaelewa masuala ya maendeleo vizuri kabisa lugha ya Kikamba inapotumika, 11.1% wanaelewa kidogo na 11.1% hawaelewi kabisa. Kwa upande wa lugha ya Kiswahili, 88.9% walielewa vizuri kabisa, 11.1% walielewa kidogo na hakuna ambaye hakuelewa kabisa. Kuhusu lugha ya Kiingereza, 55.6% walielewa vizuri sana, 44.4% walielewa kidogo wala hakuna ambaye hakuelewa kabisa. Kwa sababu maeneo ya utafiti huu yalipakana na Wamaasai, Waembu na Wagikuyu, lugha zao pia ziliorodheshwa katika uchanganuzi huu. Katika kijiji cha Konza, ni 22.2% ya watafitiwa wa eneo hili walioelewa Kimaasai vizuri sana, 11.1% walioelewa Kiembu vizuri sana, 11.1% walioelewa Kigikuyu vizuri sana na 11.1% walioelewa lugha nyingine vizuri sana. Katika kijiji cha Grogon, 75.6% ya watafitiwa wa eneo hilo walielewa Kikamba vizuri sana, 17.1% walikielewa kidogo na 4.9% hawakukielewa kabisa. 88.9% walikielewa Kiswahili vizuri sana na 17.1% walikielewa kidogo. Hakuna watafitiwa ambao hawakuelewa kabisa Kiswahili. 61.1% nao walielewa Kiingereza vizuri sana, 44.4% walikielewa kidogo na wala hakukuwa na yeyote ambaye hakuelewa Kiingereza

kabisa. Kuhusu lugha nyingine, ni 4.9% walioelewa Kimaasai, 2.4% walioelewa Kiembu, 7.3% walioelewa Kigikuyu na 12.1% walioelewa lugha nyingine zinapotumiwa kuelezea maendeleo.

Katika kijiji cha Mlolongo, 50% ya watafitiwa wa eneo hilo walielewa Kikamba vizuri kabisa, 30.8% walikielewa kidogo na 19.2% hawakukielewa kabisa. 92.3% nao walielewa maelekezo ya maendeleo vizuri sana Kiswahili kilipotumika, 7.7% walielewa kidogo na hakukuwa na yeyote ambaye hakuelewa kabisa Kiswahili kilipotumika. Kwa upande wa lugha ya Kiingereza, 61.5% walielewa vizuri sana, 30.8% walielewa kidogo na 7.7% hawaelewi kabisa. Ni 7.7%, 7.7%, 15.4%, na 15.4% za watafitiwa wa eneo hili walioelewa maelekezo ya maendeleo lugha za Kimaasai, Kiembu, Kigikuyu na lugha nyingine zilipotumika mtawalia. Katika kijiji cha Katulye, 88.9% walielewa maelekezo ya maendeleo vizuri sana Kikamba kilipotumika, 11.1% walielewa kidogo na wala hakuna ambaye hakuelewa kabisa. Kwa upande wa lugha ya Kiswahili, 88.9% yao walielewa maelekezo kwa Kiswahili vizuri kabisa huku 11.1% wakielewa kidogo. Hakuna ambaye hakuelewa kabisa. 55.6% yao walielewa maelekezo kwa lugha ya Kiingereza vizuri sana, 33.3% walielewa kidogo, huku 11.1% wakiwa hawaelewi kabisa. Kwa upande wa lugha za Kimaasai, Kiembu, Kigikuyu na lugha nyinginezo, ni 0.0%, 11.1%, 11.1% na 22.2% waliozielewa vizuri kabisa. Wengine walizielewa kidogo na wengine hawakuzielewa kabisa.

Katika kijiji cha Kianzambe, 84.2% walielewa maelekezo ya maendeleo vizuri kabisa Kikamba kilipotumika huku 10.5% wakielewa kidogo na 5.3% wakiwa hawaelewi kabisa. Kuhusu Kiswahili, watafitiwa wote (100%) waliewa maelekezo kwa Kiswahili vizuri kabisa. Kwa upande wa lugha ya Kiingereza, ni

52.6% ambao walielewa maelekezo ya maendeleo vizuri kabisa, huku 42.1% wakielewa kidogo na 5.3% wakiwa hawaelewi kabisa. Katika kijiji hiki, ni 5.3%, 0.0%, 21.1% na 5.3% walioelewa maelekezo ya maendeleo lugha za Kimaasai, Kiembu, Kigikuyu a lugha nyingine zilipotumika. Matokeo yalionyesha kuwa katika kijiji cha Ndithini, 81.8% walielewa maelekezo ya maendeleo kwa Kikamba vizuri sana, 9.1% walielewa kidogo na 9.1% hawakuelewa kabisa. Katika uelewa wa maelekezo ya maendeleo kwa Kiswahili, wote (100%) walielewa vizuri kabisa na Kiingereza kilipotumika, 54.5% walielewa vizuri kabisa, 45.5% walielewa kidogo na hakuna ambaye hakuelewa kabisa. Kuhusu uelewa wa lugha za Kimaasai, Kiembu, Kigikuyu na lugha nyinginezo katika maelekezo ya maendeleo, ni 0.0%, 9.1%, 18.2% na 36.4% ambao waliyaelewa maelekezo ya maendeleo vizuri sana.

Kulingana na matokeo haya, kwa jumla uelewa wa lugha ya Kikamba na Kiswahili ni wa viwango vya juu sana katika vijiji vyote sita. Hata hivyo, viwango hivi ni vya chini katika maeneo vizingasifa ya mjini ikilinganishwa na maeneo vizingasifa ya mashinani. Kinyume cha hali hii ni lugha ya Kiingereza ambapo viwango vya uelewa wake ni vya juu katika maeneo vizingasifa ya mjini ikilinganishwa na maeneo vizingasifa ya mashinani. Ni lugha ya Kiswahili tu ambayo viwango vya uelewa katika maeneo yote ni vya juu. Matokeo haya yalithibitishwa na mahojiano na maafisa waliohusishwa kupitia kwa kauli zao kama ifuatavyo:

> Afisa Mkuu, Idara ya Utamaduni: *Katika maeneo ya mipakani yaliyo mijini kutokana na watu wa jamii mbalimbali tunatumia Kiswahili na Kiingereza sana lakini katika maeneo ya vizingasifa vya mashinani, utapata kuwa wengi wa wananchi wanaelewa lugha za jirani zao kwa sababu wameingiliana kwa muda mrefu na wamejifunza lugha za kila jamii na hivyo tunatumia Kikamba na nyakati zingine kuchanganya na Kiswahili.*

> Afisa Mkuu, Kitengo cha Mimea: *Katika maeneo ya mjini utapata kuna watu wa kila aina na hivyo tunachanganya lugha zote tatu lakini mashinani ambapo Wakamba huwa takriban asilimia 90 tunatumia Kikamba sana na kuchanganya na Kiswahili pale panapohitajika.*
>
> Afisa Mkuu, Idara ya Biashara: *Tunapotaka kuwafikia wananchi mijini, sanasana tunatumia lugha rasmi, Kiswahili na Kiingereza lakini mashinani ambako watu wengi wanaongea lugha za mama tunatumia Kikamba. Tunatumia lugha kutegema mazingira na wasikilizaji.*
>
> Afisa Mkuu, Idara ya Nyumba na Ukuaji wa Miji: *Katika maeneo ya mashinani lugha inayotumiwa sana ni Kikamba lakini wakati ninapozungumza na wananchi ninatumia Kiswahili zaidi na kuchanganya na Kiingereza pale ambapo kuna maneno maalumu … Tukija mijini, mimi ninatumia Kiswahili zaidi na kuchanganya na Kiswahili katika utekelezaji wa miradi.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Matokeo haya yanaonyesha uwiano mkubwa kati ya data za hojaji kutoka kwa watafitiwa wa vijiji lengwa na maoni ya wasimamizi wa idara husika ambazo zina uhusiano wa karibu sana na utekelezaji wa maendeleo. Ijapokuwa viwango vya uelewa wa Kingereza katika maeneo haya ni vya wastani, matumizi yake katika utekelezaji wa maendeleo sio mkubwa sana. Uchunguzi zaidi kwa njia ya uchunzaji ulionyesha kuwa wananchi katika vijiji hivi hawakutumia lugha ya Kiingereza katika shughuli zao katika mawanda mbalimbali.

Hali hii ni tofauti kabisa katika vijiji vilivyo mjini kwa kuwa maafisa waliohojiwa walionyesha kuwa iwapo lugha ya Kikamba itatumika kikamilifu, basi utekelezaji wa maendeleo utaathiriwa kabisa kwa njia hasi kwa sababu kuna watu wengi ambao si Wakamba wanaoishi katika maeneo haya. Kwa mfano, Afisa Mkuu katika Kitengo cha Biashara alisema kuwa:

> *Kwa upande mwingine, lugha ya Kiswahili ndiyo huwaunganisha watu wa makabila tofautitofauti katika maneneo ya mashinani na hata mijini na huwa na athari chanya hasa pale ambapo watu wanazungumza lugha tofautitofauti.*

Aliendelea kueleza kwa kusema kuwa:

> *Itategemea pia na hadhira yako kwa sababu iwapo unazungumza na wazee mara nyingi wanapenda lugha za mama tofauti na vijana ambao wanapenda lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng' hivyo miongoni mwa wazee lugha za mama zitaleta athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo lakini athari hasi miongoni mwa vijana. Kwa upande wa vijana lugha za mama zitakuwa na athari hasi ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng' ambazo zitaleta athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Kauli hizi zinaonyesha namna lugha mbalimbali zinazounda wingilugha zinavyoathiri utekelezaji wa maendeleo katika Kaunti ya Machakos katika maeneo vizingasifa ya mjini na yale ya mashinani. Matokeo haya yanalingana sana na matokeo ya utafiti wa Chhaya (2017) hasa kuhusu lugha asili kuwa zina nafasi kubwa katika maendeleo ya watu wa eneo lolote kwa sababu katika utafiti huu, lugha ya Kikamba ambayo ndiyo lugha asili ina nafasi kubwa zaidi katika utekelezaji wa maendeleo katika maeneo ya mashinani. Matokeo haya vilevile yanakubaliana na matokeo ya utafiti wa Saidi (2021) kuwa lugha ya Kiswahili ni nguzo kuu ya maendeleo ya mashambani kwa sababu matokeo haya yameonyesha jinsi lugha ya Kiswahili inavyofanya kazi muhimu katika maeneo yenye wingilugha katika kuhakikisha usawa na ushirikishaji wa wananchi wote katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo kama anavyosema Chayya (2017).

Kwa msingi wa kinadharia, matokeo haya yanaafiki misingi na mihimili ya Kiunzi cha Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi. Ithibati ya uwiano huu ni kuwa matokeo haya yanaonyesha jinsi matumizi ya fomyula ya lugha tatu, yaani lugha ya kimataifa, lingua franka ya kitaifa na lugha asili, inayopendekezwa na kiunzi hiki, yanavyofanya kazi katika muktadha wa Kaunti ya Machakos katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo. Vilevile,

matokeo haya yanathibitisha kuwa lugha za Kikamba, Kiswahili na Kiingereza ni muhimu katika mfumo wa ubunifu wa serikali ya Kaunti ya Machakos kama ulivyo mhimili wa kiunzi hiki cha kinadharia. Hivyo lugha zinazounda wingilugha zina athari chanya na hasi kwa utekelezaji wa maendeleo katika Kaunti ya Machakos kutegemea eneo zinamotumiwa na sifa za hadhira maalumu.

### 4.5 Nafasi ya Mielekeo katika Uteuzi wa Lugha.

Mielekeo ya lugha huwa ni jambo ambalo haliwezi kuepukika katika mazingira ya wingilugha. Suala hili la mielekeo katika uteuzi wa lugha katika mazingira ya wingilugha linaungwa mkono na Sridhar (1996) ambaye anaorodhesha mielekeo kama mojowapo ya viukulio vya uteuzi lugha. Zaidi ni maoni ya Kavoi (2019) kuwa mielekeo ya lugha huwa ni jambo la lazima katika mazingira ya uteuzi huru wa lugha. Ni katika msingi huu ambapo sehemu hii ilichanganua data zilizokusanywa kwa madhumuni ya kutambua nafasi ya mieleko katika uteuzi wa lugha ya kuundia na kusambaza sera za maendeleo miongoni mwa maafisa wa idara nne lengwa na wananchi wenyewe. Miongoni mwa watafitiwa katika vijiji lengwa vya utafiti huu, watafitiwa walitakiwa kutoa hisia zao kuhusu kauli tano kutumia kiunzi cha likati. Matokeo ya miitiko yao kwa kauli husika yanawasilishwa katika sehemu ifuatayo:

#### 4.5.1 Lugha ya Kwanza ni Bora Kuleta Maendeleo katika Nyaraka za Maendeleo

Kauli hii ililenga kutathmini mielekeo yao kuhusu matumizi ya lugha ya kwanza katika nyaraka za maendeleo. Miitiko ya watafitiwa kuhusu kauli hii ni kama ifuatavyo:

*Jedwali 4.16 Miitiko ya watafitiwa*

| | **Mdafao** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| SK | 32 | 27.8 |
| S | 40 | 34.8 |
| SH | 21 | 18.3 |
| N | 20 | 17.4 |
| NK | 2 | 1.7 |
| **JUMLA** | **115** | **100.0** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Matokeo haya yanaonyeshwa kuwa 27.8% hawakukubali kabisa na 34.8% hawakukubali. Hivyo, kwa mujibu wa takwimu hizi, jumla ya 62.6% walikuwa mielekeo hasi kuhusu kutumika kwa lugha ya Kikamba katika nyaraka za maendeleo. 18.3% nao hawakuwa na hakika na kauli hii. Kwa upande mwingine, ni 17.4% ambao walikubali huku 1.7% wakikubali kabisa. Kwa jumla ni 19.1% pekee walioegemea upande wa kukubali kuwa lugha ya kwanza ndiyo bora kutumika katika nyaraka za maendeleo. Uchanganuzi zaidi ulionyeshwa kuwa miongoni mwa waliokuwa na mielekeo hasi, asilimia kubwa zaidi (SK-59.4% na S-52.5%) walikuwa wa umri wa miaka 18-35 na umri wa miaka 36-45 mtawalia na kati ya wale waliokuwa na mielekeo chanya, wengi walikuwa wa miaka zaidi ya 46 (NK – 100% na N – 55.0%). Matokeo haya yanaonyesha kuwa umri wa watafitiwa wa kati ya miaka 18-35 wana mielekeo hasi kwa maandishi na nyaraka katika lugha za kwanza ikilinganishwa na wazee ambao mielekeo yao ni chanya kuhusu nyaraka katika lugha ya kwanza.

Kwa kuzingatia nduni ya kiwango cha elimu, kati ya waliokosa kukubali kabisa, waliosoma hadi vyuo vikuu na vya kati walikuwa 46.9%, waliosoma hadi kidato cha nne 31.2%, na waliosoma hadi darasa la nane 21.9%. Hakuna yeyote ambaye hajawahi kusoma alikosa kukubaliana na kauli hii. Waliokubalina kabisa (NK) wote (100%) walikuwa miongoni mwa wale ambao hawajawahi

kusoma na miongoni mwa wale waliokubali (N), asilimia kubwa (50%) ilihusisha wale ambao walisoma hadi darasa la nane. Matokeo haya yanaonyesha kuwa kuna mielekeo hasi kuhusu nyaraka zilizoandikwa kwa lugha ya kwanza miongoni mwa watu ambao wamesoma hadi kidato cha nne na vyuo na chanya miongoni mwa wale ambao hawajawahi kusoma na ambao wamesoma hadi darasa la nane. Kwa kuzingatia kigezo cha jinsia, miongoni mwa wale ambao hawakukubali kabisa (SK), 53.1% walikuwa wa jinsia ya kike na 46.9% walikuwa wa kiume. Miongoni mwa wale ambao hawakukubali (S) 50% walikuwa wa kike na 50% wa kiume. Miongoni mwa wale ambao hawakuwa na hakika (SH) 42.9% walikuwa wa kike na 57.1% walikuwa wa kiume. Tunapoangazia upande wa waliokubali (N) 55.0% walikuwa wanawake huku 45.0% wakiwa wanaume. Waliokubali kabisa walikuwa 2 na wote (100%) walikuwa wa jinsia ya kike. Matokeo haya yanaonyesha kuwa jinsia ya kike inatawala pande zote mbili za waliokubali na waliokosa kukubali huku wengi wa wanaume wakiwa hawana hakika na kauli.

Kwa kuzingatia nduni ya kazi wanayoifanya, wengi wa wale ambao hawakukubali kabisa (SK) walikuwa wanaofanya kazi ya biashara (34.4%) na wanaofanya kazi ofisini (25.0%) na miongoni mwa wale waliokataa kukubali (S) wengi walikuwa wanaofanya biashara (40.0%) na wanaofanya kazi sehemu nyingine (25.0%). Kwa upande wa waliokubali (N), asilimia kubwa zaidi (30.0%) ilikuwa ni wale wanaofanya kazi nyumbani ikifuatiwa na wale wanaofanya kazi shambani (25%). Miongoni mwa wale waliokubali kabisa (NK) asilimia kubwa zaidi (50%) ilikuwa ya wale wanaofanya kazi nyumbani. Matokeo haya yanaonyeshwa kuwa wale ambao wanafanya kazi ya biashara na ofisini wana mielekeo hasi kuhusu nyaraka zilizoandikwa kwa lugha ya mama

na kuwa wale wanaofanya kazi katika mazingira ya nyumbani wana mielekeo chanya kuzihusu.

Kwa upande wa mahojiano, wahojiwa wote wanne, walisema kuwa wao huandika nyaraka zote kwa lugha ya Kiingereza kwa sababu ni lugha rahisi ikilinganishwa na lugha za Kiswahili na Kikamba. Hawakukubali kabisa kuwa lugha ya Kikamba ndio bora katika maendeleo kwa kusema kuwa kuandika msamiati wa Kikamba ni vigumu sana. Kwa kuzingatia sifa za wahojiwa hawa, wote walikuwa wamesoma hadi vyuo vikuu hali ambayo inajaliza matokeo ya hojaji kwa wakaazi wa vijiji vilivyohusishwa katika utafiti huu. Baadhi ya kauli zao kuhusu nyaraka kwa lugha ya Kikamba zinawasilishwa hapa:

> Afisa Mkuu, Idara ya Biashara: *Ni ukweli kuwa sio watu wengi wanaoweza kusoma Kikamba kwa njia inayostahili na nafikiri ni kwa sababu ya namna inavyoandikwa kutokana na kuwa na vokali nyingi kuliko Kiswahili na Kiingereza.*
>
> Afisa Mkuu Kitengo cha Mimea: *Ni ukweli kabisa kuwa Kikamba ni kigumu sana katika maandishi.*
>
> Afisa Mkuu Idara ya Utamaduni: *Kwa hakika lugha ya Kikamba nayo ni ngumu katika maandishi kwa sababu ya jinsi maneno yake yanavyoendelezwa* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)


Uchanganuzi wa nyaraka nao ulionyesha kuwa kati ya nyaraka zote 23 zilizopatikana hakuna hata moja iliyoandikwa kwa lugha ya kwanza hali inayothibitisha mielekeo hii. Matokeo haya kwa jumla yanaonyesha mielekeo hasi kwa lugha ya Kikamba kutumiwa katika nyaraka hali inayoendana na mhimili wa mielekeo ya mhusika ya Nadharia ya Utendaji Razini unaoshikilia kuwa mielekeo huwa ni kiukulio muhimu cha kubashiri iwapo mhusika angetimiza kitendo fulani. Ni wazi kuwa kutokana na mielekeo hii, lugha ya Kikamba haijateuliwa kutumiwa katika utekelezaji wa maendeleo kupitia kwa nyaraka. Matokeo haya yanathibitisha ukweli wa mhimili huu kwa kuonyesha

kuwa matendo ya mhusika huwa yameathiriwa na fikra zake, ambazo huwa zimeathiriwa na mielekeo, imani, na tabiania kwa sababu kutotumika kwa lugha ya Kikamba katika nyaraka kunatokana na mielekeo hii na fikra zao kuwa lugha ya Kikamba ni ngumu kuisoma na kuandika.

### 4.5.2 Istilahi za Lugha ya Kiswahili Huifanya kuwa Ngumu

Kauli hii ilihusishwa katika utafiti huu kutokana na matumizi duni ya lugha ya Kiswahili hata baada ya kupandishwa hadhi na katiba ya 2010 kuwa lugha rasmi. Kielelezo hiki kinaonyesha matokeo ya uchanganuzi wa miitiko ya watafitiwa.

***Kielelezo 4.5. Miitiko ya watafitiwa***




*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Matokea haya yanaonyesha kuwa 1.7% ya watafitiwa haikukubali kabisa kuwa istilahi za lugha ya Kiswahili huifanya kuwa ngumu, 27.0% haikukubali, 23.5% haikuwa na hakika, 42.6% ilikubali na 5.2% ilikubali kabisa. Kwa jumla, 28.7% waliegemea upande wa kutokubali kuwa istilahi za Kiswahili hukifanya kuwa kigumu kueleza masuala katika utekelezaji wa maendeleo, 23.5% ikiwa haina

hakika na jumla ya 47.8% kuegemea upande wa waliokubali. Matokeo haya yanadhihirisha mielekeo hasi kwa lugha ya Kiswahili hasa pale ambapo lugha rasmi inaohusishwa. Matokeo haya yanafanana na yale ya mahojiano kwa sababu waliohojiwa wote walikubali kuwa lugha ya Kiswahili ni ngumu kutumia kwa sababu istilahi zake hasa sanifu ni ngumu sana. Kauli hizi za wahojiwa zinaonyesha uhalisia wa matokeo haya:

> Afisa Mkuu, Idara ya Utamaduni: *Kiswahili ni lugha ngumu kwa sababu kinabadilikabadilika kwa sababu mimi nilisoma Kiswahili hadi mwaka wa kwanza wa chuo kikuu lakini kile Kiswahili kinachozungumzwa leo kama sanifu siwezi kukielewa.*
>
> Afisa Mkuu, Kitengo cha Mimea: *Kwa mfano, kwa upande wangu nazungumza Kiswahili lakini nikiambiwa niandike barua sitaweza kwa sababu itakuwaje kwamba naandikia mkubwa wangu wa eneo bunge barua kwa Kiswahili kumualika katika mafunzo. Nitaanza vizuri lakini nitapotea kwa njia na itanilazimu nichukue kamusi inisaidia na ikishindikana kabisa nitatumia Kiingereza.*
>
> Afisa Mkuu, Idara ya Biashara: *Lugha ya Kiswahili ni lugha tamu ukipatana na mtu ambaye anaizungumza kwa namna sanifu unaifurahia. Kwa hivyo, kwangu mimi ni lugha safi, tamu na ya kutukuzwa. Hata hivyo, matumizi yake katika mazingira rasmi huwa changamoto miongoni mwa baadhi ya watu lakini kwangu si changamoto kubwa.*
>
> Afisa Mkuu, Idara ya Nyumba na Ukuaji wa Miji: *Ni kweli Kiswahili ni lugha ngumu hasa katika mazingira rasmi… Katika miktadha mingi, lugha ya Kiswahili inachukuliwa kama lugha duni kama vile kwenye mazungumzo katika runinga na hata maingiliano ya kawaida.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Uchanganuzi wa nyaraka 23 za maendeleo zilizokusanywa nao ulitomelea nafasi ya mielekeo hii hasi kuhusu Kiswahili sanifu katika uteuzi wa lugha. Uchanganuzi huu ulionyesha kuwa nyaraka tano pekee (ambayo inawasilisha 21.7%) ndizo zilizokuwa na maandishi ya Kiswahili. Kati ya hizi tano, 3 (13.0% ya nyaraka zote) zilikuwa zimeandikwa kwa Kiswahili pekee japo majina maalumu yalikuwa katika Kiingereza (Kiambatisho 12 na 13) na mbili zilikuwa zimeandikwa kwa Kiingereza na tafsiri ya Kiswahili kuandikwa hapo

(Kiambatisho 10 na 11). Matokeo haya yanalandana na yale ya utafiti wa Mohochi (2011) ulioonyesha kuwa miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki, matumizi duni ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya na Uganda yalitokana na mielekeo hasi ya baadhi ya viongozi wa nchi hizi. Uwiano huu wa matokeo ni kwa sababu matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa matumizi duni ya lugha ya Kiswahili katika miktadha rasmi yanatokana na mielekeo hasi waliyonayo watu kuihusu. Vilevile, matokeo ya utafiti wa Painter na Dixon (2012) kuhusu mielekeo ya lugha nchini Afrika Kusini kuwa mielekeo hasi ya wakoloni kwa lugha asili ilisababisha mielekeo hasi miongoni mwa viongozi wa baada ya ukoloni yanafanana na ya utafiti huu hasa kutokana na kauli ya Afisa Mkuu Idara ya Nyumba na Ukuaji wa Miji kuwa:

> *Ni kweli Kiswahili ni lugha ngumu hasa katika mazingira rasmi. Kwangu mimi nilipenda Kiswahili sana lakini mwalimu wangu alifanya Kiswahili kuwa kigumu hadi kuwacha kukitumia. Vilevile ugumu huu wa Kiswahili unatokana na hali kwamba hatuweki mkazo matumizi ya lugha ya Kiswahili shuleni.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)


Nadharia ya Utendaji Razini kupitia kwa mihimili yake ya mielekeo ya wahusika na mhimili wa kanunibinafsi inaonyesha uthabiti wa matokeo haya. Kwanza, mhimili wa mielekeo ya wahusika unasisitiza kuwa japo yanaweza kuwepo matokeo yasiyotarajiwa, ni rahisi kutabiri tabia ya binadamu na kuwa mielekeo ni kiukulio muhimu cha kubashiri iwapo mhusika angetimiza kitendo fulani au la. Katika matokeo haya, mielekeo hii inathibitika kuwa sababu kuu ya kutotumia Kiswahili katika mazingira rasmi. Mhimili wa kanunibinafsi nao unasema kuwa kipengele cha nia ya mtu binafsi huhusisha manufaa atakayoyapata kutokana na tabia, jambo ambalo linaathiri mwelekeo wake kuhusu tabia husika. Kwa upande mwingine, kipengele cha ushawishi wa kijamii nacho huhusisha ukubalifu au ukataaji wa tabia kutokana na ukubalifu wake na

jamii. Matokeo haya katika kiwango cha kibinafsi yanatokana na watafitiwa kuona matokeo duni kwa kutumia Kiswahili ikilinganishwa na Kiingereza huku kijamii ikitokana na kutokubaliwa kwa Kiswahili kama lugha rasmi na viongozi na Wakenya kwa jumla hata baada ya kufanywa kuwa lugha rasmi.

### 4.5.3 Natumia Lugha ya Kwanza Zaidi

Kauli ililenga kutathmini mielekeo ya watafitiwa kuhusu matumizi ya lugha ya kwanza ikilinganishwa na lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Miitiko ya watafitiwa kwa kauli hii ilichanganuliwa na matokeo yanaonyeshwa katika kielelezo kifuatacho.

***Kielelezo 4.6 Miitiko ya watafitiwa***




*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Matokeo haya yanaonyesha kwamba 6.1% hawakukubali kabisa kuwa wao hutumia lugha ya kwanza zaidi kuliko Kiswahili na Kiingereza katika masuala ya maendeleo, 33.3% hawakukubali, 8.7% hawakuwa na hakika, 40.0% walikubali na 12.2% walikubali kabisa. Kutokana na takwimu hizi, jumla ya 39.1% walionyesha mielekeo hasi kuhusu kutumia lugha ya kwanza katika

masuala ya maendeleo ikilinganishwa na jumla ya 52.2% walioonyesha mielekeo chanya. Mielekeo hii inaonyesha uhusiano uliopo kati ya lugha ya kwanza na utelekezaji wa maendeleo katika Kaunti ya Machakos. Matokeo ya utafiti huu katika sehemu ya ruwaza za matumizi ya lugha katika mawanda mbalimbali ni dhihirisho zaidi ya uhusiano huu kwa sababu katika kila mawanda, lugha ya Kikamba inatumika. Zaidi ni kuwa, katika mazingira ya mashinani, Wakamba ni wengi na lugha ya Kikamba ilitambuliwa kuwa ndiyo bora kabisa katika kuendeleza harakati za kutekeleza maendeleo. Hali hii inadhihirisha zaidi uhusiano huu wa mielekeo ya lugha ya Kikamba na nafasi yake katika utekelezaji wa maendeleo.

Kwa kuzingatia kiwango cha elimu katika mielekeo hii, miongoni mwa wale ambao hawakukubali kabisa, 42.9% ilikuwa ya wale ambao wamesoma hadi vyuo vikuu na vya kati, 28.6% wale waliosoma hadi kidato cha nne na 28.6% wale waliosoma hadi darasa la nane. Vilevile, miongoni mwa wale ambao hawakukubali, 50.0% ilikuwa ni wale waliosoma hadi vyuo vikuu na vya kati, 36.8% wale waliosoma hadi kidato cha nne na 6.2% wale waliosoma hadi darasa la nane. Hakuna ambaye hajawahi kusoma aliyekosa kukubali kabisa au aliyekosa kukabali. Matokeo haya yanaonyesha kuwa matumizi ya lugha ya Kikamba kueleza maendeleo miongoni mwa watu wa viwango vya juu vya elimu (kidato cha nne na vyuo vikuu na vya kati) yanaweza kuathiri utekelezaji wa maendeleo kwa namna hasi. Yanaonyesha pia kuwa matumizi ya lugha ya Kikamba katika kutekeleza masuala ya maendeleo miongoni mwa watu wa viwango vya chini vya elimu (wale hawajawahi kusoma na darasa la nane) yana athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo.

Kwa kuzingatia kazi waliyoifanya watafitiwa, matokeo yalionyesha kuwa miongoni mwa wale ambao hawakukubali kabisa, asilimia ya juu kabisa (42.9%) ilikuwa ni wale wanaofanya biashara. Vilevile, miongoni mwa wale ambao hawakukubali, asilimia kubwa zaidi (28.9%) ilikuwa ni wale wanaofanya biashara, ikifuatiwa kwa karibu na wale wanaofanya kazi ofisini (26.3%). Kwa upande mwingine, asilimia kubwa zaidi ya waliokubali kabisa ilihusisha watu wanaofanya kazi shambani (35.7%) ikifuatiwa na wale wanaofanya kazi nyumbani (28.6%). 37% ya waliokubali walikuwa ni wale wanaofanya kazi za biashara na 28.3% ya wale wanaofanya kazi katika sehemu nyingine. Matokeo haya yanaonyesha mielekeo hasi kwa matumizi ya lugha ya kwanza miongoni mwa watu wanaofanya kazi ofisini na pia biashara na mielekeo chanya kwa wale wanaofanya kazi shambani, nyumbani na pia katika biashara. Nadharia ya Utendaji Razini kupitia mhimili wake wa kanunibinafsi unathibitisha matokeo haya kwa kusisitiza kipengele cha nia ya mhusika binafsi katika mielekeo huhusisha manufaa atakayoyapata kutokana na tabia husika. Miongoni mwa wanabiashara matumizi ya lugha ya kwanza itaathiri biashara zao iwapo watakosa wateja ambao hawawezi kuelewa Kikamba katika Kaunti ya Machakos hali inayoendana na mhimili huu. Vilevile, mielekeo chanya kuhusu matumizi ya lugha ya kwanza katika miktadha ya shambani na nyumbani inatokana na ukweli wa mhimili huu kwa sababu lugha hii huwasaidia kuwa na mawasiliano bora na yanayoeleweka kabisa. Zaidi ni kuwa mahojiano na Afisa Mkuu wa Idara ya Biashara yanaonyesha mielekeo hii hasi katika maeneo ya mjini kuwa

> *Hali huwa tofauti kabisa (katika maeneo ya mjini) na kinyume cha mashinani kwa sababu ukizungumza kwa lugha ya Kikamba itawaacha watu wengi sana nje ya mchakato wa utekelezaji wa maendeleo kwa sababu watu ambao hawaelewi Kikamba watakuona*

*kama mkabila, watakuchukia na hata kukuona kama mshamba.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)

Matokeo haya yanaonyesha mielekeo hasi kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika miktadha rasmi sio tu katika katika Kaunti ya Machakos bali pia katika maeneo mengine ambako matumizi haya yamebaki duni. Zaidi, sehemu hii imeonyesha sababu za mielekeo hii na jinsi inavyoathiri uteuzi wa lugha ya Kiswahili katika miktadha rasmi. Kwa mujibu wa matokeo haya, matumizi ya lugha ya kwanza katika mazungumzo ya maendeleo yanathibitika kutokana na manufaa wananchi wanayoyapata kutokana na matumizi ya lugha ya Kikamba. Hii ndiyo hali halisi ya mhimili wa kanunibinafsi wa Nadharia ya Utendaji Razini unashikilia kuwa iwapo binadamu yeyote anafanya jambo litakalomnufaisha, atakuwa na mtazamo kubalifu.

### 4.5.4 Ninapendelea Viongozi Wakitumia Kiingereza

Katika sehemu ya 4.4.1, matokeo yalionyesha kuwa viongozi hutumia lugha za Kikamba, Kiswahili na Kiingereza wanapoelezea masuala ya maendeleo. Kwa kutambua viwango tofauti vya elimu miongoni mwa watafitiwa na wananchi kwa jumla kama inavyodhihirika katika sehemu ya 4.2.3, sehemu hii ilikadiri mielekeo ya wananchi kuhusu matumizi ya Kiingereza miongoni mwa viongozi na washikadau wengine wa maendeleo ikilinganishwa na lugha za Kikamba na Kiswahili. Jedwali lifuatalo linawasilisha miitiko ya watafitiwa ya kauli hii.

***Jewali 4.17 Miitiko ya watafitiwa***

| | **Mdafao** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| SK | 23 | 20.0 |
| S | 39 | 33.9 |
| SH | 10 | 8.7 |
| N | 35 | 30.4 |
| NK | 8 | 7.0 |
| **JUMLA** | **115** | **100.0** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Kwa mujibu wa matokeo haya, watafitiwa 23 (20.0%) hawakukubali kabisa kuwa wao hupendelea viongozi na washikadau wengine wa maendeleo kutumia Kiingereza zaidi wanapowaeleza masuala ya maendeleo, 39 (33.9%) hawakukubali, 10 (8.7%) hawakuwa na hakika, 35 (30.7%) walikubali na 8 (7.0%) walikubali kabisa. Kwa jumla, 53.9% ya watafitiwa walikuwa na mielekeo hasi kuhusu viongozi na washikadau wa maendeleo kutumia lugha ya Kiingereza wanapoelezea masuala ya maendeleo huku 37.4% wakiwa na mielekeo chanya. Kwa mujibu wa uchanganuzi wa awali, ni wazi kwamba iwapo lugha ya Kiingereza itatumika hasa katika mazingira ya mashinani, basi lugha hii itakuwa na athari hasi kwa utekelezaji wa maendeleo na iwapo itatumika katika maeneo ya mijini basi itakuwa na athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo hasa mjini Mlolongo. Uchanganuzi huu unasisitiza sababu ya mielekeo hii hasi na chanya kuhusu kutumika kwa lugha ya Kiingereza miongoni mwa watafitiwa kutoka maeneo ya mashinani na mijini.

Mielekeo hii hasi kwa matumizi ya lugha ya Kiingereza katika kuelezea masuala ya maendeleo inaendana na mhimili wa Nadharia ya Utendaji Razini wa kanunibinafsi unaoshikilia kuwa kijamii mielekeo hutokana na ukubalifu au ukataaji wa tabia husika na jamii. Katika muktadha huu, wengi wa wananchi, hasa katika mazingira ya mashinani, hawaielewi lugha hii kutokana na viwango vya elimu na umri na hivyo mielekeo husika.

### 4.5.5 Ninatumia Kiswahili na Watu wa Jamii Nyingine

Kauli hii ililenga kukadiria mielekeo ya watafitiwa kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika maingiliano ya kimaendeleo na watu wa jamii nyingine katika muktadha huu wa wingilugha. Miitiko ya watafitiwa kwa kauli hii inawasilishwa katika jedwali lifuatalo:

*Jedwali 4.18 Miitiko ya watafitiwa*

| | Mdafao | Asilimia |
|---|---|---|
| S | 6 | 5.2 |
| N | 41 | 35.7 |
| NK | 68 | 59.1 |
| **JUMLA** | **115** | **100.0** |

*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022)*

Jedwali hili linaonyesha kwamba watafitiwa 6 (5.2%) hawakukubali kutumia Kiswahili wanapoingiliana na watu wa jamii nyingine katika masuala ya maendeleo, 41 (35.7%) walikubali na 68 (59.1%) walikubali kabisa kuwa wanatumia Kiswahili zaidi pale maendeleo yanapohusisha watu wa jamii nyingine kuliko wanavyotumia Kiingereza. Kutoka na takwimu hizi, jumla ya 5.2% ndio walio na mwelekeo hasi huku jumla ya 94.8% ikiwa na mwelekeo chanya kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika miktadha ya maendeleo inayohusisha watu wa jamii nyingine. Mielekeo hii inaonyesha kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mazingira yaliyo na wingilugha yatakuwa na athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo ikilinganishwa na lugha ya Kiingereza ambayo itakuwa na athari hasi kwa utekelezaji wa maendeleo. Kauli za mahojiano na baadhi ya maafisa wa idara lengwa yalidhihirisha ukweli wa matokeo haya. Kauli zao zilikuwa kama zifuatavyo:

> Afisa Mkuu, Idara ya Biashara: *Lugha ya Kiswahili ndiyo huwaunganisha watu wa makabila tofautitofauti katika maneneo ya mashinani na hata mijini na huwa na athari chanya hasa pale ambapo watu wanazungumza lugha tofautitofauti.*
>
> Afisa Mkuu, Idara ya Nyumba na Ukuaji wa Miji: *Katika maeneo ya Vizingasifa, hasa vya mashinani, tunaipa lugha ya Kiswahili kipaumbele kutokana na uwezekano wa kuwepo na watu wa jamii nyingine wasioelewa Kikamba.* (Chanzo: Utafiti wa Nyanjani, 2022).

Ukweli huu unathibitisha matokeo ya kauli ya kiwango cha maingiliano ya watafitiwa na watu wa jamii jirani ambapo matokeo yalionyesha kuwa jumla ya watafitiwa 111 (96.5%) waliingiliana na watu kutoka jamii nyingine

ikilinganishwa na wale waliokosa kukubali 1 (0.9%) kuingiliana na jamii jirani na wale ambao hawakuwa na hakika 3 (2.6%).

### 4.6 Hitimisho

Sura hii imewasilisha matokeo ya utafiti kulingana na madhumuni matatu ya utafiti na kujibu swali la kwanza, la pili na la tatu la utafiti. Madhumuni haya yalihusisha uchanganuzi wa ruwaza za matumizi ya lugha katika Kaunti ya Machakos, utathmini wa uhusiano na athari za lugha mbalimbali katika utekelezaji wa maendeleo na nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha mahsusi ya kuundia na kuwasilishia sera za maendeleo katika Kaunti ya Machakos. Utafiti huu ulitumia muundo mseto na hivyo data za kitakwimu na kitaamuli zimetumika katika sura hii. Vilevile, msingi wa kinadharia wa utafiti huu ulihusisha Kiunzi cha Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi na Nadharia ya Utendaji Razini. Kwa mujibu wa madhumuni ya kwanza, sura hii imewasilisha ruwaza za matumizi ya lugha katika mawanda manane. Imebainisha kuwa misimbo ya Kikamba na Kiswahili na mseto wa Kiswahili na Kikamba ni maarufu zaidi katika mawanda husika katika maeneo ya mashinani huku misimbo ya Kiswahili na Kiingereza na miseto inayohusisha Kiingereza ikiwa na umaarufu katika maeneo ya mjini. Kwa mujibu wa madhumuni ya pili, matokeo yameonyesha kuwa katika maeneo ya mijini lugha za Kiswahili na Kiingereza huwa na athari chanya huku za Kikamba na lugha nyingine zikiwa na athari hasi. Katika maeneo ya mashinani, lugha za Kikamba na Kiswahili huwa na athari chanya huku Kiingereza na lugha nyingine zikiwa na athari hasi. Mielekeo imetambuliwa kuchukua nafasi muhimu katika uteuzi wa lugha kwa kuonyesha jinsi ilivyoelekeza uteuzi wa lugha mbalimbali katika miktadha mbalimbali.

# SURA YA 5

# MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha muhtasari wa tasnifu hii kwa mujibu wa madhumuni matatu ya utafiti kwa kuzingatia matokeo yaliyopatikana. Vilevile, inawasilisha mahitimisho yaliyotokana na matokeo ya utafiti na kuishia kwa uwasilishaji wa mapendekezo.

## 5.2 Muhtasari

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya kwanza ambayo ni utangulizi inaonyesha vipengele vya kimsingi vya tasnifu hii. Sura ya pili inahakiki maandishi yanayoendana na madhumuni matatu ya utafiti huu yaliyokwisha andikwa kutokana na tafiti za awali. Sura ya tatu, inafafanua mbinu na njia za utafiti. Sura ya nne inachanganua data na kuwasilisha matokeo yanayotokana na data za kitaamuli na za kitakwimu kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Sura ya tano ni muhtasari wa tasnifu yote, mahitimisho na mapendekezo kwa serikali ya Machakos na ya utafiti wa baadaye.

## 5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya utafiti huu kwa muhtasari.

### 5.3.1 Ruwaza za Matumizi ya Lugha

Ruwaza za matumizi ya lugha katika maeneo yenye wingilugha katika Kaunti ya Machakos hutegemea mawanda maalum ambamo lugha inatumiwa. Katika mawanda ya sokoni, ruwaza za matumizi ya lugha zilikuwa Kikamba (7.0%), Kiswahili (14.8%), mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza (6.1%), mseto

wa Kiswahili na Kikamba (68.7%) na mseto wa Kiswahili na Kiingereza (3.5%). Katika mawanda ya nyumbani ruwaza za matumizi ya lugha zilihusisha Kikamba (53.9%), Kiswahili (6.1%), Kiingereza (0.9%), Lugha nyingine (11.3%), mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza (5.7%), mseto wa Kiswahili na Kikamba (7.8%), na mseto wa Kiswahili na Kiingereza (4.3%). Katika mawanda ya hospitalini ruwaza zilihusisha Kikamba (0.9%), Kiswahili (21.7%), Kiingereza (0.9%), mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza (17.4%), mseto wa Kikamba na Kiswahili (49.6%) na mseto wa Kiswahili na Kiingereza (9.6%). Katika mawanda ya shambani ruwaza za matumizi ya lugha zilikuwa Kikamba (64.0%), Kiswahili (14.4%), Lugha nyingine (4.4%), mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza (2.6%), mseto wa Kiswahili na Kikamba (12.3%) na mseto wa Kiswahili na Kiingereza (1.8%). Katika mawanda ya kazini, ruwaza zilihusisha Kikamba (15.7%), Kiswahili (11.3%), mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza (20.0%), mseto wa Kiswahili na Kikamba (43.5%) na mseto wa Kiswahili na Kiingereza (9.6%). Katika mawanda ya mikutano ya maendeleo, ruwaza za matumizi ya lugha ni Kikamba (18.3%), Kiswahili (13.9%), Kiingereza (0.9%), mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza (17.5%), mseto wa Kiswahili na Kikamba (35.7%) na mseto wa Kiswahili na Kiingereza (8.7%). Katika mafunzo ya kilimo ruwaza ni Kikamba (18.3%), Kiswahili (13.9), Kiingereza (0.9%), mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza (20.9%), mseto wa Kiswahili na Kikamba (37.4%), na mseto wa Kiswahili na Kiingereza (98.7%). Katika mawanda ya biashara ruwaza za matumizi ya lugha zinahusisha Kikamba (7.0%), Kiswahili (11.3%), mseto wa Kiswahili, Kikamba na Kiingereza (25.2%), mseto wa Kiswahili na Kikamba (53.9%), na mseto wa Kiswahili na Kiingereza (2.6%).

### 5.3.2 Uhusiano na Athari za Lugha Mbalimbali kwa Utekelezaji wa Maendeleo

Kutokana na uchunguzi wa jinsi lugha mbalimbali zilivyohusiana na kuathiri utekelezaji wa maendeleo, matokeo ya hojaji na mahojiano yalionyesha kuwa athari hizi za lugha maalumu hutegemea maeneo zinamotumiwa na sifa za walengwa wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Katika maeneo ya mijini, matokeo yamebainisha kuwa lugha za Kiswahili na Kiingereza pamoja na miseto isiyo na Kikamba huwa na uhusiano mzuri na utekelezaji wa maendeleo na hivyo kuwa na athari chanya kinyume na lugha za Kikamba na lugha nyingine ambazo zina athari hasi. Katika maeneo ya mashinani, idadi ya Wakamba ilitambuliwa kuwa ya juu ikilinganisha na watu wa jamii nyingine hali iliyopelekea matokeo haya kuonyesha kuwa lugha hii kuwa na athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo ikifuatiwa na Kiswahili. Lugha ya Kiswahili inaleta athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo katika maeneo haya kutokana na kuwepo kwa watu wasioelewa Kikamba na kuwa takriban watu wote wanaelewa lugha ya Kiswahili. Hali ni tofauti katika maeneo ya mashinani kuhusu lugha ya Kiingereza kwa sababu kina athari hasi kwa utekelezaji wa maendeleo kwa kiwango kikubwa. Miongoni mwa vijana waliosoma hadi viwango vya kidato cha nne na vyuo, lugha za mama zilitambuliwa kuathiri utekelezaji wa maendeleo kwa njia hasi huku Kiswahili na Kiingereza kikiwa na athari chanya.

Katika mazingira ya mijini, msimbo wa Sheng' ulitambuliwa kuwa na uhusiano wa karibu sana na maendeleo na utekelezaji wa maendeleo yanayolenga vijana. Miongoni mwa watu wa umri wa zaidi ya miaka 46, lugha za mama zilitambuliwa kuwa na athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo ikilinganishwa na lugha nyingine. Kwa kuzingatia kigezo cha elimu, matokeo

yanaonyesha kuwa miongoni mwa watu waliosoma hadi katika kidato cha nne na chuo kikuu au cha kati, lugha ya Kiingereza huathiri utekelezaji wa maendeleo kiuchanya zaidi ikifuatiwa na Kiswahili. Lugha za kwanza zilitambuliwa kuwa na athari hasi. Kwa upande wa wale ambao wamesoma hadi katika darasa la nane au hawajawahi kusoma, lugha ya Kikamba ndiyo iliyo na athari chanya zaidi ikifuatiwa na Kiswahili katika utekelezaji wa maendeleo. Kwa upande mwingine, lugha ya Kiingereza ina athari hasi kwa utekelezaji maendeleo miongoni mwa kundi hili.

### 5.3.3 Nafasi ya Mielekeo Katika Uteuzi wa Lugha

Matokeo ya data zilizolenga madhumuni haya yalionyesha kuwa mielekeo huwa na nafasi kubwa katika uteuzi wa lugha. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti, kuhusu matumizi ya lugha ya kwanza katika nyaraka, 62.6% walikuwa na mwelekeo hasi, 18.3% hawakuwa na hakika, na 19.1% mwelekeo chanya. Hali hii ilisababisha lugha hii kutotumiwa katika nyaraka za maendeleo. 28.7% walikuwa na mielekeo chanya, 23.5% hawakuwa na hakika, huku 47.8% wakiwa na mielekeo hasi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili rasmi katika muktadha wa utekelezaji maendeleo. Mielekeo hii ilisababisha watafitiwa wengi kutotumia Kiswahili rasmi katika mazingira rasmi na kutumia Kiingereza. Matokeo yalionyesha pia kuwa 39.1% wana mielekeo hasi kwa matumizi ya lugha ya Kikamba katika mazungumzo ya kimaendeleo, 52.2% wana mieleko chanya, huku 18.2% wakiwa hawana hakika. Mielekeo hii ilisababisha lugha hii kutumika sana katika maeneo ya mashinani na kutotumika sana katika maeneo ya mijini.

Vilevile, matokeo yanaonyesha kuwa 53.9% walikuwa na mielekeo hasi kwa matumizi ya Kiingereza katika kuelezea mambo ya maendeleo, 8.7% walikuwa

hawana hakika huku 37.3% wakiwa na mielekeo chanya. Ni kutokana na mielekeo hii ambapo maafisa waliohojiwa walitumia lugha ya Kikamba zaidi katika maeneo ya mashinani na Kiswahili zaidi katika maeneo ya mijini katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo. Mwisho, matokeo yalionyesha kuwa 94.8% walikuwa na mielekeo chanya kuhusu matumizi ya Kiswahili katika maingiliano ya kimaendeleo na jamii nyingine huku 5.2% wakiwa na mielekeo hasi. Mielekeo hii ilisababisha matumizi mapana ya lugha ya Kiswahili katika muktadha wa Kaunti ya Machakos ulio na wingilugha dhahiri.

### 5.4 Mahitimisho

Katika sehemu hii, mtafiti anawasilisha mahitimisho yanayotokana na matokeo ya utafiti huu.

#### 5.4.1 Ruwaza za Matumizi la Lugha

Ruwaza za matumizi ya lugha zitazidi kutofautiana kutegemea mawanda maalumu, jamii za wahusika katika mawanda haya, umri wao, kiwango cha elimu yao, na hata jinsia yao. Muhimu kwa serikali ya Kaunti ya Machakos ni kuhakikisha kuwa matumizi ya lugha katika mawanda ya sokoni, nyumbani, hospitalini, shambani, kazini, mikutano ya maendeleo, mafunzo ya kilimo, biashara na mawanda mengine ambamo maendeleo yanatekelezwa yanawahusisha wananchi wote wenye sifa tofautitofauti. Kutokana na matokeo, utafiti huu unahitimisha kuwa katika maeneo ya mashinani lugha ya Kikamba inastahili kupendelewa zaidi katika shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika mazingira ambapo kila mwananchi anaielewa vizuri. Kiswahili nacho kinastahili kupendelewa katika mazingira ya mashinani ambako kuna watu wasioelewa

Kikamba na mijini ambako kuna watu wa jamii mbalimbali kwa sababu kinaeleweka na watu wengi zaidi kinyume na Kiingereza.

### 5.4.2 Uhusiano na Athari za Lugha Mbalimbali kwa Utekelezaji wa Maendeleo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, sehemu hii inahitimisha kuwa lugha mbalimbali huhusiana na kuathiri utekelezaji wa maendeleo kwa namna tofautitofauti kutegemea eneo husika na walengwa wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Miongoni mwa watu wanaoishi mijini, utafiti huu unahitimisha kuwa lugha za Kiswahili na Kiingereza zina athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo ikilinganishwa na Kikamba na lugha nyingine. Katika maeneo ya mashinani, utafiti huu unahitimisha kuwa lugha ya Kikamba ina athari chanya zaidi ikilinganishwa na lugha zingine zote ikifuatiwa na Kiswahili, Katika maeneo yaliyo na wingilugha wenye watu wasioelewa Kikamba, Lugha ya Kiswahili huwa na athari chanya zaidi. Vilevile, lugha za Kiingereza na Kiswahili ni bora zaidi katika utekelezaji wa maendeleo miongoni mwa vijana na watu wanaoishi mjini. Katika maeneo ya mjini, hasa Mlolongo, utafiti huu unahitimisha kuwa msimbo wa Sheng’ una nafasi kubwa na maalumu katika maendeleo yanayolenga vijana.

### 5.4.3 Nafasi ya Mielekeo katika Uteuzi wa Lugha.

Katika msingi wa matokeo yaliyowasilisha katika sura ya nne, utafiti huu unahitimisha kuwa mielekeo ina nafasi kubwa sana katika uteuzi wa lugha ya kutumia katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo katika Kaunti ya Machakos. Iwapo lugha ya Kikamba itatumika katika nyaraka za maendeleo basi italazimu mielekeo hasi kuihusu katika nyaraka kubadilika. Vilevile, iwapo lugha ya Kiswahili itatumika katika mazingira rasmi ya utekelezaji wa

maendeleo, basi serikali ya Machakos haina budi kubadilisha mielekeo hasi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu katika mazingira haya miongoni mwa wafanyikazi na wananchi kwa jumla.

## 5.5 Mapendekezo

Utafiti huu unatoa mapendekezo kwa Kaunti ya Machakos kuhusu matumizi ya lugha katika utekelezaji wa maendeleo na pia kutoa mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

### 5.5.1 Mapendekezo kwa Kaunti ya Machakos

Utafiti huu unapendekeza kuwa:

i. Kaunti ya Machakos ifanye usajili wa lugha mbalimbali zinazozungumzwa katika kaunti hiyo na msambao wa watu wa lugha hizi ili kubainisha hali ya wingilugha.

ii. Kaunti ya Machakos iweke mikakati ya kuajiri wataalamu wa tafsiri na ukalimani ili kutafsiri na kufasiri nyaraka maalumu ili kuhakikisha zinabeba ujumbe uliolengwa.

### 5.5.2 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye

Utafiti huu unapendekeza kuwa utafiti wa baadaye ufanywe kuhusu:

a. Sheng’ na maendeleo ya vijana katika muktadha wa mijini nchini Kenya.
b. Mikakati ya kuondoa mielekeo hasi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi katika mazingira rasmi nchini Kenya.

## MAREJELEO

Ajzen, I. na Fishbein, M. (1980). *Understanding attitudes and predicting social behaviour.* Prentice- Hall Inc.

Almeidai, F. (2018). Strategies to perform a mixed methods study. *European Journal of Education Studies*, *5*(1), 137- 151. Retrieved March 10, 2022 from https://core.ac.uk/download/pdf/236101754.pdf

Arnold, D. G. (2021). Universal research ethics and international business studies. *Journal of International Business Studies*, *52*(7), 1229–1237. Retrieved March 8, 2022 from https://link.springer.com/article/10.1057/s41267-021-00418-1

Best, W.J na Kahn J.V. (2010) *Research in Education*. New Jersey U.S.A: Person Prentice

Baruch, Y. (1999). Response rate in academic studies-A comparative analysis. *Human Relations*, *52*(4), 421-438. Retrieved July 20, 2022 https://doi.org/10.1177/001872679905200401

Chhaya, K. S. (2017). 'Economic development and language: A journey through India'. *SSRN Electronic Journal*. Retrieved March 4, 2022 from https://doi.org/10.2139/ssrn.3053765

Cook, J. V., Dickinson, H. O., & Eccles, M. P. (2009). Response rates in postal surveys of healthcare professionals between 1996 and 2005: An observational study. *BMC Health Services Research* 9(1). Retrieved August 9, 2022 from https://doi.org/10.1186/1472-6963-9-160

Crystal, D. (2010) *The Cambridge encyclopedia of language*. Cambridge: Cambridge University Press.

Dhingra, M., & Dhingra, V. (2012). *Research methodology* (1st ed.). Enkay Publishing House.

Frawley, W.J. (2003) *International encyclopedia of linguistics* Vol 2. London: Oxford University Press.

Imbunya, J. K. (2020). *Research methods simplified for the 21st century and beyond* (1st ed.). Jabayonko Artworks.

Jain, T. (2011). Common tongue: The impact of language on economic performance. *SSRN Electronic Journal*. Retrieved April 3, 2022 from https://doi.org/10.2139/ssrn.1947148

Kamau, S. N. (2015). *Taathira za Kiswahili na Lugha Nyingine kwa Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha za Mama Mijini Nairobi, Kiambu na Thika: Mfano wa Kikuyu* [Doctoral dissertation]. Retrieved April 10, 2022 from https://ir-library.ku.ac.ke/bitstream/handle/123456789/14348/Taathira%20za%20kiswahili%20na%20lugha%20nyingine%20kwa%20uthabiti%20wa%20kiisimujamii....pdf?sequence=1&isAllowed=y

Kavoi, J. K. (2019). *Mielekeo Ya Wanafunzi Kuhusu Ufundishaji Wa Stadi Za Mawasiliano Kwa Kiswahili Katika Taasisi Za Kiufundi Za Kitaifa Nchini Kenya* [Doctoral dissertation]. Retrieved March 5, 2022 from http://repository.rongovarsity.ac.ke/bitstream/handle/123456789/2071/JACKSON%20MUTUKU%20KAVOI.pdf?sequence=1&isAllowed=y

Kawonga, G. A. (2019). *Nafasi ya Kiswahili katika mandhari-lugha: Uchambuzi kifani wa mabango ya matangazo ya makampuni ya mawasiliano ya simu*. Apache Tomcat/8.5.60. Retrieved April 26, 2022 from https://ir.mu.ac.ke:8080/xmlui/handle/123456789/3779

KNBS. (2019). *The 2019 Kenya population and housing census: Population by County and sub-County* (1). Kenya National Bureau of Statistics.

Retrieved April 13, 2022 from https://www.knbs.or.ke/2019-kenya-population-and-housing-census-reports/

Kevogo, A. U., Kitonga, N. N., & Adika, S. K. (2015). Multilingualism and language use patterns: Students attitude towards Kiswahili in Garissa town, Kenya. *Research on Humanities and Social Sciences*, *5*(4), 185-193. Retrieved May 3, 2022 from https://www.researchgate.net/publication/356392181Multilingualismand_Language_Use_Patterns_Students_Attitude_towards_Kiswahili_in_Garissa_Town_Kenya?enrichId=rgreq-1dcc5d30f36bc92d688028d9 8a7a27e2-XXX&enrichSource=Y292ZXJQYWdlOzM1NjM5MjE4M TtBUzoxMDkxOTU5OTcyMjEyNzQxQDE2MzczNTQ5NTM2NjI%3D&el=1_x_3&_esc=publicationCoverPdf

Kothari, C. R. (2004). *Research methodology. Methods and techniques* (Second Revised Edition). New Delhi: New Age International Ltd Publishers.

Kothari, C. R. na Garg, G. (2019). *Research methodology. Methods and techniques* (Fourth Edition). New Delhi: New Age International Ltd Publishers.

LINEE. (2010). Challenges of multilingualism in Europe: Core findings of the LINEE *(9). Language in a Network of European Excellence*. Retrieved February 25, 2022 from https://cordis.europa.eu/docs/results/28/28388/124376831-6_en.pdf

Machakos County. (2022). *About us*. Machakos County – The Place to Be! Retrieved March 3, 2022, from https://machakosgovernment.co.ke/about-us/

Mishra, P., Pandey, C. M., Singh, U., Gupta, A., Sahu, C., & Keshri, A. (2019, January). *Descriptive statistics and normality tests for statistical data*.

PubMed Central (PMC). Retrieved September 5, 2022 from https://www.ncbi.nlm.nih.gov/pmc/articles/PMC6350423/

Mohochi, S. (2011). Mielekeo ya wasomi wa Kiswahili na viongozi wa Afrika Mashariki kuhusu lugha ya Kiswahili. *Swahili Forum*, 24-36.

Mugenda, O. M na Mugenda, A. G. (2003). *Research methods: Qualitative and quantitative methods*. Nairobi: Acts press.

Mwangi, W. D. (2016). *Changamoto na Manufaa ya Kutafsiri Kiswahili Katika Miktadha ya Wingilugha Narok Kaskazini* [Master's thesis]. Retrieved April 15, 2022 from http://erepository.uonbi.ac.ke/bitstream/handle/11295/97178/CLS%20606%20PROJECT%20COPLETE%20FINAL%20COPY.pdf?sequence=1

Mutua, J. N., & Kiruhi, T. M. (2021). Village elders' participation in public governance in Kenya: A phenomenological study. *Open Journal of Leadership*, *10*(02), 110-128. Retrieved April 1, 2022 from https://doi.org/10.4236/ojl.2021.102008

Nation. (2015, September 26). *Raila encourages use of vernacular language in County assembly* [Video]. YouTube. Retrieved March 18, 2022 from https://www.youtube.com/watch?v=6ebsmfrw3XY

Nursanti, E., Andriyanti, E., Kurnianta, P., & Sudartinah, T. (2020). Patterns of language use among multilingual university students majoring in English. *LITERA*, *19*(2), 231-244. Retrieved April 6, 2022 from Https://Www.Researchgate.Net/Publication/343209767_Patterns_Of_Language_UseAmong_Multilingual_University_Students_Majoring_In_English

Nyandwaro, L. K. (2015). *Mielekeo Ya Wafanyakazi Kuhusu Kiswahili Kama Lugha Rasmi Katika Wizara Za Serikali Nchini Kenya: Mintaarafu,*

*Kaunti Ya Kisii* [Master's thesis]. Retrieved February 19, 2022 from https://ir-library.ku.ac.ke/handle/123456789/13476

Painter, D. & Dixon, J. (2012). Language Attitudes in Southern Africa. *To Cindy Galloris*, 105.

Pendakur, K., & Pendakur, R. (2015). Speak and ye shall receive: Language knowledge as human capital. In *Economic Approaches to Language and Bilingualism. New Canadian Perspectives* (1st ed., pp. 89-120). EDRS.

Rassool, N., Edwards, V., & Bloch, C. (2006). Language and development in multilingual settings: A case study of knowledge exchange and teacher education in South Africa. *International Review of Education*, *52*(6), 533-552. Retrieved March 2, 2022 from https://doi.org/10.1007/s11159-006-9008-x

Saidi, M. V. (2021). Kiswahili na maendeleo mashambani nchini Kenya. *Jarida la CHAKITA*, *1*(1), 19-26.

Sangili, N. K. (2019). *Udumishaji wa Lugha ya Kimaragoli Katika Eneobunge la Uriri, Kenya* [Doctoral dissertation] Retrieved March 6, 2022 from http://repository.rongovarsity.ac.ke/bitstream/handle/123456789/2073/SANGILI%20NABETA%20NIXON%20KENYANI.pdf?sequence=1&isAllowed=yChuo Kikuu cha Rongo

Sarantakos, S. (2005). *Social research*. Palgrave Macmillan.

Sridhar, K. K. (1996). Societal multilingualism. In *Sociolinguistics and Language Teaching* (11th ed., pp. 47-70). Cambridge University Press.

Wamalwa, E. W., Mohochi, E. S., & Odeo, E. I. (2019). *Mielekeo ya Lugha Na Ruwaza Za Matumizi ya Lugha ya walimu wa Kiswahili wa shule*

*Za msingi*. Repository Home. Retrieved July 26, 2022, from https://erepository.kibu.ac.ke/handle/123456789/2329

Wambugu, L., & Njoroge, N. (2022). The search for understanding of mixed method research among graduate students: A case of learners in the school of continuing and distance education, university of Nairobi, Kenyaeducation, university of Nairobi, Kenya. *Quality and Quantity*, *56*(2), 843-855. Retrieved August 23, 2022 from, https://link.springer.com/article/10.1007/s 11135-021-01150-6

Walsh, J. (2006). Language and socio-economic development. Towards a theoretical framework. *Language Problems & Language Planning*, *30*(2), 127-148. Retrieved March 9, 2022, https://doi.org/10.1075/lplp.30.2.03wal

Wisbey, M. (2016, October). *Sustainable Development through Multilingual Education* [Paper presentation]. 5th International Conference on Language and Education, Bangkok, Thailand. Retrieved May 24, 2022, from http://www.lc.mahidol.ac.th/mleconf/2016/program.htm

## VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO 1 A:

## HOJAJI FUNGE

Kwa msailiwa mpendwa,
Mimi ni mwanafunzi wa shahada ya uzamili (Masters) na ninafanya utafiti kuhusu **Wingilugha na Athari zake kwa Utekelezaji wa Maendeleo katika Kaunti ya Machakos, Kenya. N**aomba majibu yako kuhusu maswali na kauli zifuatazo. Ujumbe na majibu utakayotoa yatabaki kuwa ya siri na yatatumika kwa minanjili ya utafiti huu pekee.

***Sehemu ya Kwanza: Taarifa kuhusu Msailiwa***
Jaza nafasi iliyoachwa wazi na uweke alama ya vema [√ ] pafaapo kwa jibu lifaalo

**Kijiji ……………………… Kata ………………………. Eneo bunge ……………………**

| | | |
|---|---|---|
| **Jinsia** | Kike | ☐ |
| | Kiume | ☐ |
| **Umri** | Miaka 18-35 | ☐ |
| | Miaka 36-45 | ☐ |
| | Zaidi ya miaka 46 | ☐ |
| **Kiwango cha elimu** | Sijawahi kusoma | ☐ |
| | Darasa la Nane (Std. 8) | ☐ |
| | Kidato cha Nne (Form 4) | ☐ |
| | Chuo Kikuu (University) | ☐ |
| **Kazi Unayoifanya** | Ofisini | ☐ |
| | Nyumbani | ☐ |
| | Shambani | ☐ |
| | Hospitalini | ☐ |
| | Nimejiajiri | ☐ |
| | Sehemu nyingine | ☐ |

***Sehemu ya Pili: Uhusiano na athari za lugha kwa maendeleo, na nafasi ya mielekeo***
Hii sehemu inalenga kukadiria kiwango chako cha kukukabaliana au kutokubaliana na kauli zifuatazo. Jibu kwa kuweka alama [√] kwa jibu lako.

**SEHEMU A: Ruwaza za Matumizi ya Lugha**
Nakubali Kabisa [**NK**], Nakubali [**N**], Sina Hakika [**SH**], Sikubali [**S**], Sikubali Kabisa [**SK**]

| NO. | KAULI | NK | N | SH | S | SK |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kaunti ya Machakos ina watu kutoka jamii mbalimbali | | | | | |
| 2 | Kaunti ya Machakos ina zaidi ya lugha tatu zinazozungumzwa | | | | | |
| 3 | Tunaingiliana sana na watu kutoka jamii jirani katika shughuli za kibiashara, kijamii na kisiasa. | | | | | |
| 4 | Nazungumza zaidi ya lugha moja | | | | | |
| 5 | Katika kijiji chetu kuzungumza lugha nyingi kumesababishwa na sababu zaidi ya moja | | | | | |

Onyesha msimbo au mseto wa lugha kwa kutumia alama [√ ] unaotumia katika maeneo/mawanda yafuatayo: **Kik** – Kikamba, **Kisw** – Kiswahili, na **Kiing** - Kiingereza

| | ***Kik*** | ***Kisw*** | ***Kiing*** | ***L.N*** | ***Kisw+Kik+ Kiing*** | ***Kisw+ Kik*** | ***Kisw+ Kiing*** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Sokoni | | | | | | | |
| Nyumbani | | | | | | | |
| Hospitalini | | | | | | | |
| Shambani | | | | | | | |
| Kazini | | | | | | | |
| Mikutano ya Maendeleo | | | | | | | |
| Vipindi vya Mafunzo ya Kilimo | | | | | | | |
| Biashara | | | | | | | |

**SEHEMU YA B: Uhusiano na Athari za Lugha Mbalimbali kwa Utekelezaji wa Maendeleo**

1. Viongozi wa Kaunti ya Machakos hutumia lugha gani zaidi wanapoelezea masuala ya maendeleo?

   Kikamba ☐ Kisw+Kiing+Kikamba ☐
   Kiswahili ☐ Kikamba+Kiswa ☐
   Kiingereza ☐ Kiswa+Kiingereza ☐
   Lugha nyingine ☐ Kiingereza+Kikamba ☐

2. Je ni lugha gani inapotumika au zinapotumika kuelezea maendeleo unaelewa zaidi?
   Kikamba ☐ Kisw+Kiing+Kikamba ☐
   Kiswahili ☐ Kikamba+Kisw ☐
   Kiingereza ☐ Kiswa+Kiingereza ☐
   Lugha nyingine ☐ Kiingereza+Kikamba ☐

3. Wewe unapenda kusoma maandishi na nyaraka za maendeleo katika lugha ipi au zipi?
   Kikamba ☐ Kisw+Kiing+Kikamba ☐
   Kiswahili ☐ Kikamba+Kiswa ☐
   Kiingereza ☐ Kisw+Kiingereza ☐
   Lugha nyingine ☐ Kiingereza+Kikamba ☐

Kwa nini?
…………………………………………..……………………………………
……..…………………………………….………………………………
…………..…………………………………………..…………………………
………………..……………………Wewe una uwezo wa kuelewa na kuzungumza lugha ngapi?

Moja ☐ Mbili ☐ Tatu ☐ Zaidi ya Tatu ☐

4. Je, uelewa wa idadi ya lugha uliyoitaja unakusaidia vipi kufanya maendeleo?
   Hausadii kabisa ☐ Unasaidia kidogo ☐ Unasaidia sana ☐
5. Je, ni lugha gani inapotumika au zinapotumika zinachangia maendeleo ya eneo hili sana?
   a. …………………………
   b. …………………………
   c. …………………………
   d. …………………………
6. Je, ni lugha gani inapotumika au zinapotumika zinalemaza maendeleo ya eneo hili sana?
   a. …………………………
   b. …………………………
   c. …………………………
   d. …………………………

**SEHEMU C: Nafasi ya Mielekeo katika Uteuzi wa Lugha**

| NO. | KAULI | NK | N | SH | S | SK |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Lugha ya kwanza ndiyo bora kabisa kuleta maendeleo inapotumika katika maandishi na nyaraka za kimaendeleo | | | | | |
| 2 | Msamiati wa lugha ya Kiswahili hukifanya kuwa kigumu sana katika kuelezea masuala ya kimaendeleo | | | | | |
| 3 | Ninapozungumzia masuala ya maendeleo ninapenda kutumia lugha ya kwanza zaidi kuliko Kiswahili na Kiingereza | | | | | |
| 4 | Ninapendelea zaidi viongozi na washikadau wa maendeleo wanapotumia lugha ya Kiingereza kutuelezea mambo ya maendeleo | | | | | |
| 5 | Ninatumia Kiswahili zaidi pale maendeleo yanapohisha watu wa jamii nyingine kuliko Kiingereza | | | | | |

## KIAMBATISHO 1B:

## HOJAJI NUSU FUNGE

### *Sehemu A: Hali ya Wingilugha*

1. Je, katika eneo hili kuna lugha ngapi zinazozungumzwa?
   ………………… Zitaje hapa chini
   a. ………………………… e. …………………………
   b. ………………………… f. …………………………
   c. ………………………… g. …………………………
   d. ………………………… h. …………………………
2. Kati ya lugha hizi wewe unaelewa na kuzungumza ngapi?
   …………… Zitaje
   i. ………………… iv. …………………..
   ii. ……………....... v. ………………….…
   iii. ………………… vi. ………………..…
3. Hebu eleza jinsi mnavyotumia lugha ulizozitaja hapa juu katika maendeleo ya eneo hili
   ………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………
   …………………………
4. Mnaposhirikia katika shughuli za kimaendeleo na majirani mnatumia lugha ipi au zipi?
   a) Kikamba ☐ e) Kisw+Kiing+Kikamba ☐
   b) Kiswahili ☐ f) Kikamba+Kisw ☐
   c) Kiingereza ☐ g) Kisw+Kiingereza ☐
   d) Lugha nyingine ☐ h) Kiingereza+Kikamba ☐
   Lugha hii au hizi zinawasaidia vipi kupata maendeleo?
   ………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………
5. Matumizi ya lugha zaidi ya mbili katika eneo hili yanaletwa na nini?
   a) ………………………………………………………………………………
   b) ………………………………………………………………………………
   c) ………………………………………………………………………………
   d) ………………………………………………………………………………
   ***e)*** ………………………………………………………………………………

### *Sehemu B: Uhusiano na aAthari za lugha mbalimbali kwa maendeleo*

6. Je ni lugha gani kati ya Kikamba, Kiswahili, na Kiingereza ambayo viongozi wenu wa kisiasa na washikadau wengine wa maendeleo wanapoitumia kuwaelezea masuala ya maendeleo mnaelewa na kufanya maendeleo zaidi? ………………………………….
   Kwa nini?
   ………………………………………………………………………………

7. Hebu zipange lugha za Kiswahili, Kiingereza, Kikamba na lugha nyinginezo kulingana na jinsi zinavyochangia kuleta maendeleo kutoka nambari 1 hadi 4
   1) …………………. 3) ………………….
   2) …………………. 4) ………………….

8. Hebu onyesha jinsi unavyoelewa maelekezo ya kimaendeleo lugha zifuatazo zinapotumika kufafanua masuala ya kimaendeleo

i. **Kikamba**
Vizuri kabisa ☐ Vizuri ☐ Sielewi kabisa ☐

ii. **Kiswahili**
Vizuri kabisa ☐ Vizuri tu ☐ Sielewi kabisa ☐

iii. **Kiingereza**
Vizuri kabisa ☐ Vizuri tu ☐ Sielewi kabisa ☐

iv. **Kiembu**
Vizuri kabisa ☐ Vizuri tu ☐ Sielewi kabisa ☐

v. **Kimaasai**
Vizuri kabisa ☐ Vizuri tu ☐ Sielewi kabisa ☐

vi. **Kikuyu**
Vizuri kabisa ☐ Vizuri tu ☐ Sielewi kabisa ☐

vii. **Lugha Nyingine ……….….……………**
Vizuri kabisa ☐ Vizuri tu ☐ Sielewi kabisa ☐

9. Je, unapendelea nyaraka za kimaendeleo zilizoandikwa vipi?
   1. Kikamba pekee ☐
   2. Kiswahili Pekee ☐
   3. Kiingereza Pekee ☐
   4. Kimaasai ☐
   5. Kikuyu ☐
   6. Kiembu ☐
   7. Zilizoandikwa na kutafsiriwa kwa lugha zote tatu ☐

Kwa nini?
…………………………………………………………………………………

***Sehemu C: Nafasi ya Mielekeo katika Uteuzi wa Lugha Maalumu ya Maendeleo***

1. Je, ni lugha gani unayopendelea kutumika katika kuelezea masuala ya maendeleo?

Kiingereza ☐ Kiswahili ☐ Lugha ya Mama ☐
Kwa nini?
…………………………………………………………………………

2. Lugha gani inapotumika katika maandishi na nyaraka za kimaendeleo unaelewa zaidi?

Kiingereza ☐ Kiswahili ☐ Lugha ya Mama ☐
Kwa nini?
…………………………………………………………………………

3. Kati ya lugha za Kiingereza, Kiswahili na lugha ya mama, ni gani iliyo ngumu kabisa kuelewa inapotumika katika kuelezea masuala ya maendeleo?
Kiingereza ☐ Kiswahili ☐ Lugha ya Mama ☐
Kwa nini?
…………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………

## KIAMBATISHO 2:

## DODOSO

***Ruwaza za Matumizi Lugha***

1. Je, Kaunti ya Machakos ina lugha ngapi? Unaweza kuzitaja?
   …………………………………………………………………….…………
2. Ni nini kinachosababisha uwepo na matumizi ya lugha?
   ……………………………………………………………………………
3. Je, ni lugha ngapi na zipi zilizo na umuhimu mkubwa kati ya hizi ulizozitaja katika jamii hii? Je zinatumika vipi (Zitaje kwa mpangilio kuanzia iliyo na umuhimu mkubwa zaidi hadi ile iliyo na umuhimu mndogo zaidi)
   ……………………………………………………………………………
4. Wewe kama mshidau mkuu katika masuala ya maendeleo ya kaunti unatumia lugha gani au zipi kati ya hizi ulizotaja katika kuwasiliana na wananchi na washikadau wengine wa kimaendeleo katika:
   a. Maeneo ya mashambani
   b. Maeneo ya mjini
   c. Mawasiliano ya washikadau wengine wa uundaji sera
   d. Mazungumzo rasmi

   ………………………………………………………………………………
5. Je, lugha hizi zinawasaidia vipi katika maingiliano na wananchi wa Kaunti ya Machakos?
   ………………………………………………………………………………

***Uhusiano kati ya lugha mbalimbali na maendeleo***

6. Watafiti wamesisitiza uhusiano kati ya lugha na maendeleo hata katika wingilugha. Je, lugha zinazounda wingilugha katika Kaunti ya Machakos zinahusiana na kuathiri vipi maendeleo?
   ………………………………………………………………………………
7. Ni lugha gani kati ya Kiingereza, Kiswahili na lugha za mama ambayo kwa maoni yako unaona inachangia kuleta maendeleo zaidi? ……………………………………………
   Ni gani ambayo unaona inapunguza kasi ya maendeleo?
   …………………………………
   Kwa nini?
   ………………………………………………………………………………
8. Kila lugha ina nafasi yake katika maendeleo. Kwa maoni yako, lugha za Kiingereza, Kiswahili, na lugha za mama zina nafasi gani katika maendeleo ya kaunti hii?
   ………………………………………………………………………………
   ………………….......................................................................................
9. Mnaposambaza sera za kimaendeleo mashinani, mnatumia lugha ipi?
   ………………………………………………………………………………
   Kwa nini?
   ………………………………………………………………………………
10. Je, na mnaposambaza sera hizi katika maeneo ya miji?
    …………………

Kwa nini?

………………………………………………………………………………

11. Mnasambaza sera hizi za kimaendeleo katika maeneo ya vizingasifa, mnafanyaje pale ambapo msemaji mmoja au zaidi ni wa kabila jirani (Mmaasai, Mkikuyu, Muembu, na lugha nyingine)

    ………………………………………………………………………………

12. Mnapokuwa na mikutano ya hadhara au umma, maafisa kilimo shambani nao hutumia lugha gani kufikia wakaazi wa lugha mbalimbali za Machakos?

    ………………………………………………………………………………

    Kwa nini?

    ………………………………………………………………………………

13. Je, mnawafikiaje wale wakaazi ambao hawajawahi kusoma?

    ………………………………………………………………………………

14. Je, mnatumia mikakati gani kuhakikisha kuwa kila mwananchi na mkazi wa Kaunti ya Machakos anazielewa sera za kimaendeleo kwa wakati unaofaa na kwa urahisi kabisa?

    ……………..………………………………………………………………

15. Katika mazingira ya wingilugha, tafsiri na ukalimani huwa ni jambo la muhimu ili kuhakikisha usawa kimaendeleo. Je, mnatumia vipi tafsiri na ukalimani katika mchakato wa kuunda sera za kimaendeleo na kuziwasilisha kwa wananchi?

    ………………………………………………………………………………

***Nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha***

16. Nchini Kenya, kwa mujibu wa katiba Kiswahili na Kiingereza ni lugha rasmi. Je ni gani unayoipenda katika kuendesha shughuli za kimaendeleo na kwa nini?

    ………………………………………………………………………………

17. Lugha ya Kiswahili imeonekana kuwa lugha ngumu katika utekezaji wa shughuli rasmi. Kwako wewe kama muundaji sera za kimaendeleo maoni yako ni yepi?

    ………………………………………………………………………………

18. Je, katika kuendelesha vikao vya uundaji sera unapenda kutumia lugha gani na kwa nini?

    ………………………………………………………………………………

19. Wakati mnapoandika nyaraka na jumbe maalum za kimaendeleo unapendelea lugha gani kutumika kati ya lugha za Kiswahili, Kiingereza na lugha za mama? Kwa nini?

    ………………………………………………………………………………

20. Kati ya lugha hizi zinazohusisha wingilugha ni gani ambayo ni ngumu kutumia kuundia na kuwasilishia sera?

    ……………………………………………………………………………….

    Kwa nini?

21. Kati ya lugha hizi zinazohusisha wingilugha ni gani ambayo ni rahisi kutumia kuundia na kuwasilishia sera?

    ………………………………………………………………………………

    Kwa nini?

22. Je, pale ambapo inatokea kuwa lugha iliyo rahisi kwenu kama waundaji sera haiwezi kutumika kufikia malengo mnayolenga, lugha badala huwa gani? Kwa nini?

    ………………………………………………………………………………

## KIAMBATISHO 3:

## MWONGOZO WA UCHUNZAJI

| | **Sokoni** | | **Nyumbani** | | **Mikutano** | | **Elimu ya Kilimo na Afya** | | **Hospitalini** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **K** | **Sn** | **K** | **Sn** | **K** | **Sn** | **K** | **Sn** | **K** | **Sn** |
| Kiswahili | | | | | | | | | | |
| Kikamba | | | | | | | | | | |
| Kiingereza | | | | | | | | | | |
| Lugha Nyingine | | | | | | | | | | |
| Kiswahili/Kikamba /Kiingereza | | | | | | | | | | |
| Kikamba/Kiswahili | | | | | | | | | | |
| Kiswa/Kiingereza | | | | | | | | | | |

**K –** Kidogo **Sn -** Sana


## KIAMBATISHO 4:

## KIUNZI CHA UCHANGANUZI WA NYARAKA

| | KIGEZO | MASUALA YA KUZINGATIA |
|---|---|---|
| 1 | Idara Maalumu | Data ya maendeleo idara zifuatazo za Kaunti hii:<br>1. Idara ya Biashara, Viwanda na Ubunifu,<br>2. Idara ya Kawi, Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Miji<br>3. Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi<br>4. Idara ya Utamaduni na Michezo |
| 2 | Serikali na Mashirika Mengine | • Data ya nyaraka rasmi za kaunti ya Machakos, serikali kuu, na mashirika mengine yaliyohalalishwa na kaunti ya Machakos<br>• Data kutoka kwa nyaraka za kipindi cha kutoka 2018 hadi sasa |
| 3 | Walengwa wa Maendeleo Husika | Data kutoka kwa nyaraka zinazolenga kuendeleza maendeleo ya kibinafsi ya wakaazi wa kaunti ya Machakos na maendeleo ya jumla ya kaunti nzima. |

## KIAMBATISHO 5:

## RAMANI YA KAUNTI YA MACHAKOS




*Chanzo: ResearchGate2022*

Kaunti ya Machakos

Kaunti jirani

## KIAMBATISHO 6:

## MAHOJIANO NA MKUU WA IDARA YA UTAMADUNI

**Mtafiti**: *Kaunti ya Machakos ina lugha ngapi ambazo mmezitambua?*
**Mtafitiwa**: Kuna lugha ya Kiingereza ambayo ndiyo tunatumia sanasana katika mawasilisho ya kiofisi, kuna Kiswahili ambacho tunatumia pia katika ofisi katika mawasiliano na wananchi ambao hawajui lugha asili (Kikamba). Kwa hivyo tunatumia lugha tatu: Kiingereza, Kiswahili na Kikamba, ambacho ndicho lugha ya wenyeji wa hapa Machakos.
**Mtafiti**: *Na kwa jumla ni lugha ngapi kwa idadi zinazozungumzwa katika Kaunti hii?*
**Mtafitiwa**: Hiyo bado hatujatambua lakini Machakos iko karibu na Nairobi na hivyo kuna watu wa asilia mbalimbali ambao wanaishi huku Machakos, wengine wafanyikazi, wengine wafanyibiashara na hivyo kuna lugha nyingi zinazozungumzwa katika kaunti hii. Hata hivyo, kutoka na hilo swali umeniuliza nafikiri hiyo ni changamoto kwetu ndiposa tuweze kuchukua hatua ya kusajili lugha ambazo zinatumiwa katika kaunti hii ya Machakos. Hata hivyo, kwa kuzingatia walio wengi na lugha zinatumika hapa, ninaweza kusema kuna Kigikuyu, Kiembu, Kimeru, Kimaasai, Kisomali na pia Kiarabu kwa sababu kuna Waislamu wengi.
**Mtafiti**: *Watu hawa wa jamii nyingine wanaletwa katika Kaunti ya Machakos na nini?*
**Mtafitiwa**: Wengine ni kazi, wengine ni wafanyibiashara kama vile Wasomali, wengine ni masomo, wengine wamenunua shamba na kuhamia kuishi huku, na wengine ni ndoa.
**Mtafiti***: Umetangulia kusema kuwa lugha za Kiingereza na Kiswahili ndizo zinazotumika katika mazingira rasmi na Kwamba Kikamba hutumika ila si sana. Kati ya hizi ni gani inayotumika zaidi kati ya hizi na ni gani inayoifuata kwa matumizi?*
**Mtafitiwa:** Kikazi na katika shughuli rasmi na wafanyikazi wengine ni lugha ya Kiingereza inayotumika zaidi lakini katika mawasiliano yasiyorasmi na kuwahudumia wananchi ni Kiswahili kwa sababu inawezekana kuwa hawajui Kiingereza vizuri ama Kikamba. Ingawaje tunatumia Kiingereza sana hasa katika nyaraka na mawasiliano rasmi, katika mazungumzo ya mdomo ni Kiswahili kwa sababu hata nikikutana na watu kwa mazingira yasiyo rasmi huwaongelesha Kiswahili na si Kiingereza ama Kikamba hata kama ni Mkamba hasa nikiwa simjui. Hata katika ofisi tunapendelea kutumia Kiswahili zaidi kwa sababu ndiyo inayowaunganisha watu wengi zaidi. Hata hivyo tutatumia lugha kulingana na muktadha au mtu au watu tunaozungumza nao.
**Mtafiti:** *Na je pale ambapo kuna watu wasioelewa Kiswahili mnafanyaje?*
**Mtafitiwa:** Katika hali kama hiyo tunamuuliza lugha anayoielewa na tunapopata ni Mkamba tunatumia Kikamba na iwapo si Mkamba tutafuta katika ofisi yetu ama nyingine mtu anayeelewa lugha yake atafsiri. Katika vibandiko na nyaraka, kama vile hospitalini, inabidi kutumia lugha za Kiingereza, Kiswahili, na Kikamba ili ujumbe huo ufike kwa watu wote.
**Mtafiti:** *Je mnatumia lugha vipi katika vizingasifa (mipakani na watu wasio Wakamba)?*

**Mtafitiwa:** Katika maeneo ya mipakani yaliyo mijini kutokana na watu wa jamii mbalimbali tunatumia Kiswahili na Kiingereza sana lakini katika maeneo vizingasifa vya mashinani, utapata kuwa wengi wa wananchi wanaelewa lugha za jirani zao kwa sababu wameingiliana kwa muda mrefu na wamejifunza lugha za kila jamii na hivyo tunatumia Kikamba na nyakati zingine kuchanganya na Kiswahili. Tofauti ya maeneo ya mipakani ni katika Kaunti ya Kajiado kuliko na Wamaasai ambao uelewa wao wa Kikamba ni wa kiwango cha chini ikilinganishwa na maeneo tunayopakana na Wagikuyu na Aembu na katika eneo hili tunatumia Kiswahili zaidi.

**Mtafiti:** *Je, lugha zinazounda wingilugha katika Kaunti ya Machakos zinaathiri vipi utekelezaji wa maendeleo?*

**Mtafitiwa:** Katika mazingira rasmi na hasa ya ofisini ambako ndiko sera za lugha zinakoundiwa lugha ya Kiingereza huathiri uundaji sera kwa namna chanya ikilinganishwa na matumizi ya Kiswahili na Kikamba kwa sababu hata serikali kuu hutumia lugha hii katika utekelezaji wa maendeleo. Katika miktadha inayohusisha wananchi, lugha ya Kiingereza haitumiki sana kwa sababu baadhi ya wananchi ni wazee na viwango vya chini vya elimu na hivyo hawataelewa. Katika mazingira haya, hasa yale ya mashinani, lugha ya Kikamba hufanya wananchi waelewe mambo ya maendeleo kwa undani na kusababisha utekelezaji mwema wa maendeleo. Lugha ya Kiswahili pia huwa na nafasi nzuri katika utekelezaji wa maendeleo hasa katika mazingira ambayo yanahusisha watu wasioelewa kikamba kwa sababu inaleta usawazishaji wa wananchi wote katika mchakato huu. Athari chanya ya lugha ya Kiingereza katika maeneo ya Mashinani huwa pale tu mambo yanayowasilishwa yana dhana ambazo zinaeleweka vizuri katika lugha ya Kiingereza. Katika maeneo ya mijini, hali huwa tofauti kabisa kwa sababu lugha ya Kikamba huwa na athari hasi kwa utekelezaji wa maendeleo kutokana na uwepo wa watu kutoka jamii mbalimbali huku lugha za Kiswahili na Kiingereza zikiwa na athari chanya. Lugha nyingine pia huwa na nafasi katika utekelezaji wa maendeleo kwa sababu iwapo tutapata mtu ambaye hajui Kikamba, Kiswahili na Kiingereza, tunatafuta mtu ambaye anaelewa lugha yake ili kumhudumia au kutafsiri na iwapo katika ofisi yetu hakuna tunatafuta katika ofisi zingine.

**Mtafiti:** *Katika kutoa huduma kwa wananchi wote, tafsiri na ukalimani ina nafasi gani?*

**Mtafitiwa:** Suala la tafsiri na ukalimani bado hatujaliingilia sana kwa sababu wananchi wote hata wale wa mashinani wanajua Kiswahili hata kama ni kidogo. Ukalimani sanasana unatokea sana makanisani. Kwa upande wa tafsiri, tunatafsiri nyaraka wenyewe na hasa katika hatua ya ushirikishaji umma katika mchakato wa maendeleo ambapo iwapo ni nyaraka rasmi ya serikali ya kitaifa au kaunti, huwa imeandikwa kwa Kiingereza na hivyo tunawasomea tukitafsiri kwa sababu hatuna wataalamu wa kutafsiri na pale palipo na haja kuu tunakodi huduma za tafsiri kutoka kwa wataalamu. Vilevile, tunatumia vyombo vya habari, hasa mno vile vya Kikamba, kutafsiri ujumbe huu kwa wananchi. Kile ambacho tumefanya katika Kaunti ya Machakos ni kufunza mtu wa lugha ya ishara ili kusaidia katika mawasiliano na watu wasioweza kuzungumza.

**Mtafiti:** *Kuna watu wanaosema kuwa Kiswahili ni lugha ngumu katika mazingira rasmi na kuwa lugha ya Kikamba ni ngumu kusoma maoni yako ni yepi?*

**Mtafitiwa:** Kiswahili ni lugha ngumu kwa sababu kinabadilikabadilika kwa kuwa mimi nilisoma Kiswahili hadi mwaka wa kwanza wa chuo kikuu lakini

kile Kiswahili kinachozungumzwa leo kama sanifu siwezi kukielewa. Kila uchao kinaendeleo kuwa kigumu kwa sababu hata ninaposikiliza kipindi cha Longa Longa katika Runinga ya citizen, maneno yanayoongelelewa pale sijawahi yasikia kabisa. Hivyo, Kiswahili kitaendelea kuwa kigumu kwa sababu ya hili. Kwa hakika lugha ya Kikamba nayo ni ngumu katika maandishi kwa sababu ya jinsi maneno yake yanavyoendelezwa lakini kwangu mimi ninajua kukisoma lakini kukiandika si sana.

**Mtafiti:** *Kwa maoni yako, unaona wingilugha unaathiri vipi utekelezaji wa maendeleo?*

**Mtafitiwa:** Kulingana na vile ambavyo tumetumia lugha nyingi katika Kaunti ya Machakos, nitasema kuwa matumizi ya lugha hizi yanasaidia sana katika utekelezaji wa maendeleo kwa sababu yanawezesha kufikisha ujumbe wa maendeleo kwa kila mwananchi, awe wa jamii yoyote, kiwango chochote cha elimu, jinsia yoyote, umri wowote na awe anafanya kazi yoyote.

## KIAMBATISHO 7:

## MAHOJIANO NA MKUU WA KITENGO CHA MIMEA – IDARA YA KILIMO, UFUGAJI NA UVUVI

**Mtafiti:** *Kaunti ya Machakos ina lugha nyingi zinazotumiwa. Je katika usambazaji wa sera za maendeleo mnatumia lugha vipi katika maeneo ya vizingasifa vya mijini na vya mashinani?*

**Mtafitiwa:** Katika maeneo ya mjini utapata kuna watu wa kila aina na hivyo tunachanganya lugha zote tatu lakini mashinani ambapo Wakamba huwa takriban asilimia 90 tunatumia Kikamba sana na kuchanganya na Kiswahili pale panapohitajika. Katika maeneo haya ya mashinani tunatumia Kikamba na Kiswahili lakini kama ni masomo ya kilimo utapata kuna maneno maalumu ambayo hayajulikani kwa Kikamba ama Kiswahili na hivyo tunatumia Kiingereza. Vilevile, mawasiliano yanapotoka ofisini katika nyaraka au katika mitandao ya kijamii tunatumia Kiingereza lakini inapofika katika kiwango cha kuwasilisha kwa wananchi tunalazimika kutafsiri ujumbe husika kwa njia ya mdomo kwa lugha za Kikamba au Kiswahili ili walengwa waelewa. Kwa mfano tunaweza kupata maelekezo ya kuwa ni msimu wa kupanda na kuwa wakulima wanahitaji kupanda mbegu fulani kutumia mbolea maalumu na yote ni kwa Kiingereza. Wakati tunapowasilisha ujumbe huu kwa wakulima hasa wa mashinani inalazimu tutumie lugha za Kikamba au Kiswahili yenye itaweza kueleweka vizuri. Hata hivyo, katika mazingira haya pia tunachanganya lugha katika mafunzo ya kilimo na Kiingereza hutumika kwa sababu kuna baadhi ya maneno ambayo tafsiri yake kwa Kiswahili na Kikamba haipo kama vile mbolea ya DAP na DAN.

**Mtafiti:** *Mnachanganya lugha hizi kwa namna gani?*

**Mtafitiwa:** Tumebahatika sana kuwa na wakulima ambao wameenda shuleni na kufikia aghalau kidato cha nne au darasa la nane. Katika maeneo ya mjini na yanayokaribiana na ya mjini, tunachanganya lugha za Kikamba, Kiswahili na Kiingereza na wakulima wote wanaelewa. Hata hivyo, bado tuna wale wazee ambao huhitaji kufikiwa kwa lugha ya Kikamba ambayo ndiyo wanayoielewa zaidi. Hali hii hupelekea matumizi mapana ya lugha ya Kikamba na Kiswahili kutumika tu pale ambapo panahitajika. Huko Mashinani unaweza kwenda na kwa sababu wewe unashughulika na masuala maalumu uzungumze kwa Kiingereza lakini mwisho wa siku utapa ya kwamba asilimia ndogo kabisa ndio walielewa ulichokuwa ukisema kwa sababu ya kikwazo cha kilugha. Katika maeneo ya mipakani na jamii zisizo za Wakamba, kutegemea kiwango cha wananchi cha elimu tunaweza kutumia Kiswahili. Hata hivyo, katika maeneo haya ya mashambani takriban 90% ya wananchi ni Wakamba na katika maeneo vizingasifa, hata wale watu wa jamii jirani wamejifunza Kikamba na hivyo wanatumia Kikamba bila tatizo lolote.

**Mtafiti:** *Na je katika mazingira rasmi ya ofisini na nyaraka rasmi?*

**Mtafitiwa:** Katika mikutano rasmi nyakati zingine tunabebwa na lugha yetu na tunaongea Kikamba. Hata hivyo katika mikutano, itategemea kiwango na aina ya mkutano. Iwapo mkutano unahusisha maafisa wa serikali ofisini, Kiingereza hutumika zaidi na pengine kuchanganya na Kiswahili kidogo lakini kama ni mkutano na washikadau wengine kama vile wawakilishi wa wakulima tunatumia lugha za Kiswahili, Kiingereza na Kikamba ili waweze kijieleza kwa lugha

wanayoipenda na kuielewa zaidi. Hata hivyo, katika maandishi ni Kiingereza pekee kinachotumiwa Vilevile katika utekelezaji wa maendeleo ni lazima kuwepo na kushirikisha umma na hivyo tunapoenda kule, maafisa wa serikali watatumia lugha kulingana na maeneo husika. Iwapo ni mashinani tutatumia Kikamba na Kiswahili kwa upana lakini iwapo ni mijini tunatumia Kiswahili na Kiingereza zaidi japo tunawapea wananchi uwezo wa kujieleza kwa lugha wanayoielewa zaidi.

**Mtafiti:** *Lugha hizi zinazounda wingilugha huu zinaathiri vipi utekelezaji wa maendeleo?*

**Mtafitiwa:** Lugha ya Kiingereza huwa bora zaidi katika mawasiliano na wasimamizi wa kilimo katika viwango vya eneobunge na wadi kwa sababu baadhi yao si Wakamba na pia hawajazoea Kiswahili sana. Vilevile iwapo ni nyaraka zinazohusisha mawasiliano, lugha ya Kiingereza ndiyo hufanikisha mawasiliano hata kwa wananchi kwa sababu mfumo wa kuwasiliano kuhusu masaa na siku za wiki hueleweka kwa haraka na kwa usahihi kabisa kwa lugha ya Kiingereza ikilinganishwa na Kiswahili. Lugha za Kiswahili na Kikamba nazo husaidia utekelezaji wa maendeleo zaidi pale ujumbe unapopitishwa kwa njia ya mdomo kwa wananchi katika maeneo ya mashinani muktadha ambao Kiingereza huwa na athari hasi kwa utekelezaji wa maendeleo. Katika maeneo ya mijini hali ni tofauti kidogo kwa sababu lugha za Kiswahili na Kiingereza ndizo zinazochangia pakubwa utekelezaji wa maendeleo huku Kikamba na lugha nyingine zikipunguza kasi ya maendeleo. Hata hivyo, miongoni mwa vijana katika maeneo ya mijini lugha ya Kiswahili inaweza kuathiri maendeleo kwa njia hasi au kupunguza kasi ya utekelezaji maendeleo kutokana athari za Sheng' inayosababisha Kiswahili rasmi kutopitisha ujumbe unaolengwa jinsi inavyofaa.

**Mtafiti:** *Umetaja kuhusu miradi ya maendeleo. Katika Kaunti ya Machakos mna miradi gani mnayotekeleza?*

**Mtafitiwa:** Katika Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi tuna miradi ambayo tunaendelea kutekeleza ambayo ni Small Scale Irrigation and Value Addition (SIVAP), Kenya Cereal Enhancement Program- Climate Resilient Agriculture for Livelihood (KCEP-CRAL), Agriculture Sector Support Program II (ASSP II) na Kenya Climate Smart Agriculture Project (KCSAP). Katika miradi hii yote tunatumia mbinu ya vikundi na hatushirikishi mhusika mmoja. Katika miradi hii kuna masomo katika kila hatua ambayo huwapa wanavikundi mafunzo ya stadi za kutekeleza shughuli maalumu kila hatua.

**Mtafiti:** *Katika miradi hii, tafsiri na ukalimani zina nafasi gani?*

**Mtafitiwa:** tafsiri kwa nyaraka zilizo na maagizo na maelekezo maalumu ya maendeleo. Hata hivyo, watu wengi hawapendi kusoma kwa sababu kunaweza kuwa na ujumbe muhimu katika nyaraka lakini watu wasiusome kwa sababu wanapenda maelezo ya moja kwa moja kupitia mdomo. Katika Kaunti ya Machakos, inatulazimu kutumia njia ya maelezo ya moja kwa moja na kuwaonyesha kwa vitendo sana na nyaraka chache katika lugha ya Kiingereza na chache mno kwa Kiswahili. Pia, ujumbe wa nyaraka husika huwasilishwa kupitia kwa vyombo vya habari ambavyo pia hutafsiri ujumbe maalum kwa lugha mbalimbali. Katika maelezo haya ya mdomo, tunatumia lugha zote tatu na hata kukalimani pale ambapo panahitajika ili watu waelewe kwa usahihi.

**Mtafiti:** *Katika ya lugha ya Kiswahili na ya Kiingereza, ni gani unayoipenda zaidi na kwa nini?*

**Mtafitiwa:** Ni Kiingereza kwa sababu ya mafunzo ambayo nimepata kwa sababu mara ya mwisho kutumia Kiswahili kwa makini ni katika mtihani wa kidato cha nne ambapo nilifanya mtihani na kupita. Jambo hili limenifanya kupenda Kiingereza zaidi kuliko Kiswahili na hasa katika mazingira rasmi kwa sababu nimekitumia sana katika mazingira ya chuo kikuu na hata kazini.
**Mtafiti:** *Kuna watu wanosema kuwa Kiswahili ni lugha ngumu na kusoma Kikamba ni vigumu. Hali kwako ni ipi?*
**Mtafitiwa:** Hili ni suala la mielekeo kwa sababu kila mwananchi huzungumza Kiswahili lakini inapofika masuala rasmi wanakwepa. Kwa mfano, kwa upande wangu nazungumza Kiswahili lakini nikiambiwa niandike barua sitaweza kwa maana itakuwaje kwamba naandikia mkubwa wangu wa eneo bunge barua kwa Kiswahili kumualika katika mafunzo. Nitaanza vizuri lakini nitapotea kwa njia na itanilazimu nichukue kamusi inisaidia na ikishindikana kabisa nitatumia Kiingereza. Kwa upande wa kusoma Kikamba, ni ukweli. Ni ukweli kabisa kuwa Kikamba ni kigumu sana katika maandishi.
**Mtafiti:** *Kwa maoni yako ya jumla, unaona wingilugha unaathiri vipi mchakato wa utekelezaji maendeleo?*
**Mtafitiwa:** Wingilugha una athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo kwa sababu unaondoa vikwazo vya kimawasiliano na kusaidia wakulima kuelewa mafunzo sawa na kupanua soko ya mazao yao.

## KIAMBATISHO 8:

## MAHOJIANO NA MKUU WA IDARA YA BIASHARA

**Mtafiti:** *Nchini Kenya hakuna sera ya matumizi ya lugha. Je mnatumia lugha zinazounda wingilugha Machakos vipi katika kutekeleza maendeleo?*
**Mtafitiwa:** Inategemea kwa sababu Machakos kuna sehemu za mjini na zingine za mashinani, ambako watu wengi ni Wakamba au wana uwezo wa kuongea Kikamba. Hivyo tunatumia lugha kutegema na mazingira maalumu. Tunapotaka kuwafikia wananchi mijini, sanasana tunatumia lugha rasmi, Kiswahili na Kiingereza lakini mashinani ambako watu wengi wanaongea lugha za mama tunatumia Kikamba. Tunatumia lugha kutegema mazingira na wasikilizaji. Katika maeneo ya mashinani pia, kabla ya kuanza mkutano, huwa tunauliza kama yupo mtu asiyeelewa Kikamba na tunapopata mmoja inalazimu tutumie Kiswahili ili tueleweke na kila mmoja na nyakati nyingine kuchanganya Kiswahili na Kikamba kwa sababu maeneo kama haya huwa pia na watu ambao hawaelewi Kiswahili. Iwapo tunapata hali kama hii, tunatumia lugha moja kisha kutafsiri kwa ile nyingine mara hiyo tu. Kwa mfano, iwapo ni mimi nazungumza nao, naeleza kwa Kikamba kisha kutafsiria wasioelewa Kikamba kwa Kiswahili
**Mtafiti:** *Katika maeneo haya ya mjini mnatumia aje lugha hizi za Kiswahili na Kiingereza?*
**Mtafitiwa:** Tunanchanganya lugha hizi kwa sababu nimeona kwamba Kiswahili ni lugha ngumu kwa watu wengi na si kila mtu anaweza kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha pasipo na kuchanganya na Kiingereza.
**Mtafiti:** *Kuna wasomi na watafiti ambao wameonyesha kuwa maendeleo hutegemea lugha sana kwa sababu lugha ni rasilimali kubwa. Je, lugha zinazounda wingilugha katika Kaunti ya Machakos zina nafasi gani kwa utekelezaji wa maendeleo?*
**Mtafitiwa:** Zina nafasi kubwa kwa sababu tunapotaka kuchukua maoni kutoka kwa wananchi kuhusu maendeleo lazima tutumie lugha wanayoielewa ili maendeleo husika yafikiwe. Ninaweza kufananisha lugha na gari inayobeba mambo yote yanayohusika katika mchakato wa utekelezaji wa maendeleo Kwa mfano katika siasa ambazo zimetamatika tu hivi majuzi wanasiasa walitumia kaulimbiu kwa lugha ya mama ili wawafikie watu vizuri na waweze kuelewa. Mfano mzuri ni gavana mpya wa Kaunti ya Machakos ambaye alitumia kaulimbiu iliyosema kuwa "*Mbesa Muvuko, Liu Mesani"* ambayo ni ya kimaendeleo.
**Mtafiti:** *Katika maeneo ya mashinani, lugha za Kikamba, Kiswahili na Kiingereza zinaathiri vipi utekelezaji wa maendeleo?*
**Mtafitiwa:** Mara nyingi ukiongelesha wananchi kwa lugha wasiyoielewa unatengeneza kikwazo, hali ambayo inaletwa na matumizi ya lugha ya Kiingereza katika maeneo haya lakini unapotumia lugha wanayoielewa kama vile Kikamba wanaelewa na kushiriki katika machakato wa utekelezaji maendeleo sana. Kwa upande mwingine, lugha ya Kiswahili ndiyo huwaunganisha watu wa makabila tofautitofauti katika maneneo ya mashinani na hata mijini na huwa na athari chanya hasa pale ambapo watu wanazungumza lugha tofautitofauti. Hivyo, lugha za Kikamba na Kiswahili mara nyingi huwa na athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo huku Kiingereza kikiwa na athari hasi.

**Mtafiti:** *Na je katika maeneo ya mijini?*
**Mtafitiwa:** Hali huwa tofauti kabisa na kinyume cha mashinani kwa sababu ukizungumza kwa lugha ya Kikamba itawaacha watu wengi sana nje ya mchakato wa utekelezaji wa maendeleo kwa sababu watu ambao hawaelewi Kikamba watakuona kama mkabila, watakuchukia na hata kukuona kama mshamba. Hata hivyo, unapozungumza kwa Kiswahili watu wote wanaelewa hata wale wazee kutokana na mazingira haya ya mjini. Itategemea pia na hadhira yako kwa sababu iwapo unazungumza na wazee mara nyingi wanapenda lugha za mama tofauti na vijana ambao wanapenda lugha za Kiswahili, Kikamba na Sheng' hivyo miongoni mwa wazee lugha za mama zitaleta athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo lakini athari hasi miongoni mwa vijana. Kwa upande wa vijana lugha za mama zitakuwa na athari hasi ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng' ambazo zitaleta athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo. Hali hii ni sawa pia na huko mashinani.
**Mtafiti:** *Umetaja kuwa Sheng' inatumika miongoni mwa vijana katika maeneo ya mjini. Je mnaitumia vipi katika maeneo haya mnapotekeleza maendeleo?*
**Mtafitiwa:** Hatutumii lugha ya Sheng' katika mikutano na shughuli za maendeleo kwa sababu haijatambuliwa kama lugha rasmi au ya taifa na pia haieleweki na watu wote hasa wazee. Ijapokuwa lugha hii ina uwezo wa kuathiri maendeleo, itategemea hadhira inayolengwa na maendeleo husika. Iwapo hadhira ni wazee basi Sheng' italeta athari hasi kwa utekelezaji wa maendeleo lakini iwapo ni vijana utekelezaji wa maendeleo utaathirika kiuchanya.
**Mtafiti:** *Je katika kutumia nyaraka kupitisha ujumbe maalumu wa kimaendeleo mnatumia lugha vipi?*
**Mtafitiwa:** Mara nyingi huwa ni lugha ya Kiingereza na chache kwa lugha za Kiswahili na Kikamba. **Mtafiti:** *Nimatambua kuwa wananchi wanapenda nyaraka zilizotafsiriwa kwa lugha tofautitofauti. Mnatumiaje mbinu hii katika nyaraka katika idara yenu?*
**Mtafitiwa:** Katika idara yetu hatutumii nyaraka zilizotafsiriwa kwa sababu kama ni ujumbe tunaupitisha wenyewe kwa njia ya mdomo kwa wananchi lakini katika masuala ya afya nyaraka na maandishi yataweza kuwa katika lugha za Kiingereza, Kiswahili na nyakati zingine Kikamba. Matumizi haya ya maelezo ya mdomo yanasababishwa na hali kuwa katika mchakato wa maendeleo ni lazima kuwashirikisha wananchi kabla ya kuanza mradi wa maendeleo na katika kuutekeleza na hivyo kulazimisha tuwaeleze na kuchukua maoni yao na mawasiliano ya mdomo ndiyo bora kwa jukumu hili.
**Mtafiti:** *Lugha ya Kiswahili imeonekana kuwa lugha ngumu? Unaionaje wewe?*
**Mtafiti:** Lugha ya Kiswahili ni lugha tamu ukipatana na mtu ambaye anaizungumza kwa namna sanifu unaifurahia. Kwa hivyo, kwangu mimi ni lugha safi, tamu na ya kutukuzwa. Hata hivyo, matumizi yake katika mazingira rasmi huwa changamoto miongoni mwa baadhi ya watu lakini kwangu si changamoto kubwa.
**Mtafiti:** *Lugha ya Kikamba kwa watu wengi ni ngumu kusoma. Kwako wewe hali ni ipi?*
**Mtafitiwa:** Ni ukweli kuwa sio watu wengi wanaoweza kusoma Kikamba kwa njia inayostahili na nafikiri ni kwa sababu ya namna inavyoandikwa kutokana na kuwa na vokali nyingi kuliko Kiswahili na Kiingereza. Hata kwangu na watoto wangu lugha ya Kikamba ni ngumu.
**Mtafiti:** *Katika mikutano rasmi, ni lugha gani unayopenda kuitumia zaidi?*

**Mtafitiwa:** Mimi ninapenda lugha zote na nina uwezo wa kuzizungumza kwa ufasaha na hivyo nitatumia lugha husika kulingana na hadhira yangu.

**Mtafiti:** *Kwa kumalizia, wingilugha una athari gani katika utekelezaji wa maendeleo katika Kaunti ya Machakos?*

**Mtafitiwa:** Kutokana na tajriba yangu, wingilugha unaathiri utekelezaji wa maendeleo kwa njia nzuri kwa sababu unahakikisha kuwa kila mwananchi ameshirikishwa katika utekelezaji wa maendeleo. Athari hasi itatokea pale tu lugha zinazounda wingilugha zinapotumika kuwabagua watu katika mchakato wa kutekeleza maendeleo.

## KIAMBATISHO 9:

## MAHOJIANO NA MKUU WA IDARA YA NYUMBA NA UKUAJI WA MIJI

**Mtafiti:** *Nchini Kenya hakuna sera ya lugha ya Kitaifa na Machakos kuna wingilugha. Mnatumiaje lugha husika kwa utekelezaji wa maendeleo; hebu zitaje kulingana na umuhimu wake?*

**Mtafitiwa:** Tunatumia lugha kulingana na mazingira ambayo tumo. Tukiwa maeneo ya mashinani tunatumia Kikamba sana, kikifuatiwa na Kiswahili na kama tutatumia Kiingereza itakuwa kidogo sana kwa sababu wengi wa wananchi ni Wakamba na hata kama si Wakamba, hasa katika maeneo ya mipakana na jamii nyingine wamejua Kikamba kutokana na kukaa hapo kwa muda mrefu. Tukiwa katika mazingira ya Mijini, hali hubadilika kwa sababu tunatumia Kiswahili zaidi kikifuatiwa na matumizi ya Kiingereza na iwapo Kikamba kitatumika kitatumika kidogo sana kwa sababu katika maeneo haya kuna watu ambao si Wakamba na hawaelewi Kikamba kabisa. Mfano mzuri ni eneo la Mlolongo ambako kuna jamii nyingi ambazo zinaishi huko, ikilinganishwa na mjini Machakos, tunapotekeleza miradi kama ununuzi wa mashamba, utengenezaji wa barabara na usafishaji kupitia kwa uokotaji takataka, tunatumia lugha kulingana na maeneo hayo maalumu.

**Mtafiti:** *Wewe kama mshikadau wa maendeleo, unatumia lugha ipi au zipi katika mawasiliano na wananchi na washikadau wengine katika maeneo ya mashinani, mijini na vizingasifa?*

**Mtafitiwa:** Nianze kwa kusema kuwa mimi si Mkamba. Katika maeneo ya mashambani lugha inayotumiwa sana ni Kikamba lakini wakati ninapozungumza na wananchi ninatumia Kiswahili zaidi na kuchanganya na Kiingereza pale ambapo kuna maneno maalumu. Iwapo nina maafisa wenzangu Wakamba nazungumza kidogo na kuwaachia wazungumze na wananchi kwa Kikamba huko mashinani kwa sababu kuna utamu wa kutumia na kusikiliza mambo kwa Kikamba miongoni mwa wananchi kutokana na umri wa wazee na makamo kuwa wengi zaidi katika maeneo haya. Tukija mijini, mimi ninatumia Kiingereza zaidi na kuchanganya na Kiswahili katika utekelezaji wa miradi ya barabara kwa sababu ukweli ni kwamba hatujaweka juhudi za ukuzaji wa Kiswahili kwa sababu tulilelewa na Kiingereza jambo ambalo limesababisha Kiswahili kutowekewa mkazo kama ilivyo lugha ya Kiingereza na Kikamba. Katika maeneo ya Vizingasifa, hasa ya mashinani, tunaipa lugha ya Kiswahili kipaumbele kutokana na uwezekano wa kuwepo na watu wa jamii nyingine wasioelewa Kikamba. Hata hivyo, kutokana na ujirani kwa muda mrefu unapata kwamba wengi wa wananchi hata wale wasio Wakamba wanaelewa Kikamba kwa sababu wamejifunza.

**Mtafiti:** *Watafiti wamesisitiza uhusiano wa karibu sana kati ya lugha na maendeleo. Je lugha zinazounda wingilugha katika Kaunti ya Machakos zinaathiri vipi utekelezaji wa maendeleo?*

**Mtafitiwa:** Ni ukweli kuwa lugha ni kigezo muhimu katika utekelezaji wa maendeleo na huathiri utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Katika eneo hili na hasa maeneo ya mshinani, kumekuwa na miradi ambayo imekataliwa na wananchi lakini walipoelezewa kwa Kikamba wakaelewa kabisa, kuikubali na hata kushiriki katika miradi hiyo jambo ambalo lugha za

Kiingereza na Kiswahili zilishindwa kufanya. Katika hali hii, ni wazi kuwa lugha ya Kiingereza itafanya wananchi wasielewa kile kinachofanyika na nafasi yao katika miradi hii na hivyo katika maeneo ya mashinani lugha hii kuwa na uhusiano duni sana na maendeleo na hivyo kuwa na athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo. Kwa upande mwingine Kikamba ambayo ndiyo lugha asili kinahusiana kwa karibu sana na utekelezaji wa maendeleo na kuwa athari chanya kwa utekelezaji wa maendeleo. Kiswahili nacho huwa na jukumu maalumu katika maendeleo kwa sababu karibu watu wote wanaelewa Kiswahili katika kaunti hii na hivyo hutumika pia. Hata hivyo Kiswahili huwa na uhusiano wa karibu sana na maendeleo katika maeneo ya vizingasifa kwa sababu Kiswahili huhakikisha kuwa utekelezaji wa maendeleo unahusisha watu wote bila kubagua mtu wa jamii yoyote na hata katika mashinani ambako kunaweza kuwa na watu wa jamii nyingine. Katika maeneo ya mijini, uhusiano katika ya lugha ya Kikamba na maendeleo ni mdogo sana kwa sababu kuna watu wa jamii mbalimbali na hivyo Kikamba huwa na athari hasi kwa utekelezaji wa maendeleo katika maeneo ya mijini. Hata hivyo katika maeneo haya, lugha ya Kiswahili huwa na uhusiano wa karibu sana na utekelezaji wa maendeleo kwa sababu ni lugha inayoeleweka na watu wa umri wowote na kiwango chochote cha elimu na huathiri utekelezaji wa maendeleo kiuchanya zaidi ikilinganishwa na Kiingereza. Kiingereza hutumika lakini wakati mwingine kinaweza kubagua watu ambao hawajasoma sana na wale wazee ambao hawakielewi vizuri. Lugha ya Sheng' katika mazingira ya mjini inatumiwa sana hasa miongoni mwa vijana na wanaipenda sana hasa wale wa mitaani wanofanya uchuuzi na wanaofanya kazi katika sekta ya usafiri na hivyo miongoni mwao msimbo huu unawasaidia sana katika shughuli zao za kikazi na kila siku. Hata hivyo, hatupei Sheng' msisitizo katika mikutano rasmi na ya maendeleo kwa sababu haieleweki na watu wengi. Hata hivyo, iwapo tunazungumza na vijana pekee tunaweza kuchanganya kidogo na maneno machache ya Sheng' ili wahisi kwamba lugha yao ya mtaani inathaminiwa katika utekelezaji wa maendeleo. Hutumiwa sana katika mawanda ya burudani na mazungumzo ya mitaani tu.

**Mtafiti:** *Kuna maagizo na maelekezo ya utekelezaji wa maendeleo ambayo hupitishwa kupitia kwa nyaraka. Je katika idara yenu mnatumia lugha ipi au zipi katika nyaraka hizi?*

**Mtafitiwa:** Katika idara yetu hatutumii nyaraka zozote kwa sababu sisi tunaingiliana na wananchi moja kwa moja na iwapo kuna ujumbe maalumu ambapo uko katika maandishi tunawaelezea kwa njia ya mdomo. Iwapo kuna ujumbe kama huu, unakuwa umeandikwa kwa lugha ya Kiingereza lakini tunapoenda kuuwasilisha kwa wananchi tunautafsiri kwa Kikamba au Kiswahili kutegemea maeneo tunakouwasilisha.

**Mtafiti:** *Umetaja kuhusu tafsiri, je kwa maoni yako tafsiri na ukalimani zina nafasi gani katika utekelezaji wa maendeleo?*

**Mtafitiwa:** Tafsiri itahusisha tu pale kuliko na ujumbe maalumu kutoka kwa serikali na tunajitafsiria wenyewe wakati tunapozungumza na wananchi. Hata hivyo, ukalimani ndio unatumika sana katika kutekeleza maendeleo kwa sababu katika mikutano ya maendeleo hasa kule mashinani, mtu kama mimi ambaye sielewi Kikamba, huwa ninaandamana na maafisa wengine ambao ni Wakamba ili kuwasilisha sera husika kwa wananchi. Hata hivyo, pale ambapo sijaandamana na afisa wa asili ya Kikamba, ninawaomba wananchi kuteua mmoja wao anayeelewa lugha zote mbili ili kuwatafsiria kwa Kikamba ama kutumia wasimamizi wa wadi, vijiji na machifu. Iwapo kuna mawasiliano rasmi

kupitia kwa barua, tunatumia wasimamizi hawa wa wadi na wa vijiji na machifu ili kuwatafsiria wananchi ujumbe huo

**Mtafiti:** *Kiswahili ni lugha ngumu sana. Wewe unakiona Kiswahili aje?*

**Mtafitiwa:** Ni kweli Kiswahili ni lugha ngumu hasa katika mazingira rasmi. Kwangu mimi nilipenda Kiswahili sana lakini mwalimu wangu alifanya Kiswahili kuwa kigumu hadi kuwacha kukitumia. Vilevile ugumu huu wa Kiswahili unatokana na hali kwamba hatuweki mkazo matumizi ya lugha ya Kiswahili shuleni. Katika miktadha mingi, lugha ya Kiswahili inachukuliwa kama lugha duni kama vile kwenye mazungumzo katika runinga na hata maingiliano ya kawaida. Miongoni mwa vijana, Sheng' inaendelea kuchukua nafasi ya Kiswahili. Hata katika kiwango na utamaduni wa kitaifa, lugha ya Kiswahili haijakumbatiwa na mambo haya yanasababisha watu kukosa uzoefu wa kutumia Kiswahili na hivyo kuwa lugha ngumu. Hata katika vyombo vya habari huwa sisikilizi programu za Kiswahili kwa sababu zinakaa ngumu sana.

## KIAMBATISHO 10:

## MSETO WA NYARAKA YA KILIMO ILIYOANDIKWA KWA KIINGEREZA KATIKA UKURASA WA MBELE NA KUTAFSIRIWA KWA KISWAHILI UKRASA WA NYUMA








*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani)*

## KIAMBATISHO 11:

## NYARAKA YA MAELEKEZO YA KILIMO ILIYOANDIKWA KWA KIINGEREZA NA KUTAFSIRIWA KWA KISWAHILI




*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani)*

**KIAMBATISHO 12:**

**NYARAKA YA KILIMO ILIYOANDIKWA KWA KISWAHILI PEKEE**

**NA PICHA ZA UFAFANUZI**




*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani)*

**KIAMBATISHO 13:**

**MSETO WA NYARAKA YA MAELEKEZO YA KILIMO**


**ZILIZOANDIKWA KWA KISWAHILI**




*(Chanzo: Utafiti wa Nyanjani)*

**KIAMBATISHO 14:**

**IDHINI KUTOKA KWA CHUO**



**KAIMOSI FRIENDS UNIVERSITY**

Tel: 0773040235 / 0771373639
E-mail: dgs@kafu.ac.ke
Website: www.kafu.ac.ke

P.O Box 385
Kaimosi – 50309,
Kenya

**Office of the Director, Directorate of Graduate Studies**

**REG NO:** DGS/EDK/G/0002/2019

**Date:** 9th September, 2022.

**FROM: DIRECTOR, GRADUATE STUDIES**

**TO: WILLINGTON KILONZO PETER**

**RE: APPROVAL OF PROPOSAL**

This is to inform you that your research proposal titled '**Wingilugha na Athari zake kwa utekelezaji wa Maendeleo katika Kaunti ya Machakos, Kenya"** was approved by the **1st Senate** meeting of **6th September, 2022.**

You will work closely with the following approved supervisors in executing your research:

1. Dr. Nixon Sangili - Idara ya Lugha na Fasihi, KAFU
2. Dr. Solomon Aunga - Idara ya Lugha na Fasihi, KAFU

You will be expected to submit progress reports regularly to the Director, Graduate Studies. Do not hesitate to consult the undersigned on any matter pertaining to your studies. The Directorate of Graduate Studies wishes you success in your studies.

**Dr. B. R. Shiundu, PhD**

Director, Graduate Studies.

Copy to: Ag. Vice Chancellor
Ag. Deputy Vice chancellor, (A&SA)
Dean, SESS
Supervisors
Registrar, Academic Affairs

## KIAMBATISHO 15:

## IDHINI KUTOKA YA NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

NACOSTI

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 409327

Date of Issue: 20/September/2022

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Mr.. WILLINGTON KILONZO PETER of Kaimosi Friends University College , has been licensed to conduct research in Machakos on the topic: WINGILUGHA NA ATHARI ZAKE KWA UTEKELEZAJI WA MAENDELEO KATIKA KAUNTI YA MACHAKOS, KENYA for the period ending : 20/September/2023.**

License No: **NACOSTI/P/22/20398**

**409327**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**KIAMBATISHO 16:**

**IDHINI YA KAUNTI YA MACHAKOS**

REPUBLIC OF KENYA
COUNTY GOVERNMENT OF MACHAKOS
OFFICE OF THE COUNTY SECRETARY

Telephone: +254-202004086
Email: info@machakosgovernment.co.ke
countysecretary@machakosgovernment.co.ke

Machakos Highway
P.O Box 1996-90100
Machakos, Kenya.

*When replying please quote:*
OUR REF: GMC/2/CS/GEN/VOL.II/105

21st September, 2022.

To,

Willington Kilonzo Peter,
P.O Box 43,
MUUMANDU.

RE: RESEARCH PROPOSAL TITLED "WINGILUGHA NA ATHARI ZAKE KWA UTEKELEZAJI WA MAENDELEO KATIKA KAUNTI YA MACHAKOS, KENYA"

I trust this finds you well.

Reference is made to a letter dated 9th September 2022 from Dr. B.R. Shiundu PhD – Kaimosi Friends University on the above subject matter.

The request to carry out research in Machakos County is hereby approved.

Thank you.

COUNTY GOVERNMENT OF MACHAKOS
21 SEP 2022
OFFICE OF THE COUNTY SECRETARY

ROBERT MAITHA
Ag. COUNTY SECRETARY AND HEAD OF PUBLIC SERVICE